# UFORENSIKI KATIKA RIWAYA PENDWA YA KISWAHILI: MIFANO KUTOKA *MZIMU WA WATU WA KALE*, *MHANGA WA IKULU* NA *KIU YA HAKI*

**KOMBO FAKI JUMA**

**SHAHADA YA UMAHIRI KATIKA FASIHI YA KISWAHILI**

**CHUO KIKUU CHA DODOMA**

**OKTOBA, 2018**

# UFORENSIKI KATIKA RIWAYA PENDWA YA KISWAHILI: MIFANO KUTOKA *MZIMU WA WATU WA KALE*, *MHANGA WA IKULU* NA *KIU YA HAKI*

NA

KOMBO FAKI JUMA

TASNIFU KWA AJILI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UMAHIRI KATIKA FASIHI YA KISWAHILI YA CHUO KIKUU CHA DODOMA

CHUO KIKUU CHA DODOMA

OKTOBA, 2018

**IKIRARI**

**NA**

**HAKI MILIKI**

Mimi, **KOMBO FAKI JUMA,** ninathibitisha kwamba tasnifu hii ni kazi yangu asilia, na kwamba, haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada inayofanana na hii au nyingine yoyote.

Saini: ………………………………

Hairuhusiwi kuzalisha, kunakili, wala kusambaza sehemu yoyote ya tasnifu hii kwa namna yoyote bila kibali cha maandishi kutoka kwa mwandishi wa tasnifu hii au Chuo Kikuu cha Dodoma.

# ITHIBATI

Aliyesaini hapa chini anathibitisha kwamba ameisoma tasnifu hii inayoitwa: **Uforensiki katika riwaya pendwa ya Kiswahili: Mifano kutoka Mzimu wa Watu wa Kale Mhanga wa Ikulu na Kiu ya Haki**, na anapendekeza kwamba inafaa kukubaliwa na Chuo Kikuu cha Dodoma kwa ajili ya kukamilisha mahitaji ya Shahada ya Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili.

......................................

Dkt. Zuhura A. Badru

(Msimamizi)

Tarehe: ...............................

## SHUKURANI

Kama ilivyo kawaida, tasnifu hubeba jina la mtu mmoja, lakini ni matokeo ya michango na msaada wa watu wengi. Si kazi rahisi kuandika kwa undani mchango wa kila mtu aliyesaidia katika kufanikisha kazi hii. Hata hivyo, wafuatao wanastahili shukurani zangu za pekee.

Kwanza kabisa, ninamshukuru Mwenyezi Mungu muumba wa ulimwengu na vyote vilivyomo ndani yake kwa kuwa pamoja nami na kunipa afya njema, nguvu, uwezo, uelewa, akili, busara, maarifa na uvumilivu mkubwa katika kipindi chote cha masomo yangu.

Pili, ninatoa shukurani zangu za dhati kabisa kwa msimamizi wangu, Dkt. Zuhura Abdallah Badru, ambaye hakusita kunishauri katika hatua zote za uandishi wa kazi hii mpaka nilipoikamilisha.

Tatu, ninawashukuru wazazi, Bi. Time Mkadam Jabu na Bw. Faki Juma Mbwana, pamoja na mke wangu mpendwa kwa moyo wao wa uvumilivu na imani pamoja na kunitia moyo na ujasiri pale ambapo nilianza kukata tama juu ya jambo hili. Pia, shukrani zangu ziwaendee watoto wangu, pamoja na ndugu zangu wote katika familia walionisaidia kwa hali na mali katika kipindi chote cha masomo yangu. Mungu awabariki wote.

Nne, napenda pia kuzishukuru taasisi zilizosaidia katika kufanikisha utafiti huu. Nazo ni Chuo Kikuu cha Dodoma, Chuo Kikuu Cha Waislamu Morogoro, Taasisi ya upelelezi ya Polisi, Vituo vya huduma ya Sheria pamoja na Taasisi ya Afya Zanzibar. Pia, ninawashukuru watu wote walioshiriki na kusaidia katika kufanikisha ukusanyaji wa data za utafiti huu.

## TABARUKU

Kazi hii ninaitunuku kwa mke wangu mpendwa, Bi. Time M. Hamad, pamoja na watoto wangu, Fat-hia Kombo Faki, Husein Kombo Faki na Mur-shid Kombo Faki, kwa ushirikiano na uvumilivu wao mkubwa katika kipindi chote cha masomo yangu. Mwenyezi Mungu awape maisha marefu yenye kheri na awabariki sana. AMIIN.

## IKISIRI

Tasnifu hii inahusu Uforensiki katika riwaya pendwa ya Kiswahili. Lengo kuu lilikuwa kuchunguza ujitokezaji wa uforensiki katika riwaya pendwa ya Kiswahili, hususan kwenye riwaya teule ambazo ni *Mzimu wa Watu wa Kale*, *Mhanga wa Ikulu* na *Kiu ya Haki.* Pia, utafiti uliongozwa na malengo mahususi matatu ambayo ni kuchanganua matukio yanayosababisha kufanyika kwa uforensiki katika riwaya, kubainisha miktadha ambayo taaluma ya uforensiki inafanyika na kuchunguza uhusiano uliopo kati ya uforensiki katika riwaya na maisha halisi ya jamii.

Taarifa za awali zilikusanywa kwa njia ya udurusu wa maandiko na zile za upili zilitumia mbinu ya mahojiano. Sampuli ya utafiti iligawiwa katika sehemu nne ambazo ni riwaya tatu teule, wataalamu wa upelelezi pamoja na wanafasihi ya Kiswahili, wanafunzi wa fasihi ya Kiswahili vyuo vikuu na wahanga wa matukio ya uhalifu katika jamii. Sampuli ilipatikana kwa kutumia mbinu ya usampulishaji holela kwa kundi la wanafunzi na mbinu ya usampulishaji lengwa kwa riwaya teule na wataalamu kutoka katika taasisi mbalimbali. Aidha, ufafanuzi wa taarifa uliongozwa na Nadharia ya Uhalisia na mbinu ya ufafanuzi ndiyo iliyotumika katika uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo.

Matokeo ya utafiti yameonesha kuwapo kwa matukio ya kihalifu ambayo huhitaji kifanyiwa uforensiki. Baadhi ya matukio hayo ni mauaji na ujambazi. Pia, utafiti uligundua miktadha iliyohusishwa na uforensiki kama vile, muktadha wa polisi, muktadha wa kitabibu na muktadha wa kijamii. Aidha, utafiti umebaini kuwa uforensiki ni dhana mpya kwa wanajamii walio wengi. Pia, baadhi ya waandishi wa kazi za kifasihi hawakuizamia kwa kina taaluma hii ya uforensiki katika kazi zao kwa kule kutokuwa na ufahamu wa kutosha juu ya taaluma hiyo. Hivyo, waandishi hao hukitumia kipengele hiki cha kiforensiki kama kionjo tu cha kifani katika kazi zao bila kudhihirisha umuhimu wake kwa jamii na taifa kwa jumla.

## YALIYOMO


IKIRARI NA HAKI MILIKI ........ i
ITHIBATI ........ ii
SHUKURANI ........ iii
TABARUKU ........ iv
IKISIRI ........ v
YALIYOMO ........ vi
ORODHA YA VIFUPISHO ........ ix

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI ........ 1**
1.1 Ufafanuzi wa Dhana ........ 1
1.1.1 Uforensiki ........ 1
1.1.2 Riwaya ........ 1
1.1.3 Riwaya Pendwa ........ 2
1.1.4 Upelelezi ........ 3
1.1.5 Ushahidi ........ 4
1.1.6 Kipimo cha Vinasaba (DNA) ........ 5
1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti ........ 6
1.3 Tamko la Tatizo la Utafiti ........ 12
1.4 Malengo ya Utafiti ........ 13
1.4.1 Lengo la Jumla ........ 13
1.4.2 Malengo Mahsusi ........ 13
1.5 Maswali ya Utafiti ........ 13
1.6 Manufaa ya Utafiti ........ 14
1.7 Muhtasari wa Sura ya Kwanza ........ 14

**SURA YA PILI: MAPITIO YA MAANDIKO NA NADHARIA YA UTAFITI .... 15**
2.1 Utangulizi ........ 15
2.2 Maandiko kuhusu Riwaya za Kipelelezi ........ 15
2.3 Mapitio ya Maandiko Kuhusu Uforensiki ........ 18
2.4 Pengo la Utafiti ........ 19
2.5 Nadharia ya Utafiti ........ 20

2.5.1 Nadharia ya Uhalisia ........ 20
2.6 Muhtasari wa Sura ya Pili ........ 22

**SURA YA TATU: METHODOLOJIA YA UTAFITI ........ 23**
3.1 Utangulizi ........ 23
3.2 Usanifu wa Utafiti ........ 23
3.3 Walengwa wa Utafiati ........ 23
3.3.1 Jamii ya Watafitiwa ........ 24
3.3.2 Sampuli ya Watafitiwa na Upatikanaji Wake ........ 24
3.4 Eneo la Utafiti ........ 26
3.5 Itikeli za Utafiti ........ 27
3.6 Ukusanyaji wa Data ........ 27
3.6.1 Mbinu za Ukusanyaji wa Data ........ 28
3.6.1.1 Mahojiano ........ 28
3.6.1.2 Udurusu wa Maandiko ........ 29
3.6.2 Zana za Kukusanyia Data ........ 29
3.6.3 Mchakato wa Ukusanyaji wa Data ........ 29
3.7 Uhalali na Uthabiti wa Matokeo ya Utafiti ........ 30
3.8 Uchanganuzi wa Data ........ 30
3.9 Mipaka ya Utafiti ........ 31
3.10 Changamoto za Utafiti na Utatuzi Wake ........ 31
3.11 Mpango wa Tansifu ........ 32
3.12 Muhtasari wa Sura ya Tatu ........ 32

**SURA YA NNE: UWASILISHAJI NA MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI ........ 34**
4.1 Utangulizi ........ 34
4.2 Historia Fupi za Waandishi wa Riwaya Teule ........ 34
4.2.1 Historia Fupi ya Mwandishi Muhammed Said Abdulla (MSA) ........ 34
4.2.2 Historia Fupi ya Mwandishi Beka Mfaume ........ 37
4.2.3 Historia Fupi ya Mwandishi Zainab M. Mwanga ........ 39
4.3 Muhtasari wa Riwaya za Waandishi Teule ........ 39
4.3.1 Muhtasari wa Riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* ........ 39

4.3.2 Muhtasari wa Riwaya ya *Mhanga wa Ikulu* .................................................... 40
4.3.3 Muhtasari wa Riwaya ya *Kiu ya Haki* ............................................................ 42
4.4 Matukio Ambayo Husababisha Kufanyika kwa Uforensiki katika Riwaya Teule ........................................................................................................ 42
4.4.1 Tukio la Mauaji ........................................................................................ 44
4.4.2 Tukio la Wizi ............................................................................................ 52
4.4.3 Tukio la Ujambazi ..................................................................................... 55
4.4.4 Tukio la Utekaji Nyara .............................................................................. 57
4.4.5 Kutoa/Kupokea Rushwa ............................................................................ 60
4.5 Miktadha Ambayo Taaluma ya Uforensiki Inafanyika ..................................... 66
4.5.1 Muktadha wa Kipolisi ............................................................................... 69
4.5.2 Muktadha wa Mahakamani ........................................................................ 75
4.5.3 Muktadha wa Kitabibu .............................................................................. 77
4.5.4 Muktadha wa Kijamii ................................................................................ 79
4.6 Uhusiano Uliopo Kati ya Uforensiki katika Riwaya na Maisha Halisi ya Jamii ........................................................................................................ 82
4.6.1 Uhusiano wa Uforensiki Kimatukio katika Riwaya na Maisha Halisi ya Jamii ........................................................................................................ 83
4.6.2 Uhusiano wa Uforensiki Kimuktadha katika Riwaya na Maisha Halisi ya Jamii ........................................................................................................ 87
4.7 Muhtasari wa Sura ya Nne ........................................................................... 91

**SURA YA TANO: MUHTASARI, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO ......... 92**
5.1 Utangulizi ................................................................................................. 92
5.2 Muhtasari wa Utafiti ................................................................................... 92
5.3 Hitimisho .................................................................................................. 94
5.3.1 Mchango Mpya wa Utafiti .......................................................................... 94
5.3.2 Utoshelevu wa Nadharia Iliyotumika ............................................................ 95
5.4 Mapendekezo ya Tafiti Zijazo ...................................................................... 95
5.5 Muhtasari wa Sura ya Tano .......................................................................... 96
**MAREJELEO ............................................................................................. 97**
**VIAMBATISHO ........................................................................................ 100**

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| BAKIZA | Baraza la Kiswahili la Zanzibar |
| BBH | *Bahari Beach Hotel* |
| Bi. | Bibi |
| Bw | Bwana |
| C.I.D | *Criminal Investigation Department* |
| DNA | *Deoxyribo Nucleic Acid* (kipimo cha vinasaba) |
| DPP | *Director of Public Prosecutions* |
| MAKL | *Master of Arts in Kiswahili Literature* |
| MSA | Muhammed Said Abdulla |
| NIJ | *National Institute of Justice* |
| TUKI | Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahi |
| U.K | *United Kingdom* |
| UNESCO | *The United National Education Scientific and Cultural Organisation* |
| UWAKI | Ukatili wa Kijinsia |

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

Sura hii imeanza kwa kutoa ufafanuzi wa istilahi muhimu ambazo zimetumika katika tasnifu hii. Pia, tumeangalia usuli wa tatizo la utafiti, tamko la tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, pamoja na manufaa ya utafiti.

## 1.1 Ufafanuzi wa Dhana

### 1.1.1 Uforensiki

Uforensiki ni taaluma ya uchunguzi wa mashauri ya jinai kwa kutumia njia na nyenzo za kisayansi na teknolojia[1]. Taaluma hiyo ya uchunguzi hutumika ili kuweza kugundua na kuwapata wahalifu katika jamii. Neno '*forensic*' linalotokana na lugha ya Kilatini ambalo linamaanisha mali ya mahakama au mijadala na midahalo ya umma (Nabar, 2002).

### 1.1.2 Riwaya

Senkoro (1982:73-74) anafafanua maana ya riwaya kwa kusema, "Riwaya ni kisa changamano ambacho huweza kuchambuliwa kwa mapana na marefu kifani na kimaudhui". Riwaya ni kisa au mkusanyiko wa visa, vyenye urefu unaoviruhusu vitambe na kutambaa mahali pengi na kuambaa vizingiti vingi vya maisha kama apendavyo mwandishi wake. Hivyo basi, riwaya ni hadithi ndefu ya kubuni, yenye visa vingi, wahusika zaidi ya mmoja na yenye mazungumzo na maelezo yanayozingatia kwa undani na upana maisha ya jamii. Riwaya inatoa picha ya jumla ya maisha ya mtu toka nyumbani hadi katika kiwango cha taifa na hata dunia nzima.

[1] Muhadhara wa Dkt. Ponera kwa wanafunzi wa (MAKL) Chuo Kikuu cha Dodoma Mei, 24 2017.

### 1.1.3 Riwaya Pendwa

Madumulla (2009) anaeleza kuhusiana na riwaya pendwa kuwa, ni riwaya ambayo inajihusisha na masuala ya mapenzi, upelelezi, na ujasusi; ambapo, mara nyingi, katika ufuatiliaji wake kuna mapigano makali ya kimwili au kiakili kati ya mtu mmoja au wachache na watu wengi. Matokeo yake ni kwamba mtu mmoja anawashinda walio wengi. Aina hii ya riwaya imezua mjadala mkubwa juu ya kuwa inaangukia wapi, kati ya udhati, usahihi na uchapwa. Mlacha na Madumulla (1991: 58), wakimnukuu Arnold (1980) akifafanua dhana ya fasihi pendwa (*popular litrature*) wanasema kuwa:

> *Is the final analysis applied to what people need and aften want, and not to want they read because nothing else is available, or what they read because forces opposed to their true prosperity claim they want it.*
>
> Hatimaye inahusu kile ambacho watu wanakihitaji na aghalabu wanakitaka, na sio kile wakisomacho kwa sababu ya kutokuwapo kwa kitu kingine, au kile wakisomacho kwa sababu ya nguvu ambazo zinapingana na kile ambacho wanakitaka zinadai kuwa wanakitaka.

Katika nukuu hii tunaona kuwa Arnold anaizungumzia hali ya fasihi andishi yenye kulenga umma katika Tanzania ya miaka ya 1970. Anaona kuwa fasihi hii inahusu kile ambacho watu wanakihitaji. Hali hiyo aliiona kutokana na upokezi wa vitabu vya Mazungumzo ya Mchana na vingine vilivyohusu Mpango wa Elimu ya Ujamaa na Kujitegemea vilivyoandikwa na Msuya miaka ya sabini.

Riwaya pendwa ni mkondo unaojumuisha riwaya zote ambazo lengo lake kubwa ni kuburudisha na kusisimuwa wasomaji. Hivyo, hizi ni riwaya zinazotungwa kwa mtindo wa kifomula usiotatanisha sana, uliojaa taharuki ili zisomeke kwa urahisi (Mulokozi, 1996). Lengo hili hutimizwa kwa kusawiri visa na matukio ya kusisimua

damu. Riwaya pendwa zina mawanda yake makuu kama vile, uhalifu (mfano, wizi, mauaji, ujambazi, dhuluma, unyong'aji na uporaji), mapenzi, maelewano, ujasusi na upelelezi, (Madumulla 2009: 83). Baadhi ya sifa muhimu za riwaya hizi ni: kuwa na mtindo rahisi, kuenzi zaidi jinsia ya kike huwa na matumizi makubwa ya taharuki, mhusika wake mkuu huwa mhusika mkwezwa na mandhari yake huwa ya mijini zaidi kuliko vijijini. Katika nchi ya Tanzania, riwaya hizi kwa mara ya kwanza zilianzishwa na Muhammed Said Abdulla alipoandika kazi yake ya kwanza inayoitwa *Mzimu wa Watu wa Kale* (1960). Kisha akafuatiwa na Faraji Katalambula alipoandika riwaya ya *Simu ya Kifo* (1965).

### 1.1.4 Upelelezi

Upelelezi ni taaluma ya kutafuta mambo kwa siri. Ni hali au tabia ya kuchunguza jambo lisilokuhusu; udadisi, upekuzi, sachi (*Kamusi ya Kiswahili Sanifu,* 2004: 438). Shughuli ya upelelezi ilikuwepo kwa miaka mingi sana tokea binadamu anaanza kuishi duniani. Shughuli hii inabadilika kutokana na mabadiliko yanayosababishwa na ukuaji wa kimaendeleo ya jamii katika taaluma, kisiasa na kiuchumi. Kutokana na kukua kwa teknolojia, mbinu na vifaa mbalimbali hutumika kukusanya taarifa na kuacha njia na mbinu za asili za upelelezi ambazo hata kwa wakati huu zinaweza kuwa sahihi kabisa.

Yapo mambo muhimu yanayoambatana na hatua ya upelelezi. Miongoni mwa mambo hayo ni kama vile, hati ya kutiwa nguvuni, hati ya kupekuliwa, hati ya kuita shaurini, maelezo ya mshtakiwa na mashahidi, pia dhamana. Mara nyingi upelelezi unapoanza huwa kuna mtu anayetuhumiwa kwamba ndiye aliyetenda kitendo kilichosababisha kosa linalofanyiwa uchunguzi. Kunaweza kuwa na ushahidi wa

mazingira au hata wa moja kwa moja kwamba, mtu fulani ametenda kosa hilo. Mpelelezi ndiye anayehusika na kesi yenye kukusanya ushahidi wote huo. Iwapo ushahidi unaonekana kama kumwelemea na kumhusisha mtuhumiwa na kosa linalohusika, basi hufunguliwa mashtaka; naye huitwa mshtakiwa. Mashtaka huanza pale hati ya mashtaka dhidi ya mshtakiwa inapowasilishwa mahakamani, uamuzi sahihi wa kufunguliwa mashtaka mtuhumiwa hutegemea sana kiwango cha uwezo wa anayechukua uamuzi huo katika kuupima ushahidi uliopatikana katika upelelezi dhidi ya mtuhumiwa.

### 1.1.5 Ushahidi

Saffar (2006), akifafanua juu ya ushahidi anasema kuwa, "ni namna ambayo inatumika kuthibitisha au kukanusha ukweli wa jambo linalochunguzwa". Maelezo na ikirari za washtakiwa ni ushahidi pia[2]. Katika jitihada za kuthibitisha au kukanusha jambo fulani kuna hatari nyingi ambazo huweza kupotosha ukweli au haki. Ili kuepuka au kupunguza hatari kama hizo, zipo kanuni ambazo zinapaswa zifuatwe na wakati mwingine kutiliwa maanani tu kabla ya kuukubali au kuukataa ushahidi fulani. Ushahidi unaokubalika ni ule tu unaothibitisha jambo linalodaiwa kwa mujibu wa sheria. Mfano, ushahidi wa kuambiwa na mtu mwingine japo ni kweli haukubaliwi isipokuwa nyakati fulani fulani kama vile, katika kuthibitisha sababu ya kifo cha mhusika kutokana na kauli yake mwenyewe au ushahidi unaounga mkono maelezo ya shahidi fulani.

[2] Kwa ufafanuzi zaidi tazama sheria ya ushahidi Na. 6 ya 1967 ya Tanzania.

### 1.1.6 Kipimo cha Vinasaba (DNA)

Ni kifupi cha neno la Kiingereza "*Deoxyribo Nucleic Acid"*. Ashoka (2007) akieleza juu ya maana ya DNA, anasema kuwa, "*is the genetic material present in the cromosomes of our body cells*". Yaani, ni chembechembe za asili au viini tete vinavyopatikana katika seli za miili yetu (tafsiri yetu). DNA hutumika katika sayansi ya viumbe hai katika kuchunguza taarifa mbalimbali za utendaji wa mwili, tabia na hata suala zima la uzazi. Mbinu hii ya kutumia DNA katika uchunguzi, kwa mara ya kwanza, ilitumiwa na Alec Jeffrey wa Uingereza katika mwaka 1985. Kila binadamu ana mpangilio wa chembechembe za asili ambazo amezirithi kutoka kwa wazazi wake. DNA inapatikana kwenye damu kavu na damu ya majimaji, majimaji ya kiume, mifupa, unywele wenye mizizi, mate, kucha, vichungi vya sigara na vitu vinavyomilikiwa binafsi kama vile miswaki, nyembe zilizotumika na mavazi.

Kuna umuhimu mkubwa wa kuwapo kwa sheria ya kusimamia na kudhibiti matumizi ya DNA katika jamii. Hii ni kutokana na unyeti wa taarifa za teknolojia hii katika maisha ya binadamu na mambo yanayomzunguka. DNA inabeba taarifa binafsi za siri za chembechembe asili za urithi au viini tete za kila kiumbe, zikiwamo za binadamu. Uchunguzi na utoaji wa majibu ya utekelezwaji wa sampuli za DNA ya binadamu unazingatia maadili ya kitaalamu na miongozo ya kisheria ili kuzuia madhara yanayoweza kujitokeza kutokana na matumizi mabaya ya teknolojia hii. DNA huweza kutumika katika uchunguzi wa vielelezo vinavyohusishwa na upelelezi wa makosa ya jinai. Hii imeweza kusaidia katika kesi zenye utata, hasa za mauaji, ambapo vifaa vilivyotumika huweza kubaini watuhumiwa kama kweli walihusika au la.

## 1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Uforensiki kama taaluma ni dhana pana sana ambayo wataalamu wengi wamekuwa wakiizungumzia, hususan katika nyanja kama vile sayansi, sheria, lugha na masuala mbalimbali ya kijamii kwa lengo la kukidhi haja inayokusudiwa katika taaluma husika.

Uforensiki ni neno la Kiswahili lililotoholewa katika lugha ya Kiingereza '*forensic*' ambalo asili yake ni neno la Kilatini *forensis*. Nabar (2002: 1), akieleza asili na maana ya *forensic*, anasema kuwa, "*The term forensic derived from the Latin word 'forensis' which means belong to the courts of justice or to public discussion and debate*". Neno '*forensic*' ni neno linalotokana na lugha ya Kilatini ambalo linamaanisha mali ya mahakama au mijadala na midahalo ya umma (tafsiri yetu). Anaendelea kufafanua juu ya maana hiyo kwa kuangalia "*forensic science*", anasema:

> *Is scientific discipline which is directed to the recognition, identification, individualization, and evaluation of physical evidence by the application of the principles and methods of natural science for the purpose of administration of criminal justice.*
>
> Ni taaluma ya kisayansi ambayo inaelekezwa (imekusudiwa) katika kutambua, kuainisha, kubainisha na kutathimini ushahidi wa kimwili kwa kutumia kanuni na mbinu za kisayansi kavu kwa lengo la kuongoza (kusimamia) haki katika uhalifu (tafsiri yetu).

Harris (2007: 6), akifafanua juu ya maana ya *forensic science* (Sayansi ya uhandisi) anasema kuwa, "ni taaluma ya matumizi mbalimbali ya sayansi katika sheria ya uhalifu ambazo hutimizwa (husimamiwa) na mashirika ya polisi katika kuangalia haki dhidi ya jinai". Katika *forensic science* Wikipedia, dhana hii imefafanuliwa kama matumizi ya sayansi kisheria katika makosa ya jinai na vurugu juu ya uhalifu.

Mohammed[3] katika maelezo yake kuhusu uforensiki anasema kuwa, ni taaluma ya kisayansi inayotumika katika uchunguzi ili kugundua na kuwapata wahalifu katika jamii. Anaendelea kusema kuwa, katika taaluma hii zipo mbinu, nyenzo na zana tofauti ambazo hutumika na husaidia katika uchunguzi kwa kusudi la kuisaidia serikali na mahakama kuwadhibiti na kufanya maamuzi ya haki dhidi ya watuhumiwa hao, kwa sababu hutumika kama sehemu ya ushahidi. Miongoni mwa zana zinazotumika ni kama vile kamera, kompyuta, simu, na vifaa vingine vya kimaabara kama vile darubini. Vilevile, kuna uchunguzi wa alama kama vile michoro, alama za vidole, damu, nguo na nywele. Mambo yote haya, mara nyingi, hutumika katika uchunguzi wa awali, hasa katika eneo la tukio (*crime scene*), ili kupata ushahidi dhidi ya uhalifu huo

Ponera katika muhadhara wake kwa wanafunzi wa MAKL (2017) alisema kuwa, "Uforensiki ni taaluma ya uchunguzi wa mashauri ya jinai kwa kutumia njia na nyenzo za kisayansi na teknolojia". Sanaa ya kiforensiki ni aina yoyote ya sanaa inayohusiana na suala la usalama na sheria. Yaani ni sanaa inayosaidia kutambuliwa, kukamatwa na/au kutiwa hatiani kisheria kwa mtu yeyote ahusikaye na uhalifu. Taaluma hii huhusiana na upelelezi na hutumiwa katika nyanja nyingi kama vile utabibu, sheria, lugha na sanaa (ikiwemo fasihi), saikolojia, anthropolojia, historia na sosholojia.

Nyanja zote hizi hutumiwa na wataalamu wa uchunguzi katika kuwabaini na kuwapata wahalifu katika jamii. Kwani huweza kutumia ushahidi wa mwili (*physical evidence*) kama vile damu, DNA na alama za vidole (*fingerprints*). Kwa

[3] Mahojiano kati ya mtafiti na mkuu wa mashtaka (chief officer), Nd. Hassan Ali Mohammed, katika ofisi ya Mkurugenzi Mkuu wa Mashtaka Zanzibar (DPP *OFFICE*). Mahojiano yaliyofanyika Julai 28/2017 saa 8: 30 mchana.

mantiki hii, ni wazi kwamba, utafiti huu ameshughulika na kipengele cha uforensiki katika riwaya teule. Hii ni kutokana na umuhimu wake mkubwa kwa jamii; kwa sababu taaluma hii inaweza kusaidia kuleta maendeleo kwa kuwafichua wahalifu ambao wapo katika jamii hiyo. Hatimaye kuweza kupunguza au kuondoa kabisa matendo ya kihalifu katika jamii na taifa kwa jumla. Hii ni kwa sababu uhalifu ni msingi mkuu wa kudumaza maendeleo.

Katika fasihi ya Kiswahili tunaweza kupata mikondo kadhaa ya riwaya ukiwemo mkondo wa kihalifu na kipelelezi. Mikondo hii husanwa kwa lengo la kuakisi hali halisi ya maisha ya mwanadamu katika jamii, hususan maeneo ya mijini. Madumulla (2009: 44) anasema kuwa, "kategori hii ya ubunaji kuhusu uhalifu na kipelelezi ilijitokeza katika fasihi ya Kiswahili karibu mwishoni mwa muongo wa tano wa karne ya 20". Mkondo wa kipelelezi ni aina ya utunzi inayohusisha hadithi zinazosimulia kuhusu upelelezi juu ya uhalifu fulani kama vile: ujambazi, wizi, rushwa, na mauaji. Mara nyingi huanza na tukio fulani la uhalifu ambalo limekwishatendeka. Naye, msimulizi, huwaongoza wasomaji katika safari ya kung'amua kiini cha uhalifu husika. Hivyo basi, mkondo wa kihalifu na kipelelezi ni mkondo ambao unahusu riwaya zenye uhalifu na upelelezi ndani yake kama vile ujambazi, rushwa na mauaji. Riwaya ya *Mhanga wa Ikulu*, *Mtuhumiwa*, *Kiu ya Haki*, *Mdunguaji*, *Tutarudi na Roho Zetu*?, *Masaibu ya Ndugu Jero* na *Simu ya Kifo* ni mifano ya mkondo huu kwani zimejaa upelelezi unaotokana na uhalifu unaotendwa katika jamii mbalimbali nchini.

Upelelezi ni taaluma ya kutafuta mambo kwa siri. Shughuli ya upelelezi ilikuwepo kwa miaka mingi sana tokea binadamu alipoanza kuishi. Kimura (1992) akifafanua

juu ya upelelezi katika historia ya fasihi anasema kuwa, “Neno upelelezi linatokana na matendo ya siri yanayohusu tambiko. Matendo hayo mara kwa mara huambatana na kifo kinachosababishwa na utoaji wa siri nje”. Hata hivyo, inaelekea kuwa historia ya riwaya ya upelelezi ni fupi ikilinganishwa na mikondo mingine ya riwaya, kama anavyosema Sharma (2003: 13) kuwa, “*forensic science literature has been developing during the past few decades* (yaani, taaluma ya uchunguzi ya kifasihi ilikuwa inaendelea katika miongo michache iliyopita).

Kwa kuwa teknolojia ya kisasa ya upelelezi haikuwepo hapo awali, mbinu za upelelezi zilizotumika wakati huo zilikuwa za asili zilizohusisha imani, uchawi, uganga, mitazamo ya jadi na kiapo. Mbinu hizi zinatofautiana kulingana na vipindi vya maisha wanavyopitia wanadamu, hasa nchini Tanzania. Kwa mfano, kabla ya ukoloni, wakati wa ukoloni, baada ya uhuru na hata sasa.

Kabla ya ukoloni, mbinu kadhaa zilikuwa zinatumika katika kuwafichua na kuwakamata wahalifu. Miongoni mwa mbinu hizo ni kuwaapisha watuhumiwa. Watu waliofikiriwa au kutuhumiwa kuwa ni wahalifu waliweza kuapishwa kulingana na imani ya jamii husika. Hii ndiyo ilikuwa njia sahihi kwa wakati huo ya kuweza kumtambua na kumpata mhalifu katika jamii. Sumary (2013), akitolea mfano mbinu zilizotumika wakati huo, anasema:

> Katika jamii ya Wakaguru huko Morogoro kiapo kiliambatana na chungu. Chungu hicho kilitiwa maji na kuwekwa kwenye jiwe, mtuhumiwa alipewa kipande kidogo cha mti ambacho kila mmoja alikitemea mate na kusema “kama ndimi mhalifu niliyetenda jambo hili basi nimwagikie”. Baada ya hapo hudondosha kipande hicho kwenye maji. Kipande kikiendelea kukaa juu ya maji (kikielea) basi mtu huyo huwa hana hatia, lakini maji yakiruka ruka husemwa kuwa mtuhumiwa huyo ndie mhalifu (uk: 2-3).

Wakati wa ukoloni, mbinu za upelelezi za kuwatambuwa na kuwapata wahalifu zilibadilika kutoka zile za kijadi, kama vile matambiko, na kuanza mbinu nyingine za Kimagharibi. Kipindi hiki mifumo ya kimahakama na kipolisi ilianzishwa na kuanza kutumika. Imani za jadi, kama vile uchawi zilianza kudharauliwa kama tunavyoona katika vitabu kama vile, *Kurwa na Doto* na *Imani za Ushirikina na Uchawi*. Waandishi wa riwaya hizi walijaribu kutumia mbinu za kimagharibi kama vile, polisi na kutumia mbinu za kisayansi katika kuwatafuta wahalifu na kuachana na mbinu hizo za asili na kijadi zilizokuwepo. Hali ya amani na maelewano ambayo haikuhitaji polisi nchini Tanzania na hata baadhi ya nchi za Afrika ilianza kupotea. Badala yake palizuka wezi, wahalifu na majambazi, hasa hali ya vipato vya watu vilipoanza kutofautiana na matabaka kujitokeza. Mazingira hayo mapya ya ubepari wa kikoloni ndiyo yaliyozaa riwaya ya upelelezi ya kisasa katika fasihi ya Kiswahili. Madumulla (1991: 57) anashadidia hili kwa kusema: “Katika Tanzania aina hii ya riwaya ililetwa kwa mara ya kwanza katika fasihi ya Kiswahili na Muhammed Said Abdulla alipoandika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* (1957)”

Baada ya uhuru, pia, zipo riwaya za upelelezi zilizojitokeza zenye kueleza mambo ya kihalifu zaidi, hasa matukio na visa vya unyanyasaji, ujambazi na mauaji. Riwaya hizi huwa na mpelelezi mkwezwa anayetetea na kuiwakilisha dola. Huyu hujulikana kama polisi. Matendo na matukio yanayosawiriwa katika riwaya hizi yanashabihiana sana na hali halisi ya maisha katika jamii nyingi, hususan maeneo ya mijini. Mathalan, kuna matendo na matukio ya kihalifu katika riwaya ya *Simu ya Kifo* (1965) na *Mpelelezi Hodari na Genge la Wahalifu* (1975), ambayo yanawaathiri wanajamii katika kuleta maendeleo ndani ya jamii zao.

Mkondo huu wa upelelezi wa kipolisi umeigwa na kuendelezwa na waandishi wengine ambao hulenga kuelimisha na kuikomboa jamii juu ya matukio na matendo yanayojitokeza katika jamii zetu, yakiwemo matendo ya kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni. Miongoni mwa waandishi hao ni kama vile Beka Mfaume katika riwaya yake ya *Mhanga wa Ikulu*, Husein Tuwa katika riwaya yake ya *Mtuhumiwa*, *Mdunguaji na Utata wa* 9/12, Zainab Mwanga katika riwaya yake ya *Kiu ya Haki*, Eddie Ganzel katika riwaya yake *Ndoto ya Mwendawazimu*, *Jogoo la Shamba*, na *Kijasho Chembamba*, na Simbamwene katika riwaya yake ya *Mwisho wa Mapenzi* na wengine wengi.

Riwaya pendwa za Kiswahili zinaendelea kukua siku hadi siku na kuibuka na hali ya kufichua mambo mengi muhimu yaliyomo katika jamii. Waandishi hufanya hivyo kwa lengo la kuiamsha na kuisemea jamii hiyo. Uforensiki katika riwaya pendwa ni kipengele muhimu ambacho kinahitaji uhakiki na uchambuzi wa kina ili kuinufaisha jamii juu ya taaluma hiyo. Tunaweza kusema kwamba, hadi sasa kipengele hiki cha uforensiki hakijafanyiwa uchunguzi wa kutosha katika riwaya pendwa. Hii ni kwa sababu wahakiki wengi waliochunguza na kuzungumzia riwaya hizi wameangalia baadhi ya vipengele tu, kama vile, mapenzi, historia na nafasi ya mwanamke. Hivyo basi, utafiti huu umefafanua na kuweka wazi umuhimu wa taaluma ya uforensiki katika kuielewa riwaya pendwa. Umefanya hivyo kupitia kuchambua matukio yanayosababisha kufanyika kwa uforensiki, kubainisha miktadha ambayo taaluma ya uforensiki inafanyika na kuchunguza uhusiano uliopo kati ya uforensiki katika riwaya na maisha halisi ya jamii.

### 1.3 Tamko la Tatizo la Utafiti

Dhana ya uforensiki na dhima zake katika jamii nyingi za Kiafrika haionekani kutiliwa maanani kwa upana wake ikilinganishwa na vipengele vingine vinavyojenga umbile halisi la kazi za kifasihi katika fani na maudhui. Mtafiti ameamua kufanya utafiti katika kipendele hiki kutokana na msukumo ambao unadhihirisha upungufu mkubwa juu ya uelewa wa dhana ya uforensiki na faida inayopatikana kwayo.

Ni tafiti chache sana ambazo zimeonekana kujikita moja kwa moja katika kuzungumzia dhana ya uforensiki katika muktadha wa fasihi andishi hasa katika riwaya. Mfano wa tafiti hizo ni utafiti uliozungumzia mfumu wa uchunguzi wa kisayansi kwa mazingira ya wingu katika riwaya uliofanywa na Digambar (2015). Hivyo, tunaona kwamba tafiti nyingi zinajikita zaidi katika kueleza ama kuchunguza maswala kama vile, mapenzi na nafasi ya mwanamke. Kwa mfano, Augustine (1990), Sumary (2013), Mazongele (2015) na wengine wamefanya utafiti katika riwaya pendwa lakini hawakugusia kabisa kipengele hiki cha uforensiki. Jambo hili la kutokushuhulikia kipengelele hiki linachangia kudumaa kwa taaluma husika ya fasihi, hasa katika utanzu wa riwaya. Pia, riwaya zenye kutumia mtindo huu huonekana kuwa hazina maana katika jamii. Hii ni kwa sababu wanajamii husika hawajapatiwa ufafanuzi wa kutosha juu ya dhana ya uforensiki, utekelezwaji wake, manufaa yake pamoja na dhima zake katika jamii. Hivyo basi, dhana ya uforensiki inaonekana kwamba itakuwa na hamasa na mvuto kwa wasomaji wa fasihi endapo watapatiwa ufafanuzi wa kutosha juu uforensiki na utekelezwaji wake katika jamii. Hili linatokana na uchunguzi uliofanywa na mtafiti kupitia tafiti zinazozungumzia uforensiki katika nyanja tofauti kama vile, lugha (*forensic linguistic*) na utabibu

(*clinical forensic*) kama ilivyofafanuliwa na Jordan (2002), Kerry (2007) na Gillespie (2014).

### 1.4 Malengo ya Utafiti

Malengo ya utafiti huu yamegawanywa katika vipengele viwili, yaani lengo kuu na malengo mahususi.

#### 1.4.1 Lengo la Jumla

Utafiti huu ulikusudia kuchunguza uforensiki katika riwaya pendwa ya Kiswahili katika riwaya teule ambazo ni *Mzimu wa Watu wa Kale*, *Mhanga wa Ikulu* na *Kiu ya Haki*.

#### 1.4.2 Malengo Mahsusi

a) Kufafanua matukio yanayosababisha kufanyika kwa uforensiki katika riwaya teule;

b) Kubainisha miktadha inayohusiana na taaluma ya uforensiki katika riwaya teule; na

c) Kulinganisha uforensiki uliomo katika riwaya teule na maisha halisi ya jamii.

### 1.5 Maswali ya Utafiti

a) Je ni matukio gani yaliyomo katika riwaya teule yanayosababisha kufanyika kwa uforensiki?

b) Ni katika miktadha ipi ambamo taaluma ya uforensiki imefanyika katika riwaya teule?

c) Ni uhusiano gani uliopo kati ya uforensiki katika riwaya teule na maisha halisi katika jamii?

## 1.6 Manufaa ya Utafiti

Kukamilika kwa utafiti huu kunatarajiwa kuwa nyenzo muhimu katika kukuza uga wa fasihi ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu matokeo yake yanategemewa kuwa na manufaa yafuatayo. Kwanza, unategemewa kuamsha ari na hamasa za wasomaji wa kazi za fasihi kwa kule kutambua kwa kina kipengele cha uforensiki na umuhimu wake katika jamii. Pili, utafiti huu unatoa dira na uelewa kwa wanajamii na vyombo au taasisi zinazohusika na kufanya uforensiki juu ya ubora au udhaifu katika kufanya kazi yao hiyo. Tatu, matokeo ya utafiti huu yatasaidia kufanya tathmini faafu juu ya kufaa au kutokufaa kwa matumizi ya kipengele cha uforensiki katika riwaya pendwa. Hivyo, matokeo haya yatasaidia kuleta maendeleo kwa kupunguza vitendo vya uhalifu katika jamii. Nne, waandishi na wahakiki wa kazi za kifasihi watapata taaluma zaidi ya jinsi ya uforensiki unavyofanyika kwa kupitia marejeleo ya kazi ambazo zinazungumzia suala hili, ndani na nje ya bara la Afrika. Tano, ni mategemeo ya mtafiti kuwa, wale wote ambao watajitokeza hapo baadaye kuendelea kufanya utafiti katika kipengele hiki, watafaidika kwa kiasi kikubwa katika kupata rejea hii muhimu na hatimaye kuwapa fursa wao zaidi ya kuboresha tafiti zao.

## 1.7 Muhtasari wa Sura ya Kwanza

Sura ya hii ilianza kwa kutoa fasili na ufafanuzi wa dhana mbalimbali zilizotumika katika utafiti huu. Miongoni mwa dhana hizo ni forensiki, riwaya, riwaya pendwa, upelelezi, ushahidi na DNA. Dhana hizi zilifafanuliwa kwa ufupi ili kutoa mwongozo mzuri wa utafiti. Aidha, yameelezwa masuala yahusuyo usuli wa tatizo la utafiti, tamko la tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, likiwemo lengo kuu na malengo mahsusi, maswali ya utafiti na mwisho yakaelezwa manufaa ya utafiti.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA MAANDIKO NA NADHARIA YA UTAFITI

## 2.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea maandiko mbalimbali yanayohusiana na utafiti huu. Maandiko hayo yamegawanywa katika makundi mawili, ambayo ni maandiko yanayohusu riwaya za kipelelezi ambazo zipo ndani ya riwaya pendwa, na maandiko yanayohusu uforensiki. Pia, katika kipengele hiki tumeweza kuelezea pengo la utafiti pamoja na nadharia ya utafiti.

## 2.2 Maandiko kuhusu Riwaya za Kipelelezi

Mulokozi (1996: 154) aliandika juu ya riwaya ya upelelezi na kusema kuwa "Riwaya ya upelelezi ya Kiswahili ni hadithi ya kubuni yenye mpangilio na mtiririko wa kimantiki, visa na matukio yaliyotawaliwa na kisa cha upelelezi unaofanywa na polisi au mtu binafsi kwa kujitolea". Anaendelea kusema kuwa, riwaya ya upelelezi ya Kiswahili huwa na mambo mawili ya msingi; kosa la uhalifu na mpelelezi wa uhalifu huo hadi mhalifu anapopatikana. Maelezo haya yametaja mambo ya msingi yanayotakiwa kuwemo katika riwaya ya upelelezi. Hata hivyo, hayajafafanua ni makosa ama matukio yapi ya kihalifu yanayohitaji kuhusisha uforensiki, yumkini ni kutokana na kuwa hilo halikuwa lengo la mwandishi huyu. Pengo hili limefanyiwa kazi kwenye utafiti na tasnifu yetu.

Ntarangwi (2004) anaeleza kuwa, riwaya za upelelezi ziliandikwa kwa lengo la kujitatulia matatizo ya kiuchumi ambapo zaidi hujishughulisha na mada za mapenzi au uhalifu. Kazi hizi zinafaulu na kujitosheleza kwa wingi kutokana na soko lake kubwa ambalo hasa ni uchapishaji. Maelezo haya yanatoa mwanya kitaaluma kwa

kueleza kuwa, lengo la riwaya hizi ni kujikwamua kiuchumi jambo ambalo si sahihi. Kupitia utafiti huu, mtafiti ameweka bayana jambo hili kwenye tasnifu hii kwa kuchambua taaluma ya uforensiki katika riwaya teule.

Kezilahabi (1976: 36 - 37) anaeleza kuwa, riwaya za upelelezi katika fasihi ya Kiswahili ni nyingi. Anazitaja baadhi ya riwaya hizo kuwa ni: *Mzimu wa Watu wa Kale, Kisima cha Giningi*, *Duniani Kuna Watu*, *Siri ya Sifuri*, *Simu ya Kifo, Ndoto ya Mwenda Wazimu*, *Mbojo Simba Mtu*, *Tatizo la Kisauni* na *Kizimbani*. Anasema kuwa, riwaya za upelelezi zina ufundi wake na zinaweza kuwa ngumu kwa mwandishi ambaye hakuzizoea. Alieleza mambo matatu ambayo husaidia katika uandishi wa riwaya hizi; mambo hayo ni pamoja na: Kwanza, mwandishi awe na uwezo wa kutumia hali ya hewa na mazingira katika kujenga hali. Pili, awe na uwezo wa kueleza mazingira au kitu kilivyo, yaani kishabihiane na matendo afanyayo au tabia yake. Na, tatu, awe na uwezo wa kuficha sababu za tukio linalofanyiwa uchunguzi. Anasisitiza kuwa riwaya hizi za upelelezi husomwa na watu wengi katika jamii zetu. Hivyo, dhima ya fasihi ifikiayo watu wengi zaidi katika jamii ni kubwa kuliko vitabu vingine vya fasihi vinavyosomwa na watu wachache.

Mabala (1987), akinukuliwa na Kimura (1992), anaeleza kuwa riwaya za uhalifu na upelelezi za Tanzania hutibua jamii wakati zinapofichua na kushambulia madhambi mbalimbali ya dola na ya wakubwa. Hiii ni kwa sababu zinapoonesha dosari ya mfumo uliopo. Riwaya hizo huleta suluhu katika jamii wakati zinapotoa utatuzi wa kibinafsi wa mgogoro uliopo; na hivyo, kuonesha kuwa mfumo uliopo unafaa kwa vile unaweza kujisahihisha wenyewe. Maelezo haya yalitoa mwongozo kwa mtafiti

na kuweza kuona mwanya uliopo. Hii ni kwa sababu mwandishi ameangalia migogoro ya kijamii dhidi ya utawala na kutokugusia kabisa kipengele cha uforensiki.

Mlacha (2004: 9), akimnukuu Agho (1991), anasema kuwa “Mwandishi wa riwaya ni kama mwandishi wa matukio ya jamii; na kwa hiyo, huwa mtetezi na mlezi wa jamii”. Katika makala hii aliangalia kwa ufupi jinsi riwaya za Kiswahili zilivyoakisi mabadiliko ya utamaduni ya jamii karne hii ya ishirini; na hivyo, kutoa picha ya uhusiano wa riwaya na utamaduni wa Mtazania katika karne ijayo, hususan kuhusiana na mwelekeo wa mabadiliko ya kisayansi na teknolojia na mafanikio yake. Kutokana na maelezo haya, ni wazi kuwa, mwandishi amezungumzia juu ya maudhui ya riwaya kwa ujumla na kuacha kipengele hiki cha uforensiki ambacho ni moja kati ya vipengele vya fani. Hivyo, kipengele hiki cha kifani na umuhimu wake katika jamii kimefafanuliwa kwenye tasnifu hii.

Sanga (2012) anabaina kuwa, waandishi na wahakiki wa kazi za kifasihi wamezichambua kazi za riwaya pendwa kwa kueleza historia na sifa zake, kuainisha, na kueleza athari zake kwa wasomaji. Hivyo, alijaribu kuongeza uga wa uchambuzi wa kazi za riwaya pendwa kwa kutumia taaluma ya ujumi. Anataja vigezo vilivyotumika katika kubainisha vipengele vya kiujumi katika riwaya pendwa ya Kiswahili. Tunakubaliana na utafiti huo kutokana na hoja na maelezo yaliyomo. Hii ni kwa sababu umeweza kutoa mwanga mkubwa kwa mtafiti juu ya utafiti wake huu kwa kuonesha nyanja zilizoshughulikiwa na watangulizi waliopita na pia kuonesha mapengo yaliyoachwa na watafiti hao

## 2.3 Mapitio ya Maandiko Kuhusu Uforensiki

Silverman (2011), katika utafiti wake uliohusu upelelezi katika uhalifu, anazungumzia mbinu nzuri za uboreshaji juu ya suala la utoaji wa ushahidi katika baadhi ya maeneo nyeti katika jamii ambayo ni pamoja na maeneo yanayofanyika uhalifu, ugaidi na baadhi ya matukio mengine ya Kiraia. Vile vile, utafiti huu unazungumzia jinsi taaluma ya uforensiki inavyoweza kuchangia kwa urahisi kupatikana kwa maendeleo nchini kwa kuwafichua wahalifu na uhalifu katika jamii husika.

NIJ (2015) wanaelezea jinsi ya kuongeza teknolojia ambayo itaongeza ufanisi katika kusaidia kufichua uhalifu na kufikisha katika vyombo vya kisheria nchini Marekani. Pia, wanaeleza jinsi ya kutumia sampuli moja kuamua na kutoa habari nyingi zinazohusishwa na utambulisho katika mwili wa mwanadamu, kama vile aina ya maji katika mwili wa mwanadamu. Maji haya hutumika katika kufanya uchunguzi kisayansi kwa kutumia vipimo maalumu ili kumtambua mhusika wa uhalifu uliotendeka. Maelezo hayo ya NIJ yametoa dira na mchango mkubwa katika utafiti huu kwa kule kuonesha baadhi ya viashiria ambavyo vinapatikana katika mwili wa mwanadamu na ambavyo husaidia kutumika katika kufanya uchunguzi kwa lengo la kumtambua mhalifu.

Jordan (2002) amefanya utafiti katika lugha na aliangalia matumizi ya lugha kwa ajili ya ushahidi katika kesi za jinai. Anasema "*In the United States, forensic linguists are hired by either the defense or the prosecution to analyze linguistic evidence in case*" yaani, katika nchi ya Marekani wataalamu wa taaluma ya uchunguzi wa lugha huajiriwa na ulinzi au kwenye mashtaka kuchambua ushahidi

wa lugha katika kesi (tafsiri yetu). Katika utafiti wake huo anasema kuwa, ikiwa wakili wa utetezi anaona kwamba uchambuzi haukubaliki katika mahakama dhidi ya kesi yake, utetezi utamwachia mtaalamu huyo na kutafuta mwengine ambaye uchambuzi wake ni bora zaidi. Maelezo hayo ya Jordan yametoa dira na mchango mkubwa katika utafiti huu kwa kuangalia kipengele hiki cha lugha. Hata hivyo, utafiti huu umechambua matukio tofauti yanayofanyiwa uforensiki kupitia nyenzo na vipengele tofauti.

Duvall (2013) katika utafiti wake alichunguza mambo kadhaa ambayo hutumika ili kuleta maendeleo ya mbinu za uchunguzi kwa ya makosa ya jinai yanayofanyika katika jamii. Miongoni mwa mambo hayo ni majimaji yanayotoka katika viungo vya uzazi kwa mwanamume (*semen*), damu (*blood*), na nywele (*hair and fibre*). Maelezo hayo ya Duwell yamemsaidia mtafiti kujua kuwa, ushahidi katika kufanya uforensiki huweza kupatikana kutokana na vitu au mambo mbalimbali yaliyomo au anayokuwa nayo mwanadamu husika. Mambo hayo husaidia katika uchunguzi wa tukio la jinai ama uhalifu uliofanywa kwa mhusika huyo.

## 2.4 Pengo la Utafiti

Kama ilivyokwishaonekana kuwa, wataalamu mbalimbali wamezichambua riwaya pendwa katika vipengele kama vile, historia, aina, athari zake, maudhui, migogoro na umuhimu wake katika jamii. Hata hivyo, pamoja na uchambuzi huo inaonekana bado wataalamu hawa hawajazungumzia kipengele hiki cha uforensiki katika riwaya pendwa za Kiswahili. Hili ni pengo linalohitaji kuzibwa katika uga huu wa riwaya pendwa za Kiswahili. Kwa msingi huo, ndio maana mtafiti ameteua katika utafiti huu kushughulikia uforensiki katika riwaya pendwa za Kiswahili kwa kuonesha

matukio, miktadha na uhusiano uliopo katika riwaya hizo na maisha halisi katika jamii.

### 2.5 Nadharia ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Uhalisia. Hivyo, ukusanyaji wa data, uchambuzi na uwasilishaji wake umefanywa kwa kuzingatia dhana msingi ya uhalisia.

#### 2.5.1 Nadharia ya Uhalisia

Ntarangwi (2004: 48) anasema kwamba, "Uhalisia ni uwakilishi wa mambo katika fasihi. Mhalisia huamini katika matokeo ya mambo na ukweli unaozingatiwa ni ule unaoweza kuonekana na kuthibitishwa kwa tajiriba". Kazi yoyote ya fasihi yapaswa kuwaweka wanajamii katika ulimwengu wao wa kawaida wa kweli na halisi. Qusby (1988) aneleza kuwa, neno 'uhalisia' kwa mara ya kwanza lilitumika huko Ufaransa mnamo mwaka 1850 kwa lengo la kuelezea kazi za sanaa zilizojikita katika kuusawiri ulimwengu kama ulivyo, wala sio kama unavyofikiriwa kuwa.

Uhalisia ni nadharia yenye kuelezea aina ya mtazamo au tapo la kifasihi ambalo kazi za fasihi zinachukuliwa kuwa na sifa za msingi zinazohusishwa na uhalisi. Kimsingi, kazi za kifasihi zinatarajiwa kuwa kama uakisi wa hali halisi ya maisha katika jamii inayohusika. Katika mawanda ya fasihi, uhalisia hutokana na matatizo yanayowakabili watu. Matatizo haya ndiyo yale yaliyowafanya wasanii kuutuhumu ulimbwende ambao matamanio yake yalikuwa ni ya kinjozi zaidi yakilinganishwa na taabu zilizokuwa zikiwakabili watu (Wamitila, 2002; Wafula na Njogu, 2007).

Kufikia mwaka 1798, wahakiki kama vile Schiller, walikuwa wakitumia dhana mbili, yaani udhanaifu na uyakinifu kuashiria vinyume. Kutokana na historia hii, dhana ya uhalisi imekuja kuhusishwa na miktadha miwili. Muktadha wa kwanza ni ule unaozitazama kama njia za kutathmini hali, ukihusisha uhalisia wa maisha ya watu. Na, muktadha wa pili unaitazama dhana hii kama kazi ya sanaa inayoonesha maisha ya binadamu jinsi yalivyo kwa kuhusisha na uigaji wa mazingira anamopatikana mwanadamu kwa kutumia mbinu za kisanaa.

Nadharia hii iliwekewa misingi yake na mwanafalsafa aliyejulikana kama G.F Hegel[4] katika kitabu chake kinachojulikana kama "*Aesthetics"* ujumi (1885). Mtaalamu huyu alipendekeza matumizi ya neno uhalisia kuelezea kazi ya kifasihi ambayo inawasilisha ulimwengu wa maisha ya kijamii (Wamitila 2002). Naye, Wafula na Njogu (2007: 62-63), wakizungumzia suala la uhalisia, wanasema:

> Istilahi ya uhalisia imediriki kuhusishwa na mikondo mitatu ambayo ni: Uhalisia kama mwelekeo. Katika mkodo huu, uhalisia ni mwelekeo unaozingatia njia za kisayansi kutekeleza jambo fulani. Pia, unazingatia upinzani dhidi ya mtazamo wa kinjozi juu ya maisha na kupingana na ulimwengu. Pili, uhalisia kama mbinu ya kisanaa. Katika mkondo huu, uhalisia unahusishwa na mbinu iliyo na mashiko katika hali halisi ya maisha ya watu na uwezo wa kuonesha hali ya kisaikolojia ya watu. Tatu, uhalisia kama mbinu ya kihakiki. Katika kuihusisha na uhalisi, wataalamu hawa wanasema, uhalisia huzingatia muundo na muwala katika kazi ya fasihi, uchambuzi wa kazi ya sanaa kama zao linalojitosheleza, hali halisi ya wahusika na lugha wanayotumia na kuainisha vielelezo vya kihistoria vinavyosababisha mabadiliko makubwa ya kijamii.

Kwa jumla, tunaweza kuiangalia misingi mikuu ya nadharia hii ya uhalisia kama ambavyo wataalamu wameelezea juu ya jambo hili kama ifuatavyo: (a) Kuzingatia

[4]Georg Wilhelm Friederic Hegel alizaliwa tarehe 27/8/1770 na kufariki mwaka 1831. Hegel ni mwanafalsafa wa Kijerumani aliyechangia sana katika nadharia zinazohusu ujumi na unavyohusiana na uhalisi wa maisha ya jamii.

kwa hali ya juu uhalisi katika kuwakilisha maisha kupitia sanaa ya fasihi; (b) Sifa ya mtunzi wa fasihi au sanaa; na (c) Kiwango cha mtunzi kuwasilisha maisha jinsi yalivyo kwa uhuru na demokrasia.

Kutokana na maelezo hayo, ni dhahiri kuwa kazi za kifasihi hukusudia kusawiri jamii katika matukio halisi ya kila siku kwa njia ya kisanaa. Uforensiki ni moja kati ya vipengele muhimu vya kifani katika riwaya pendwa ya Kiswahili ambayo dhima yake kuu ni kubeba ujumbe unaoisawiri jamii hiyo katika matendo halisi yaliyopo au yanayotokea kila siku ndani ya jamii hizo. Hivyo basi, utafiti huu umesawiri na kuangaza kipengele cha uforensiki katika riwaya pendwa ya Kiswahili kwa kuongozwa na misingi ya nadharia hii. Misingi hiyo ilitumika katika kuchanganua matukio katika riwaya teule ambayo yanasababisha kufanyika kwa uforensiki, na ambayo pia hutokea katika maisha halisi ya jamii. Aidha, ilitumika katika kubainisha miktadha mbalimbali iliyohusiana na uforensiki; na pia, ilitumika katika kutathimini na kuangalia uhusiano uliopo katika wa kiforensiki katika riwaya na maisha halisi ya jamii.

## 2.6 Muhtasari wa Sura ya Pili

Sura hii imezungumzia mapitio ya maandiko na kiunzi cha nadharia, ambapo imeanza kwa kuangalia maandiko ya kifasihi yanayohusu riwaya pendwa na maandiko kuhusu uforensiki. Pia, imezungumzia mapengo ya utafiti yaliyojitokeza kutokana na mapitio ya maandiko hayo. Vilevile, imefafanua nadharia ya utafiti iliyotumika katika kukusanya na kuchambua data za utafiti uliozaa tasnifu hii.

# SURA YA TATU

# METHODOLOJIA YA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii inafafanua juu ya usanifu wa utafiti, walengwa wa utafiti, jamii ya watafitiwa, eneo la utafiti, sampuli ya watafitiwa na itikeli za utafiti. Aidha, imeelezea njia na zana za ukusanyaji data, mchakato wa ukusanyaji data, uchambuzi wa data uhalali na uthabiti wa matokeo ya utafiti, uchanganuzi na uwasilishaji data pamoja na mipaka ya utafiti huu.

## 3.2 Usanifu wa Utafiti

Katika utafiti huu aina ya usanifu ulikuwa wa muda maalumu (*cross-section studies*). Hii ni kwa sababu utafiti huu hautumii mawanda mapana sana, na hivyo kutoa majibu kwa haraka. Utafiti huu umefanyika maktabani na uwandani. Maktabani kwa ajili ya kurusu maandiko mbalimbali yaliyohusiana na mada husika zikiwemo riwaya teule zilizotumika katika utafiti huu. Na uwandani kwa ajili ya kufanya mahojiano na udodosaji kwa watafitiwa. Kwa vile utafiti huu ni wa kitaamuli, ufafanuzi na uchanganuzi wa kina wa matukio ya kiforensiki ndio ulioongoza katika utoaji wa matokeo ya utafiti huu. Data zilizokusanywa zimechambuliwa na kufafanuliwa kwa njia ya maelezo.

## 3.3 Walengwa wa Utafiati

Walengwa wa utafiti huu wamewekwa katika makundi mawili ambayo ni jamii ya watafitiwa na sampuli ya watafitiwa.

### 3.3.1 Jamii ya Watafitiwa

Ponera (2010: 63) anasema kuwa "Jamii ya tafitiwa ni jumla ya vitu vyote ambavyo mtafiti anaweza kuvitumia kwa ajili ya kupata data za utafiti wake. Huweza kuwa kundi la watu, eneo fulani la kijiografia, aina ya miti au aina fulani ya maandiko". Hivyo, jamii ya watafitiwa iliyotumika katika utafiti huu imegawanyika katika makundi yafuatayo:

a) Riwaya za Kiswahili.

b) Wataalamu mbalimbali wanaoshunghulika na masuala ya uchunguzi, upelelezi, uhalifu na jinai katika jamii kupitia taasisi mbalimbali za kijamii kama vile; ulinzi na usalama, hospitali na mahakama. Hawa wamesaidia kutoa mchango juu ya miktadha mbalimbali, vifaa na zana zinazosaidia katika kufanya uforensiki.

(c) Wanafunzi wa vyuo vikuu wanaosoma fasihi ya Kiswahili.

(d) Baadhi ya wanajamii ambao wamewahi kufikwa na kadhia ya uhalifu.

### 3.3.2 Sampuli ya Watafitiwa na Upatikanaji Wake

Sampuli humaanisha sehemu ndogo ya jamiii ya watafitiwa, ambayo mtafiti huichagua ili kuwakilisha jamii nzima. Homby (2006) anadai kuwa, sampuli ni jumla ya washiriki walengwa kutoka katika kundi kubwa ambalo mtafiti amekusudia kulifanyia utafiti ili kupata taarifa zihusuzo mada yake, na hatimaye, kupata hitimisho. Uteuzi wa sampuli, kama unavyoelezwa na Bryman (2004), ni mchakato wa kuchagua kikundi cha vitu au watu ili kutumika katika utafiti kama kiwakilishi cha kundi lolote linalotafitiwa, kwani sio rahisi kutafiti kundi zima. Mtafiti ametumia namna mbili za usampulishaji. Kwanza, ni usampulishaji lengwa. Hii ni mbinu ya usampulishaji ambayo humruhusu mtafiti kuchagua wawakilishi wa

kutafitiwa kulingana na jinsi wanavyokidhi haja na malengo ya utafiti wake. Mugenda (2003:50) anasema kuwa "katika kuitumia njia ya sampuli lengwa, mtafiti huchukua data ambazo zinahusu taarifa na malengo ya utafiti wake". Mtafiti huwa huru kuchagua watafitiwa kadiri aonavyo kuwa wanaweza kutoa taarifa za kutosheleza. Usampulishaji huu ulitumika zaidi kwa riwaya teule za Kiswahili, wataalamu wa uchunguzi, upelelezi, uhalifu na jinai katika taasisi mbalimbali za kijamii pamoja na wanajamii waliopatwa na kadhia hii ya uhalifu. Pili, ni usampulishaji nasibu holela. Hii ni aina ya usampulishaji ambayo humuwezesha kila mtu katika jamii ya watafitiwa kuwa na nafasi ya kuweza kushiriki, na hivyo, kuwakilisha wengine. Aina hii husaidia kupunguza upendeleo kwa mtafiti na watafitiwa wake. Usampulishaji huu ulitumika zaidi kwa wanafunzi wa vyuo vikuu. Hivyo basi, kwa ajili ya kufikia ufanisi na kupata taarifa zinazofaa, sampuli ya utafiti huu ilikuwa kama ifuatavyo:

a) Riwaya tatu teule ambazo ni *Mzimu wa Watu wa Kale* (1960) ya Muhamed Said Abdulla. *Mhanga wa Ikulu* (2015) ya Beka Mfaume na *Kiu ya Haki* (2004) ya Zainab M. Mwanga;

b) Wataalamu mbalimbali wanaoshughulika na masuala ya uchunguzi, upelelezi, uhalifu na jinai katika jamii kupitia taasisi mbalimbali za kijamii kama vile, ulinzi na usalama, hospitali na mahakama wapatao ishirini na moja (21). Wataalamu hao ni pamoja na wanasheria wanane (8), watano kutoka Unguja na watatu kutoka Pemba. Polisi wa upelelezi wa makosa ya jinai na uhalifu sita (6), watatu kutoka Unguja na watatu kutoka Pemba, pamoja na wauguzi wa hospitali wapatao saba (7), wanne kutoka Unguja na watatu kutoka Pemba;

(c) Wanafunzi kumi na watano (15) wa vyuo vikuu wanaosoma fasihi ya Kiswahili.

Saba kutoka Chuo Kikuu cha Waislamu Morogoro, na nane kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma.

(d) Wanajamii sita (6) ambao wamewahi kufikwa na kadhia ya uhalifu, wawili kutoka Mkoa wa Mjini Magharibi na wanne kutoka Mkoa wa Kaskazini Pemba. Jumla ya makosa makubwa ya jinai mia moja na sabiini na moja (171) yaliripotiwa katika jeshi la polisi kuwapata wanajamii katika Mkoa wa Mjini Magharibi mwaka 2014. Na makosa makubwa ya jinai arubaini na tisa (49) yaliripotiwa katika Mkoa wa Kaskazini Pemba kuwapata wanajamii mwaka 2014[5].

**3.4 Eneo la Utafiti**

Utafiti huu ulifanyika katika maeneo ya Tanzania Bara na visiwani Zanzibar, ili kupata data za uwandani na maktabani. Kwa upande wa Tanzania Bara, eneo husika lilikuwa ni mji wa Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Dodoma. Kwa upande wa Zanzibar, ulifanyika katika Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja; na kwa Pemba utafiti huu ulifanyika katika Mikoa yote miwili, yaani Mkoa wa Kusini na Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Sababu za uchaguzi wa maeneo haya ni hizi zifuatazo: Dodoma, tulitembelea maktaba ya Chuo Kikuu cha Dodoma ili kupata tasnifu na maandiko yanayohusiana na kazi za watafitiwa teule. Pia, kuzungumza na wataalamu waliowahi kufanya tafiti katika riwaya, hasa zenye kutumia mtindo wa upelelezi. Kwa upande wa Dar es Salaam, tulitembelea maktaba ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa ajili ya kupata marejeleo yaliyohusiana na mada husika, pamoja na kufanya mahojiano na mmoja wa watunzi wa riwaya teule ambaye ni Beka Mfaume.

[5] Kwa ufafanuzi zaidi wa takwimu hii, tazama katika Takwimu ya Hali ya Uhalifu Nchini Tanzania Januari- Desemba 2014 ya Januari 2015 (uk 11).

Kwa upande wa Zanzibar, katika kisiwa cha Unguja tulifanya mahojiano na wanasheria mbalimbali wanaoshughulika na mashtaka (makosa) ya uhalifu na jinai kupitia taasisi maalumu kama vile, Ofisi ya Mkurugenzi Mkuu wa Mashtaka Zanzibar, pamoja na kutembelea Hospitali ya Mnazi Mmoja ambapo tulifanya mahojiano na madaktari husika pamoja na wale wote wanaoshughulika na mambo ya uchunguzi yanayohusu uhalifu. Pia, tulifanya mahojiano na maafisa wa usalama dhidi ya matukio ya kihalifu yanayojitokeza katika jamii na changamoto zake. Kwa Pemba, tulitembelea maktaba ya mkoa kwa ajili ya kujisomea zaidi. Pia, tulifanya mahojiano na wataalamu wa uchunguzi wa makosa ya uhalifu na jinai, wakiwemo polisi. Pia, kutembelea hospitali kuu za Mkoa kwa ajili ya uchunguzi na mahojiano zaidi na wauguzi wakuu wa hospitali hizo.

### 3.5 Itikeli za Utafiti

Ili kupata data kutoka kwa watafitiwa, mtafiti aliomba barua ya utambulisho kutoka Kurugenzi ya Masomo ya Shahada ya Juu ya Chuo Kikuu cha Dodoma. Pia, mtafiti aliomba ridhaa kwa watafitiwa kwa lengo la kupata ushirikiano nzuri. Aidha, maadili yote ya utafiti yanayomhusu mtafiti na watafitiwa kama vile, utunzaji wa siri za taarifa na majina ya watafitiwa yalizingatiwa kadiri ya matakwa yao wenyewe.

### 3.6 Ukusanyaji wa Data

Sehemu hii inaelezea mbinu na zana mbalimbali zilizotumika katika ukusanyaji wa data za utafiti, pamoja na mchakato (utaratibu) mzima wa kukusanya data za utafiti husika.

### 3.6.1 Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Mbinu za utafiti ni utaratibu maalumu unaopangwa kufuatwa na kumwongoza mtafiti katika kukusanya na kuchambua data ili kujibu maswali ya utafiti husika (Best na Kahn, 1993). Mbinu za mahojiano na udurusu wa maandiko zilitumika katika mchakato mzima wa ukusanyaji wa data za utafiti huu. Hii ni kwa sababu mbinu hizi zilimsaidia mtafiti kupata data za msingi na za uhakika kutoka kwa watafitiwa na vitafitiwa. Jambo ambalo husaidia kuzifanya data hizo kuwa thabiti na zenye kuaminika.

#### 3.6.1.1 Mahojiano

Njia hii inahusu mazungumzo kati ya mtafiti na watafitiwa. Mtafiti ametumia mbinu hii ya mahojiano kwa ajili ya kukusanya taarifa za utafiti huu wakati akiwa uwandani. Chuachua (2010: 70) akiifafanua mbinu hii, anaeleza kuwa:

> Mahojiano ni mbinu muhimu na inayotamalaki katika utafiti unaotumia mbinu inayoegemea ubora wa jambo linalotafitiwa. Inahusisha kubadilishana mawazo kati ya watu wawili au zaidi kuhusu mada fulani inayotafitiwa, mbinu hii inasisitiza umuhimu wa kuhusisha mawazo toka kwa watu tofauti wakati wa kukusanya data za utafiti.

Hivyo, katika kuitumia mbinu hii, mtafiti alitayarisha maswali ya mahojiano ya ana kwa ana baina yake na watafitiwa. Maswali yaliyotayarishwa yanatokana na malengo mahsusi ya utafiti huu. Yalihusisha wanasheria, wauguzi, polisi na maafisa wa upelelezi, wanajamii, wasomi pamoja na wataalamu mbalimbali katika uga huu wa fasihi ya Kiswahili. Matumizi ya mbinu hii yamemwezesha mtafiti kupata taarifa za moja kwa moja kutoka kwa watafitiwa. Pia, mbinu hii ilitoa fursa na muda nzuri kwa mtafiti kuuliza maswali ya nyongeza na kutoa ufafanuzi zaidi pale ilipohitajika kufanya hivyo.

#### 3.6.1.2 Udurusu wa Maandiko

Maandiko mbalimbali hutupatia taarifa kuhusu mada inayotafitiwa. Pia, hutuwezesha kutoa ithibati kuhusu data zilizokusanywa kwa mbinu ya mahojiano. Kothari (2004) anaeleza kuwa, hii ni mbinu inayohusisha uchambuzi wa maudhui yaliyomo katika nyaraka kama vile vitabu, magazeti na maudhui ya maneno ambayo yanaweza kuwa ya maandishi au mazungumzo. Sababu ya kuchagua kutumia mbinu hii ni kwamba, kwa vile kumbukumbu mbalimbali huhifadhiwa katika maandishi, inaweza kurahisisha kupata data muhimu zinazohusu utafiti huu.

### 3.6.2 Zana za Kukusanyia Data

Zana zinazotumika katika utafiti mara nyingi hutegemea mada inayotaka kutafitiwa, lengo la utafiti huo, uwezo alionao mtafiti mwenyewe kama vile fedha na upeo wa taaluma, utamaduni na mazingira yanayomzunguka mtafiti. Hivyo basi, vifaa vilivyotumika kukusanyia data katika utafiti huu ni daftari na kalamu, ambavyo vimetumika katika kunukuu na kuhifadhia data. Kamera ya picha mgando au tuli ambayo imetumika kuwekea kumbukumbu za matukio mbalimbali huko uwandani wakati wa mahojiana ya mtafiti na watafitiwa. Kinasa sauti pia kilitumika kuhifadhi taarifa za watafitiwa. Kutumika kwa vifaa hivi vimemsaidia mtafiti kuhifadhi data zilizotarajiwa kukusanywa katika mahojiano baina ya mtafiti na watafitiwa wake alipokuwa uwandani akikusanya data za utafiti huu.

### 3.6.3 Mchakato wa Ukusanyaji wa Data

Kwa mujibu wa BAKIZA (2010:63) “data ni mkusanyiko wa taarifa za kiuchunguzi wa kitaalamu unaopelekea kupatikana ushahidi wa jambo”. Katika ukusanyaji wa data, utafiti huu ulifuata taratibu na miiko ya utafiti. Utafiti ulizingatia maadili na

miiko inayoongoza mchakato mzima wa utafiti. Kabla ya mchakato wa kukusanya data kuanza, mtafiti aliomba ruhusa toka kwa mamlaka zinazohusika ili kumruhusu kufanya utafiti wake. Data za uwandani zimekusanywa kwa kutumia njia ya mahojiano kati ya mtafiti na watafitiwa walioteuliwa kulingana na malengo ya utafiti huu. Na data za maktabani, zimekusanywa kwa kutumia mwongozo wa usomaji ambao ulimuongoza mtafiti kupata data zinazohusiana na utafiti huu.

### 3.7 Uhalali na Uthabiti wa Matokeo ya Utafiti

Uhalali wa matokeo ya utafiti ni hali ya matokeo ya utafiti kuwa na maelezo yenye vigezo vya kupima jambo au mambo yanayotakiwa kupimwa katika kutafitiwa huko. Uthabiti wa utafiti ni hali ya utafiti kuweza kutoa matokeo yatakayolingana na tafiti nyingine zinazolingana nazo katika siku za mbele. Vipengele hivi viwili vinabebana na kutoshelezana. Hii ikiwa na maana kuwa, ni vigumu kuwa na utafiti wenye matokeo thabiti lakini hakuna uhalali wa matokeo hayo (Kothari, 2009). Uhalali wa matokeo ya utafiti huu umethibitishwa kwa mambo yafuatayo: Kwanza, kuweka bayana malengo na mipaka ya utafiti. Hivyo, maswali yaliyoulizwa yalihusiana na malengo ya utafiti huu. Pili, matumizi mazuri ya lugha inayofahamika kwa urahisi ambayo iliwasaidia watafitiwa kuelewa kinachotafitiwa. Tatu, njia zilizotumika kukusanyia data (mahojiano na udurusu wa maandiko) zimewezesha matokeo ya utafiti huu kuwa na kiwango kinachoridhisha cha uthabiti.

### 3.8 Uchanganuzi wa Data

Data za utafiti huu zimechanganuliwa kwa njia ya maelezo kwa kutumia misingi ya Nadharia ya Uhalisia. Nadharia hii ndiyo iliyomwongoza mtafiti katika kubainisha na kuchambua kazi za kifasihi, hususani riwaya pendwa zinavyovuta hamasa kwa

wasomaji na uelewa wao juu ya dhana ya uforensiki katika jamii. Aidha, nadharia hii ilimwongoza mtafiti katika kulinganisha uforensiki uliomo katika riwaya teule na maisha halisi ya jamii. Hii ni kwa sababu ya kutaka kupata uhalisi wa kifasihi katika maisha. Hivyo, data zilizopatikana katika udurusu wa maandiko zimechujwa na kutumika pale tu zilipokidhi na kufaa kwa mahitaji ya tasnifu hii. Pia, data zilizopatikana katika mbinu ya mahojiano zilichanganuliwa na kuwasilishwa kwa kuzingatia malengo ya utafiti. Hivyo, uwasilishaji na uchanganuzi wa data ulikuwa katika mtiririko sawa na malengo ya utafiti.

## 3.9 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu umejikita zaidi katika fasihi andishi katika uga wa riwaya. Kupitia riwaya pendwa za Kiswahili, mtafiti alichunguza uforensiki ndani ya riwaya teule kutoka kwa waandishi mbalimbali. Waandishi hao ni pamoja na Muhammed Said Abdulla na riwaya yake ya *Mzimu wa Watu wa Kale* (1960), Beka Mfaume kupitia riwaya yake ya *Mhanga wa Ikulu* (2015) na Zainab M. Mwanga kupitia riwaya yake ya *Kiu ya Haki* (2004).

## 3.10 Changamoto za Utafiti na Utatuzi Wake

Mtafiti alikumbana na changamoto mbalimbali ambazo zilisababisha ugumu katika uandaaji wa tasnifu hii. Miongoni mwa changamoto hizo ni kama vile, uhaba wa fedha kwa mtafiti, mwamko mdogo kwa baadhi ya watafitiwa juu ya taaluma hii ya uforensiki na hata kudhani kwamba ni usaliti kutoa taarifa zinazohusiana na upelelezi, hasa taasisi za uchunguzi na upelelezi kama vile polisi.

Katika kupambana na changamoto hizo, mtafiti alifanya yafuatayo. Kwa upande wa fedha, mtafiti alijaribu kuwasiliana na ndugu, jamaa na marafiki, pamoja na

kuwaandikia wahisani mbalimbali ili waweze kusaidia juu jambo hili. Vilevile, kuhusu mwamko na uelewa mdogo kwa watafitiwa juu ya uforensiki, kwa upande wa wanafunzi mtafiti alitoa ufafanuzi uliowasaidia kuielewa taaluma hii na hivyo kuweza kuchangia maarifa waliyokuwa nayo juu taaluma ya uforensiki katika jamii zao. Aidha, kwa upande wa taasisi ya uchunguzi na upelelezi mtafiti aliweza kuwaeleza dhima na lengo la utafiti husika ambapo walimwelewa na kutoa ushirikiano mzuri kwa mtafiti.

### 3.11 Mpango wa Tansifu

Tasnifu hii ina jumla ya sura tano. Sura ya kwanza inahusu utangulizi, ufafanuzi wa dhana, usuli wa tatizo la utafiti, tamko la tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti. Sura ya pili imehusisha mapitio ya maandiko, ambayo ni maandiko yaliyohusu riwaya pendwa na maandiko yaliyohusu uforensiki. Pia, sura hii imehusisha mapengo ya utafiti pamoja na kiunzi cha nadharia ya utafiti. Sura ya tatu imefafanua usanifu wa mbinu na vifaa vya utafiti, eneo la utafiti, maadili na miiko ya utafiti, uhalali, umakini na usahihi wa upatikanaji wa data. Sura ya nne ni yenye mchakato mzima wa uwasilishaji na mjadala wa matokeo ya utafiti. Sura ya tano imeeleza muhtasari, mapendekezo na hitimisho la tasnifu hii.

### 3.12 Muhtasari wa Sura ya Tatu

Sura hii imeelezea methodolojia ya utafiti ambayo ilimwongoza mtafiti katika zoezi zima la ukusanyaji data za utafiti huu. Mambo yaliyoelezwa ni pamoja na usanifu wa utafiti, walengwa wa utafiti, jamii ya watafitiwa, sampuli ya watafitiwa na upatikanaji wake. Pia, sura hii imeelezea eneo la utafiti, itikeli za utafiti, ukusanyaji

wa data, vifaa au zana za kukusanyia data na mbinu za ukusanyaji wa data ambazo ni mahojiano na udurusu wa maandiko. Halikadhalika, vipengele vya mchakato wa ukusanyaji data na udhibiti wake, uhalali na uthabiti wa matokeo ya utafiti, uchanganuzi na uwasilishaji data vimeelezwa. Vipengele vingine ni mipaka ya utafiti, changamoto za utafiti na utatuzi wake pamoja na mpango wa tasnifu. Sura inayofuata inahusu, uchambuzi, mjadala na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI NA MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI

## 4.1 Utangulizi

Sura hii inahusisha uwasilishaji wa data na mjadala wa matokeo ya utafiti, pamoja na namna malengo yetu yalivyofikiwa. Data za msingi/awali zilitokana na sampuli iliyoteuliwa ya riwaya teule. Wakati data za upili zilitokana na watafitiwa pamoja na maandiko mengine ya kitaaluma. Aidha, sura imeanza kwa kueleza muhtasari wa waandishi pamoja na riwaya teule. Mjadala umegawanywa katika sehemu tatu ambazo zinaakisi malengo mahsusi ya utafiti huu. Sehemu ya kwanza inachanganua matukio katika riwaya teule ambayo hulazimika kufanyiwa uforensiki.

Sehemu ya pili inabainisha miktadha mbalimbali ambamo taaluma ya uforensiki hufanyika. Na, sehemu ya tatu inaangazia uhusiano wa kiforensiki uliomo kwenye riwaya na ule uliomo katika maisha halisi ya jamii. Aidha, mjadala na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti uliongozwa na Nadharia ya Uhalisia ambayo imeasisiwa na Hegel (1958). Nadharia hii inasisitiza kwamba, kazi ya fasihi yapaswa kuwa na ukweli, iliyowazi na inayozingatia masuala halisi na ya moja kwa moja, bila kupiga chuku.

## 4.2 Historia Fupi za Waandishi wa Riwaya Teule

Sehemu hii inatoa historia fupi za waandishi wa riwaya teule ambao ni Muhammed Said Abdulla (MSA), Beka Mfaume na Zainab M. Mwanga.

### 4.2.1 Historia Fupi ya Mwandishi Muhammed Said Abdulla (MSA)

Muhammed Said Abdulla alizaliwa tarehe 25/4/1918, katika mtaa wa Malindi Mji Mkongwe Zanzibar. Muhammed Said Abdulla alikuwa mtoto wa pekee wa Bw. Said

Abdulla na Bibi Anoi bint Mselem aliyetokana na ukoo wa Al-khalas kutoka Maskat. MSA, baada ya kujifunza kusoma Qur-ani, wazazi wake walimpeleka katika shule ya Serikali ya Kikoloni iliyokuwepo kwa wakati huo na kuanza kupata elimu ya msingi mwaka 1928. Na aliendelea na masomo hayo hadi pale alipo hitimu na kufanikiwa kujiunga na masomo ya sekondari mwaka 1938. Baada ya kuhitimu masomo ya sekondari, MSA aliajiriwa na kufanya kazi ya ukaguzi katika idara ya afya ya Serikali ya Kikoloni kwa muda wa miaka kumi (10). Mwaka 1948 alijiunga na taaluma ya uandishi wa habari na akawa mhariri wa magazeti likiwemo gazeti la Al- Mahda kutoka mwaka 1958 hadi alipoacha kazi hiyo mwaka 1968 (Sanga, 2012; Mjawiri, 2011).

Mwaka 1958, akiwa mhariri wa gazeti la *Mkulima*, nathari yake ya *Mzimu wa Watu wa Kale* ilipata tunzo ya juu ya heshima katika mashindano ya uandishi wa hadithi za Kiswahili. Mashindano hayo yaliandaliwa na shirika la uchapishaji la Afrika Mashariki. Kazi hiyo iliyochapishwa mwaka 1960 kama riwaya ilimtambulisha kwa mara ya kwanza mhusika Bwana Musa ambaye katika nathari za baadaye alipewa jina la Bwana Msa ili kusawiri ufupisho wa majina matatu ya mwandishi, yaani Muhammed Said Abdulla.

Muhammed Said Abdulla pia aliwahi kufanya kazi ya utayarishaji wa kipindi cha redio kilichoitwa “Sadiki Ukipenda” katika Sauti ya Unguja. Muhammed Said Abdulla alimuoa bibi Thrieyuu Muhammed Juma, maarufu kwa jina la Bi Mtumwa. Alibahatika kuzaa naye watoto wanne (4), wanaume wawili na wanawake wawili, ambao ni Abdul-rahman, Khadija, Fatma na Said. Mke wa MSA na watoto wake

Khadija na Fatma inasemakana waliuawa wakati wa Mapinduzi ya Zanzibar mwaka 1964. Muhammed Said Abdalla alifariki mwaka 1992 (Khamis, 2011).

Said Ahmed Mohamed katika kitabu chake kiitwacho Muhammed Said Abdullah (2011) anaeleza kuwa, MSA aliandika hadithi fupi iitwayo *Mke Wangu* na riwaya saba za kipelelezi ambazo ni:

i. *Mzimu wa Watu wa Kale* (1960)
ii. *Kisima cha Giningi* (1968)
iii. *Duniani Kuna Watu* (1973)
iv. *Siri ya Sifuri* (1974)
v. *Mke mmoja Waume Watatu* (1975)
vi. *Mwana wa Yungi Hulewa* (1976)
vii. *Kosa la Bwana Msa* (1984)

Inaaminika kuwa licha ya kuandika riwaya saba na hadithi fupi moja, MSA aliandika insha kadhaa. Miongoni mwa insha hizo ni pamoja na, Bwawani Hoteli, Utukufu wa Funguni na Mchuchu si Mchumba. Vitabu vyake vya *Mzimu wa Watu wa Kale* na *Kisima cha Giningi* ndivyo vilivyowahi kupata tunzo ya ubora ya sanaa. Pia, vitabu hivi vimekuwa na mchango mkubwa katika kuunda riwaya pendwa zenye sura ya upelelezi kwa waandishi fuatizi ambao huandika kazi zao kwa mtindo wa upelelezi, kwa lengo la kufichua uozo uliomo katika jamii.

Kisanii, MSA ameathiriwa sana na waandishi wa Ulaya kama vile, Arthur Conan Dayle. Said Ahmed Mohamed anaamini kuwa athari za Holmes ni jambo lililo dhahiri ambalo halikutokea kwa bahati mbaya bali lilikusudiwa baada ya MSA kuathiriwa na kuvutiwa na kazi za Edgar Allan na A. R Freeman ambao ni waandishi mashuhuri wa riwaya za Upelelezi. Katika uhalisi unapovutiwa na mtu ni wazi kuwa unaathiriwa naye na unapoathiriwa naye huwa unataka uwe kama yeye.

Kwa kupitia athari hizo ndipo Khamis alipoandika kuwa Bw. MSA ni Sherlverk Holmes wa Afrika.

### 4.2.2 Historia Fupi ya Mwandishi Beka Mfaume

Jina kamili la Beka Mfaume ni Bakar Mfaume Khamis[6] amezaliwa mwaka 1956 mkoani Tanga. Beka Mfaume ni mtoto pekee wa kiume katika familia ya mzee Mfaume Khamis wa mjini Tanga kwenye ukoo wa Mfaume uliokuwepo mjini Tanga takribani karne moja iliyopita. Beka Mfaume alianza masomo yake katika shule ya msingi iliyojulikana kwa jina la Matinishamba mwaka 1963. Aliendelea na masomo hadi alipohitimu masomo hayo ya msingi mwaka 1969. Alichaguliwa kujiunga na masomo ya sekondari katika shule ya sekondari ya Popatilali iliyopo Tanga. Hata hivyo, kutokana na ugumu wa maisha ya familia yake, alishindwa kuendelea na masomo zaidi. Jambo hilo lilisababisha safari yake ya kitaaluma iishie kidato cha pili.

Baada ya kushindwa kuendelea na masomo kutokana na hali ngumu ya maisha, aliamua kujiunga na mchezo wa mpira wa miguu kama sehemu yake ya ajira takribani kwa muda wa miaka sita. Baada ya hapo aliachana na mchezo huo baada ya kuona kuwa haukuwa na tija kwake. Beka Mfaume alianza kufanya kazi katika hoteli mbalimbali ikiwemo "Bahari *Beach Hotel"* (BBH) mnamo mwaka 1998 iliyomilikiwa na "Tanzania *Tourist Co-Oparation*". Kutokana na jitihada yake ya utendaji kazi, uongozi wa hoteli hiyo ulimchagua kuwa mmoja wa vijana waliopelekwa *Cypras* kuongeza ujuzi zaidi. Pia, alipata fursa ya kutembelea *Israel.*

[6] Maelezo hayo yanayohusu historia ya Beka Mfaume yamepatikana kupitia mahojiano kwa njia ya simu kati ya mwandishi mwenye Beka Mfaume na mtafiti yalifanyika siku ya Jumatano 28/02/2018 saa kumi jioni.

Vilevile, Beka Mfaume amewahi kufanya kazi katika meli mbalimbali za ndani na nje ya nchi akiwa kama baharia. Katika harakati zake za kutafuta maisha, aliwahi kutembelea na kuishi nchi kama vile Ugiriki na Dubai. Beka Mfaume ameoa na kupata watoto wawili, ambao ni Said aliyezaliwa mwaka 1982, na Latifa aliyezaliwa mwaka 1989. Said kwa sasa anaishi Kongo; na Latifa kwa sasa anaishi Dar es Salaam; na anafanya kazi katika Benki ya *CRDB.*

Katika taaluma ya fasihi, Beka Mfaume ni mwandishi mahiri wa kazi za fasihi ambaye alianza shughuli ya uandishi wa insha mbalimbali tokea yupo shuleni. Katika harakati za maisha aliyopitia alisoma kazi mbalimbali kama vile, riwaya, novela na hadithi fupi. Jambo hili lilimpa hamu na shauku ya utunzi wa kazi hizo. Hivyo, juhudi hizo alizozifanya zilimsaidia na kumfanya aingie katika tasnia hii ya uandishi. Hatimaye, kumfanya kuwa miongoni mwa waandishi wa Tanzania wenye mchango mkubwa katika jamii juu ya masuala ya kitaaluma.

Katika harakati za uandishi, Beka Mfaume amejikita kwenye uandishi wa riwaya pendwa kwa kiasi kikubwa. Kupitia riwaya zake, anaisemea jamii kwa kufichua uovu na kuonesha mwelekeo wa kupambana na uovu huo, ama unaofanywa na viongozi au wanajamii ambao wanamamlaka dhidi ya wengine. Beka Mfaume hadi sasa ameandika riwaya takriba tisa (9), riwaya hizo ni:

i. *Tufani* (1994)

ii. *Mwiba* (2009)

iii. *Dhihaka* (2013)

iv. *Mhanga wa Ikulu* (2015)

v. *Ndoa ya Haya* (2015)

vi. *Mary Mariam* (2016)

vii. *Mwanamji* (2016)

viii. *Mzee Beka* (2016)

ix. *Utakaso* (2017)

### 4.2.3 Historia Fupi ya Mwandishi Zainab M. Mwanga

Zainab M. Mwanga alizaliwa mwaka 1956 katika mkoa wa Singida nchini Tanzania. Alisoma na kupata elimu yake ya sekondari katika shule ya sekondari ya Mwenge iliyoko Singida. Aidha, Zainab M. Mwanga amepata mafunzo ya uhazili katika Chuo cha Uhazili mkoani Tabora. Baadaye alipata mafunzo ya uongozi (*personal management*) katika Chuo cha Watumishi wa Serikali jijini Dar es Salaam.

Zainab M. Mwanga alianza kuingia katika tasnia ya uandishi wa kazi za kifasihi katika miaka ya 1980. Kitabu chake cha kwanza kuandika ni riwaya ya *Kiu ya Haki* iliyopigwa chapa kwa mara ya kwanza mwaka (1983). Riwaya hii ndiyo ilimuingiza katika ulimwengu wa waandishi wa riwaya za Kiswahili nchini Tanzania. Pia, amewahi kuandika riwaya nyingine ijulikanayo kama *Hiba ya Wivu*. Zaidi ameandika hadithi mbalimbali za watoto ambazo zimechapishwa na tume ya UNESCO (Mwanga, 1984).

## 4.3 Muhtasari wa Riwaya za Waandishi Teule

### 4.3.1 Muhtasari wa Riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale*

Riwaya hii iliandikwa na Muhammed Said Abdulla katika mwaka 1957/58, na kupigwa chapa mwaka 1960. Ingawa ni kazi ya kubuni, lakini inakamilisha uhalisi wa maisha ya kila siku tunayoishi katika jamii zetu. Riwaya hii inaonesha mambo yenye utata katika mauaji (uhalifu), na namna ambavyo mpelelezi wa kujitegemea

anatatua migogoro na mikanganyiko inayotawala katika vichwa vya watu. *Mzimu wa Watu wa Kale* ni riwaya yenye kisa cha ugunduzi wa mauaji ya Bw. Ali wa Makame ambaye amekabidhiwa mali ya Yunusu aitunze mpaka mtoto wake, Ahmed, atakapokuwa mkubwa ndipo amkabidhi. Lakini, Bw. Ali anaifanya mali hiyo kama yake na kutomjali mwenye mali.

Kwa vile Bw. Ali alipata fedha za kuchezea wakati alipokuwa Kongo, akawa anatembea na wake wa watu, na hatimaye, akavunja nyumba ya Mwarabu. Mwarabu amfuata Bw. Ali anapotaka kusafiri kwa lengo la kukimbia, alimuwahi na kumshindilia jambia ambalo lilimtenganisha na dunia. Bw. Ali alipouawa na Mwarabu, Baniani Seti wakishirikiana na boi wake, walizichukua pesa alizokuwa nazo na kuficha maiti kichakani. Kutokana na historia ya mzimu, iliaminika kuwa, Bw. Ali ameuawa na nguvu za vizuu vya mzimu. Pia, Baniani na boi wake ndio wanaonekana kuhusika na mauaji hayo ya Bw. Ali. Hata hivyo, Bwana Msa mchunguzi maarufu anadhihirisha ukweli kwamba, Bw. Ali aliuawa na Mwarabu aliyekuwa amevunjiwa nyumba wakati akiwa Kongo. Baniani na boi wake walikuwa wameiba pesa kutoka kwa maiti baada ya kifo. Hivyo basi, riwaya hii, kwa kiasi kikubwa, inaonesha utetezi wa watu wanaodhulumiwa haki zao katika jamii.

### 4.3.2 Muhtasari wa Riwaya ya *Mhanga wa Ikulu*

Riwaya hii imeandikwa na Beka Mfaume mwaka 2015 kwa umahiri na weledi mkubwa. Pia, hii ni riwaya iliyojaa taharuki nyingi. Riwaya hii imezungumzia mambo ambayo hufanywa na wanajamii wa kawaida au viongozi wa vyama na serikali kwa lengo la kujinufaisha wao binafsi kwa kujiongezea kipato au kujitafutia

umaarufu katika jamii zao. Katika riwaya hii, mwandishi amemzungumzia Mheshimiwa Zumo kama mhusika mkuu na kiongozi katika chama chake cha siasa (chama tawala) juu ya uhalifu aliotenda dhidi ya mke wake. Mhusika huyu anamuua mke wake kwa makusudi kama mhanga wake ili apatiwe nafasi ya kugombea urais katika chama chake. Kutokana na kufanya tukio hili kwa usiri mkubwa, ikaonekana kuwa mke wake amekufa ghafla kwa ajali ya gari miezi michache kabla ya kufanyika kwa uchaguzi mkuu. Jeshi la Polisi na vyombo vya habari na hata hati ya kifo chake vinathibitisha kuwa kifo hicho kilitokana na ajali ya gari alilokuwa akiliendesha mwenyewe.

Miezi sita baadaye, wakati kampeni za urais zinapamba moto, anajitokeza mtu mmoja anayedai kuwa, mke huyo wa kigogo hakufa kutokana na ajali ya gari bali aliuawa; huku akidai kuwa na ushahidi unaothibitisha hilo. Anataka kifumba mdomo cha fedha taslimu shilingi bilioni mbili kutoka kwa mume wa mwanamke huyo, vinginevyo angeuweka ushahidi huo kwenye mitandao au kuwapa wapinzani. Kufanya hivyo kungewasaidia kushinda uchaguzi huo kwa mara ya kwanza.

Katika mazingira yenye utata, taarifa hizo zinafika katika taasisi ya usalama wa taifa ambao nao wanahaha kumtafuta mtu huyo. Jambo hili linakuwa ni mwanzo wa kuibuka kwa yaliyojificha nyuma ya pazia. Mtu huyo anagundua kuwa maisha yake yapo hatarini, wakati anapojaribu kuwakimbia watu wa taasisi hiyo ya usalama wa taifa, ndipo anagundua kuwa mambo mengine yanazidi kuhatarisha maisha yake na wanajamii wengine. Hatimaye, anaamua kupambana ili kuona haki inatendeka dhidi ya mhusika mkuu wa uhalifu, Mheshimiwa Zumo, na wale wote wanaomlinda na kumtetea hali wanajuwa kuwa ni mhalifu.

### 4.3.3 Muhtasari wa Riwaya ya *Kiu ya Haki*

Riwaya ya *Kiu ya Haki* ilipigwa chapa kwa mara ya kwanza katika mwaka 1983. Riwaya hii ina mawazo yaliyopangwa kwa ufasaha na kuleta mtiririko mzuri wenye kupendeza, ikionesha msuguano wa maisha katika jamii. Riwaya hii inaonesha maovu mengi ambayo yanatendwa na baadhi ya wanajamii huku wakishirikiana na baadhi ya viongozi wa serikali. Kutokana na uovu uliokithiri, uadilifu na wema vikaanza kudhihakiwa. Ubinafsi wa viongozi, ukatili pamoja na ufisadi wa wala rushwa vikaongezeka. Pia, wanajitokeza watetezi wa haki kama vile, Mzee Toboa na mke wake pamoja na Inspekta Paukwa wakikamata bango la utetezi wa haki na kupinga maovu katika jamii na taifa kwa jumla. Hawa wanapambana kwa kila hali ili kuhakikisha uovu katika jamii hiyo unamalizika kabisa, na haki inapatikana kwa mwenye haki. Hivyo, tunaweza kusema kuwa *Kiu ya Haki* ni hadithi inayotetea wanyonge kwa lengo la kupingana na uonevu, unyanyasaji na dhuluma katika jamii.

## 4.4 Matukio Ambayo Husababisha Kufanyika kwa Uforensiki katika Riwaya Teule

Matukio ni wingi wa neno tukio, likiwa na maana ya jambo lililofanyika au lililotokea. Katika mada hii tunachanganua matukio yanayosababisha kufanyika kwa uforensiki katika riwaya za waandishi teule. Mara nyingi matukio haya huambatana na uhalifu/ jinai. Miongoni mwa matukio hayo ni ujambazi, mauaji, ubakaji na mengine mengi. Uforensiki (upelelezi) hufanyika katika maeneo ambayo matukio hayo yametendeka kwa lengo la kumpata mtendaji ambaye hujulikana kama mhalifu.

Matukio mbalimbali ambayo hujitokeza katika jamii zetu, yakiwemo yale ya uhalifu, ndiyo huwahamasisha waandishi wa kazi za kifasihi kuyabainisha kupitia kazi zao kwa lengo la kuiamsha na kuielimisha jamii husika. Yakub[7], akitaja matukio ambayo yapo katika uhalifu na hujulikana kama makosa ya jinai, alieleza kuwa, ni jumla ya matukio yote ambayo hayaingii katika makosa ya madai. Anataja baadhi ya matukio hayo kuwa ni kubaka, kuiba, kutukana, kulawiti, kupigana, kuharibu mali, kujeruhi, kutoa na kupokea rushwa, utumiaji wa madawa ya kulevya, uhaini, mauaji, ujambazi na kughushi. Anaendelea kueleza kuwa, makosa haya ya jinai husimamiwa na kushughulikiwa na serikali, na si mtu aliyetendewa kosa hilo. Makosa ya madai ndiyo hushughulikiwa na kusimamiwa na mtu mwenyewe anayedai. Katika kazi za kifasihi, matukio ndiyo hutumika kuunda kazi hizo. Hivyo, matukio hayo huenda sambamba na maisha halisi ya jamii kwa sababu mwandishi huakisi yaliyomo kwenye jamii husika (jamii inayomzunguka).

Wamitila (2003:55), akifafanua juu ya utokeaji wa matukio katika kazi za kifasihi anasema kuwa, "Matukio hayatokei tu, bali hutokea kwa kuwa mwandishi anataka kuliendeleza swali fulani au nia fulani maalumu". Katika kufikia lengo la utafiti huu, ambalo liliongozwa na swali la msingi lisemalo, Je ni matukio gani yaliyomo katika riwaya teule yanayosababisha kufanyika kwa uforensiki? Mtafiti alitumia mbinu ya mapitio ya maandiko, majadiliano na udodosaji kwa lengo la kuchunguza na kuchambua matukio mbalimbali ya kihalifu katika riwaya teule ambayo huhitaji kufanyika kwa uforensiki. Hivyo, kwa kutumia mbinu hizo, utafiti huu uliweza kugundua matukio tofauti yaliyopaswa kufanyiwa uforensiki katika riwaya teule hizo, na kuyaangaza kwa kina.

[7] Haji Yakub ni mwanasheria ambaye alifanya mahojiano na mtafiti katika ofisi yake iliyopo katika Mkoa wa Mjini Magharibi Zanzibar Aprili 26/2018, Saa 4: 45 asubuhi.

Utafiti ulibaini kuwa, kwa kiasi kikubwa, matukio katika riwaya teule yamejitokeza katika makundi na miktadha tofauti iliyosawiriwa na waandishi hao. Aidha, data hizo zilionesha kuwa matukio hayo hudhihirika (hutokea) kutokana na sababu tofauti kama vile, tamaa ya kupata mali, mapenzi, kupata cheo na sababu nyingine nyingi. Data zilifanyiwa uchambuzi na mtafiti kupitia matukio mbalimbali ya kihalifu yaliyojitokeza katika riwaya teule kama ifuatavyo:

### 4.4.1 Tukio la Mauaji

Uhalifu ni utendaji wa jambo lolote lililokatazwa kutendwa kisheria au kwa sheria ndogondogo za mtaa, kijiji, kitongoji, kata/shehia au halmashauri. Uhalifu ni wizi au kufanya matendo ya jinai. Mauaji ni tukio la kuondoa uhai wa mtu au kiumbe chochote kile kwa makusudi au kwa bahati mbaya. Mauaji ni moja kati ya matukio ya uhalifu, na ni kosa la jinai kisheria. Hii ni kwa sababu ni tendo ambalo hudhoofisha maendeleo ya mtu, jamii na taifa kwa jumla. Ikumbukwe kuwa, uhalifu haupendwi na mtu yeyote Yule; maana hata mhalifu mwenyewe hapendi matendo ya kihalifu. Hii ni kwa sababu hata akikamatwa huwa anasikitika kwa sababu ya matendo machafu aliyoyafanya kwa kujuta na kuomba msamaha, msaada, na kuhurumiwa (Matho, 2013).

Kosa la jinai ni lile linalofanywa na mtu/watu au taasisi fulani kinyume na taratibu za kisheria. Aliyefanya kosa huwa anaadhibiwa na serikali, ingawa aliyemkosea inawezekana si serikali bali ni raia wa kawaida au chombo chenye hadhi ya kuweza kusimama kisheria. Serikali, kupitia polisi, hufanya upelelezi kutokana na tuhuma zilizoripotiwa polisi kuhusiana na makosa haya ya jinai. Polisi inapogundua kwamba tuhuma hizo ni za kweli humshtaki mahakamani yule aliyetuhumiwa kutenda kosa

hilo. Kesi huendeshwa na waendesha mashtaka walioteuliwa na Mkurugenzi wa Mashtaka. Mahakama nayo, kwa kufuata taratibu zake, husikiliza kesi kwa misingi ya kisheria, na baadaye humuhukumu mtu aliyefanya kosa. Hukumu inaweza kuwa ni faini, kutumikia chuo cha mafunzo, au kuitumikia jamii. Faini hupokelewa mahakamani, lakini kutumikia chuo cha mafunzo na kuitumikia jamii husimamiwa na Idara ya Chuo cha Mafunzo[8].

Matukio au makosa ya jinai yanaweza kugawanywa katika aina mbalimbali kutegemeana na maudhui yanayozungumzwa. Yapo makosa/ matukio ya jinai ambayo mtuhumiwa anaweza kukamatwa bila ya mkamataji kuwa na hati ya kukamatia. Makosa haya ni yale yanayotendeka waziwazi kama wizi; ujambazi, mauaji na uhaini. Pia, yapo yanayohitaji hati ya kukamatia ili uweze kumkamata mtuhumiwa. Mfano mzuri ni kosa la kula njama na kufanya udanganyifu. Kwa yale makosa yasiyohitaji hati ya kukamatia hata mtu wa kawaida anaweza kumkamata mtuhumiwa na kumuweka chini ya ulinzi, lakini anatakiwa amkabidhi haraka iwezekanavyo kwa vyombo vinavyohusika (Peter, 2009).

Tukio hili la mauaji ni moja ya matukio mengi ya kihalifu ambayo waandishi wa kazi za kifasihi huyazungumzia katika kazi zao kwa kuakisi uhalisi wa maisha katika jamii. Ni dhahiri kuwa, ndani ya jamii nyingi mauaji hutokea kutokana na sababu tofauti kama vile, mapenzi, umasikini, ukosefu wa elimu, imani potofu za kishirikina, ukosefu wa ajira, kutokuwa na hofu ya Mungu na tamaa ya kupata mali au cheo. Hivyo, waandishi hujaribu kuyasawiri maisha halisi ya jamii kwa kupitia matukio mbalimbali, yakiwemo ya kihalifu ambayo yanaiathiri jamii na taifa kwa jumla.

[8] Maelezo hayo yalitolewa na ndugu Juma S. ambaye ni mmoja wa wanasheria katika kituo cha huduma za sheria Zanzibar kilichopo kisiwani Pemba akiwa katika mahojia na mtafiti tarehe 05/03 2018.

Katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* mwandishi amelionesha tukio hili la mauaji ya Bw. Ali ambalo limezua taharuki na utatanishi mkubwa katika jamii hiyo. Bwana Ali hakurudi nyumbani kwake, na hatimaye akaonekana kuwa ameuwawa kwa kukatwa kichwa akiwa mzimuni. Jambo hili lilipaswa kufanyiwa upelelezi ili kupatikana mhalifu aliyehusika na mauaji hayo. Mwandishi anaonesha tukio hili la mauaji kwa kusema:

> Alikuwa ameketi chini hali ameegemea kaburi lenyewe na miguu yake kainyoosha kwa mbele. Lakini mtu huyu alizidi kutisha kwa jambo moja. Kichwa chake badala ya kuwepo mahali panapohusu, juu ya mabega yake, hakikuwepo hapo. Mtu huyo alikuwa amekipakata kichwa chake mapajani… Najum alisimama palepele mpaka Bwana Msa alipofika makaburini akampigia kelele mwenziwe, "Njoo, Najum! Njoo umtazame Bwana Ali kakatwa kichwa!" Najum akazidiwa na hofu. Kumbe yule aliyekuwa amekaa pale chini ya kaburi, hali amenyoosha miguu yake na kupakata kichwa chake alikuwa Bwana Ali! Nini kilichompeleka mzimuni magharibi … (uk: 39 - 40).

Katika nukuu hii mwandishi ameonesha jinsi tukio la mauaji ya Bwana Ali lilivyokuwa na jinsi lilivyozua taharuki kubwa katika jamii ile. Hii ni kwa vile ilikuwa ni mauaji ya kinyama na ukatili mkubwa sana. Mwandishi anaendelea kusimulia kuwa, Bwana Ali baada ya kukatwa kichwa aliwekwa makaburini na kunyooshwa miguu yake huku akionekana kupakata kichwa chake. Tukio hilo la mauaji linaashiria ukatili ambao hutokea katika maisha halisi ya jamii. Hii ni kwa sababu wapo wanajamii ambao hutenda uhalifu kutokana na hasira ama chuki binafsi waliyonayo juu ya mtu aliyewafanyia uhalifu huo. Vilevile, inawezekana hufanya hivyo kwa lengo la kulipa kisasi.

Tukio kama hili likitokea katika jamii, hujitokeza raia wema ambao huweza kutoa taarifa katika taasisi za ulinzi na usalama kama vile polisi kwa ajili ya kufanyiwa

uchunguzi wenye lengo la kumpata mhalifu aliyetenda uhalifu huo. Jambo hili linadhihirika pia kwenye riwaya hii ambapo Bwana Msa na Najum wanatoa taarifa katika kituo cha polisi (uk: 51-52).

Tukio lingine la mauaji ambalo mwandishi Muhammed Said Abdulla amelionesha katika riwaya yake ya *Mzimu wa Watu wa Kale* ni tukio la mauaji ya Sharif Halw na mtoto wake yaliyofanywa na Sufra. Mwandishi anasema:

> 'Wewe ajali yako mikononi mwangu.' Hata siku ile yule Sharifu alikuwa akichagua lozi za halwa yake kainama na kichwa chake kanyoa, cheupe. Ala! Sufra alivyotoka akaenda akalitumbukiza jisu lake lote ndani ya kichwa cha Sharifu, na mtoto wake aliyekuwa akisonga halwa, alikwenda kutaka kumsaidia baba yake. Sufra alimtia nalo ubavuni, akawauwa wote wawili… Ah? (uk: 63).

Katika nukuu hii mwandishi amekusudia kuifahamisha jamii kuwa, matukio ya kihalifu yapo ambayo hufanywa kwa usiri mkubwa na pia yapo ambayo hufanywa waziwazi. Hapa tunamuona mhusika Sufra alivyofanya mauaji ya kikatili sana kwa kumchoma Sharifu kisu cha kichwa na mtoto wake alimtia kisu cha ubavuni na hatimaye kukata maisha yao. Matukio kama haya ya uhalifu ambayo hufanywa hadharani (yaani hufanywa waziwazi) bila uficho wowote ule jamii inapaswa kuwa na hadhari kubwa katika kupambana nayo. Hii ni kwa sababu ni matukio ya hatari zaidi katika jamii, na wanajamii wenyewe wanapaswa kuchukua hatua za dharura kutoa taarifa kwa vyombo husika au kuwakamata wahalifu hao, kwani hayo ni matukio ambayo hayahitaji hati ya kukamatia. Kama ilivyoelezwa katika sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai sura ya 20 (uk: 21) kuwa, iwapo kutokana na taarifa zilizopokelewa au kwa njia nyingine yoyote afisa polisi ana sababu za kushuku utendekaji wa kosa au kuhisi uvunjwaji wa amani. Anatakiwa pale inapobidi, kwenda yeye mwenyewe katika sehemu hiyo kupeleleza ukweli wa mazingira ya

kesi hiyo na kuchukua hatua zinazofaa kutambua na kukamatwa kwa mhalifu huyo. Iwapo kosa ni lile ambalo anaweza kukamata bila hati. Kwani, yapo makosa ya jinai ambayo mtuhumiwa anaweza kukamatwa bila ya mkamataji kuwa na hati ya kukamatia. Makosa haya ni yale yanayotendeka waziwazi kama, wizi, ujambazi na mauaji.

Kwa upande wa riwaya ya *Mhanga wa Ikulu*, mwandishi Beka Mfaume ameonesha namna mauaji ya kikatili yalivyojitokeza. Mauaji hayo yamesababishwa na wanasiasa kwa lengo la kujitafutia umaarufu na kupata cheo. Chuachua (2010), akifafanua juu ya wanasiasa, anaeleza kuwa, mwanasiasa ni mtu yeyote anayejihusisha kwa vitendo au kwa nadharia katika mambo yahusuyo mfumo wa utawala wa nchi. Kwa maana hiyo basi, tunaweza kuona kwamba, mwanasiasa anaweza kusababisha matukio makubwa ya kihalifu kwa lengo la kujinufaisha binafsi ama kwa kujipatia cheo au kulinda chama chake. Mwandishi amelithibitisha hili la kufanya mauaji kwa lengo la kupata cheo pale alipomtumia mwanasiasa, Mheshimiwa Zumo, mgombea urais katika chama tawala kwa kusema:

> Baada ya kuonekana kuridhika kuwa hakukuwepo mtu, mwanaume huyo alifungua mlango wa nyuma wa abiria. Akasita, akawa kama mtu anayesubiri atoke kwenye gari hilo... Kisha aliinama, na kutumbukiza kiwiliwili chake ndani ya gari na kuanza kukukuruka na kulifanya gari hilo litingisike. Hatimaye alianza kujitoa kwa kurudi kinyumenyume huku akijaribu kudhibiti kitu anachokivuta. Hatimaye akautoa mwili wa mtu… Frank aliendelea kumpiga picha mtu huyo ambaye aliendelea kukururuka na mwili alioubeba. Akamwona akiuhamisha mwili alioutoa na kuuingiza sehemu ya dereva ambako aliukalisha kwenye kiti cha dereva… Frank akamwona mtu huyo akienda nyuma ya gari nakuanza kulisukuma kuelekea ukingoni mwa miamba iliyokuwa pale. Akatambua kusudi la mtu huyo ni kulitumbukiza gari hilo baharini ambako kuna kina kirefu. Akamwona mtu huyo akibadili mbinu kulisukuma gari hilo. Akawa ameuegemeza mgongo wake

> kwenye gari na kuonekana kutumia nguvu nyingi, mara alipoliona limekubali kusogea kwenye kasi aliyoitaka, mtu huyo aligeuka tena na kulisukuma kwa kutumia mikono yake na kuzidisha kasi ya kulisukuma hadi lilipofika ukingoni mwa miamba… Mshindo mkubwa wenye nguvu wa kitu kizito kilichotumbukia baharini ulisikika… Siku hiyo vyombo vyote vya habari nchini vikatangaza kifo cha mke wa Mheshimiwa Zumo (uk. 7- 8).

Katika nukuu hii mwandishi anadhihirisha ubaya wa baadhi ya wanasiasa ambao hawajali maisha na maslahi ya wananchi wao. Kiongozi huyu wa siasa ambaye ni katibu mkuu wa chama chake aliamua kumuua mke wake kwa lengo la kutoa mhanga ili chama chake kiweze kumchagua yeye kama mgombea urais. Wakati anafanya tukio hilo la kihalifu, aliamini kuwa hakuna mtu aliyeweza kumuona wala aliyejua nini kinachotendeka. Jambo hili linaashiria matokeo mabaya ya uongozi wake. Hii ni kwa sababu anaonekana kuwa kiongozi ambaye hana nia njema na raia wake, na inadhihirika kuwa nia yake ya kuomba uongozi ni kwa ajili ya maslahi binafsi.

Mauaji mengine ambayo yamejitokeza katika riwaya ya *Mhanga wa Ikulu* ni yale yaliyofanywa na mhusika Farouk kwa kujiua mwenyewe akiwa ofisini kwake baada ya majadiliano na Bi Hidaya. Mwandishi anasema:

> DAKIKA zisizo zidi kumi toka alipoagana na Farouk ofisini kwake, Bi. Hidaya akiwa ameingia mara moja ofisini kwake kisha arudi nyumbani, alisikia aina ya hekeheka ya hatua za watu wanaopishana wakiwa wanaitana na kukimbia kwenye korido ya gorofa aliyokuwepo. Haikuwa kawaida kwa wafanyakazi kukimbia kwenye korido za jingo hilo... “Subiri” Bi. Hidaya alisema wakati akiufuata mlango… “Mzee amejipiga risasi!” mlinzi alisema. Kitu cha kwanza alichokifanya Bi. Hidaya ni kutuliza akili yake… (uk: 293).

Nukuu inatufahamisha kuwa, Farouk ambaye ni Mkurugenzi usalama wa taifa ameondoa uhai wake mwenyewe baada ya kijipiga risasi ya kichwa akiwa ofisini

kwake. Hali hii ilitokana na mazungumzo kati yake na Bi. Hidaya kufuatia masharti yaliyowekwa na Frank dhidi ya Mheshimiwa Zumo na Farouk mwenyewe.

Aidha, tukio jingine ni lile la kuuwawa kwa Mheshiwa Zumo akiwa katika mkutano wa kampeni zake za urais mjini Morogoro (uk: 300). Mwandishi anafafanua kwa kusema:

> Huo ndio wakati aliokuwa akiusubiri Cobra ambaye aliitegesha bunduki mbele ya uso wake, akafumba jicho moja na lingine lililokuwa wazi akalilengesha kwenye darubini iliyokufungwa juu ya bunduki hiyo. Kwa kujiamini pasipo na kufanya papara yoyote, Cobra aliilengesha shabaha yake kwenye kicha cha Zumo. Darubini ikakivuta kichwa cha mheshimiwa huyo na kukijaza katikati ya msalaba wa shabaha unaoonekana kwenye darubini. Zumo akawa anajaa kimiani! Kidole cha Cobra kilichokuwa kimetulia kwenye kiwambo cha kufyatulia risasi kikaanza kujivuta taratibu huku kikisubiri jicho liidhinishe na ubongo uamue. Piga! Cobra hakusubiri sekunde nyengine. Mlio mdogo wa kikohozi ukasikika kutoka katika bunduki hiyo! milio ya hofu ikasikika baada ya Mheshimiwa Zumo kukatiza alichokuwa akikizungumza na kupiga mwereka wa ghafla jukwaani…(uk: 300-301).

Nukuu inatufahamisha kuwa Mheshimiwa Zumo amepigwa risasi na Cobra wakati akiwa katika mkutano wa kampeni za uchaguzi mkuu mjini Morogoro. Haya ni matukio ya kusisimua na yanayozua taharuki katika jamii na taifa kwa jumla. Utafiti umegundua kwamba, matukio haya yalifanywa kwa lengo la kulinda hadhi ya chama na serikali, kwani waliona kuwa wamepoteza mwelekeo wa kupata ushindi kutokana na kugundulika kwa tukio la kihalifu lililofanywa na Mheshimiwa Zumo dhidi ya mke wake. Matukio kama haya ya mauaji ya viongozi wa vyama na serikali hujitokeza mara kwa mara katika jamii na huzua taharuki kubwa kwa wanajamii. Hivyo, vyombo vinavyohusika hupaswa kufanya uchunguzi wa kisayansi

(uforensiki) kwa lengo la kutambua sababu ya mauaji hayo, na hatimaye kumkamata mhalifu aliyehusika.

Matukio haya ya mauaji pia tunaweza kuyaona katika riwaya ya *Kiu ya Haki* pale ambapo mhusika Pondamali bin Malipesa anauwawa na rafiki yake wa karibu sana, Bwana Sikujua, kwa ajili ya hasira na tamaa ya mali. Mwandishi anasema:

> Ikawa vuta nikuvute. Ulizuka ubishi tukatoleana maneno hadi nikaamini kuwa kweli rafiki yangu alikuwa na nia ya kunidhulumu zile fedha kwa kunilaghai azifaidi peke yake. Nilikasirika na kumtamkia kuwa… Maneno hayo yalimkasirisha sana marehemu. Hasira yake ilimfanya aseme maneno mengi, hadi kunitolea siri ya maudhi ambayo mimi sikuwa naifahamu. Aliniambia eti mke wangu kamfilisi!... mimi kusikia hayo, damu ilinichemka, mapigo ya moyo yakabadili mwendo, nikajisikia kukosa pumzi! Mapenzi yangu kwa Pondamali dakika hiyo hiyo yaligeuka kuwa chuki. Nilimvamia kwa hasira tukaanza kupigana. Bahati nzuri bastola tulikuwa tumeshaziingiza katika mfuko uliokuwa na fedha, hivyo hakuna aliyewahi kuzitumia. Tulipeana makonde hadi nilipomshinda nguvu na kumwangusha chini. Nilimkalia tumboni, nilimkaba koo mpaka akakata roho (uk 28).

Tunaporejelea nadharia ya Uhalisia, tunaona kuwa mawazo yanayopatikana katika dondoo hili yanalandana na misingi wa nadharia hii. Tunaona kuwa, matendo ya mhusika Sikujua na Pondamali bin Malipesa yanalandana sana na msingi ule wa kuzingatia kwa hali ya juu uhalisi katika kuwasilisha maisha kupitia sanaa ya fasihi kwa kuyachunguza mawazo na matendo ya mhusika/wahusika katika kazi ya fasihi. Hivyo basi, matendo ya wahusika Sikujua na Pondamali bin Malipesa kugombana na kupigana hadi kusababisha mauaji ya mmoja wao kwa sababu ya mapenzi na tamaa ya mali ni jambo ambalo limezoeleka na limeenea sana katika jamii. Pia, dondoo hili linatoa mwanga kwa wanajamii kuwa, wawe makini wakati wa kuchagua marafiki, kwani marafiki wengine ni sawa na nyoka wenye sumu kali

ambao wanaweza kuwadhuru na kuleta maafa makubwa. Vilevile, wawe makini katika kufanya maamuzi ya mambo mbalimbali, kwani hasira ni hasara; na hawapaswi kufanya maamuzi wakati wanapokuwa na hasira, kwa sababu huweza kuwaletea majuto makubwa, kama anavyosema mwandishi "Ama kweli hasira hasara" (uk: 30).

### 4.4.2 Tukio la Wizi

Wizi ni moja kati ya matukio ya kihalifu, ambayo katika sheria mtu aliyeiba hushtakiwa kuwa ametenda kosa la jinai. TUKI (2004) inafafanua kuwa, "wizi ni tendo au tabia ya kuiba". Wizi unatokana na vitendo vya kikatili ambavyo hufanywa na watu wenye nia mbaya kwa mtu, taasisi ama kampuni. Mwizi ni mtu mwenye tabia ya kuchukua kisicho chake bila ya ruhusa au bila ya mwenyewe kumuona. Matendo haya yanapaswa kuonywa na kuzuiliwa kwa nguvu zote katika jamii ili yasitokee. Samweli (2015: 99) anasema kuwa, "Kuonya ni kumkanya mtu aachane na tabia yake isiyofaa au isiyokubalika kwa jamii". Tukio la wizi ni tukio ambalo linatokana na tabia mbaya ambayo haipendezi na wala haifai katika jamii. Hii ni kwa sababu ni miongoni mwa matukio ambayo hudumaza maendeleo na kuleta maafa makubwa kwa wanajamii hao. Waandishi wa kazi za fasihi hutumia taaluma yao kuelimisha jamii juu ya madhara hayo ya wizi. Katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* mwandishi anaonesha tukio hili la wizi pale anaposema:

> Leo natazama naona ufanga yangu hayuko mahl yake, la shaka nashkuwa yeye tu... "Alijibiwa, anha, natoka Maskat; asli yake Konga yeye, laakin baaden nasafir Maskat, ndio sasa nakugya Swahili." "Upanga ulioibiwa uli…" Mmanga aliruka, "Aaa! Si napiga kelele namna huyu. Hii aib, alitazama huku na huku, kisha akamaliza, kama mtu nasikia ufanga naibiwa"… haya niambie basi, upanga wako ulikuwa wapi? Mmanga alimjibu bila kunyanyua sauti "Ufanga ile kaan matundika ukuta ile katika ghala huyu 1-

> ley mabisha yule mgyeni nalala. Uttow yeye nakwenda zake na-" alizunguka huku na huku, kisha kwa sauti ya chini kama ananong'ona, Ufanga yangu mashkuwa (uk: 54-56).

Katika dondoo hili mwandishi anaionesha jamii kuwa, tukio la wizi linaweza kupoteza amani na imani ya mtu, kwani huloondoa uaminifu kwa wanajamii juu ya mtu huyo. Mwandishi anatufahamisha kuwa, Mmanga baada ya kufanyiwa upelelezi na polisi kwa kuanza kuulizwa maswali mbalimbali juu ya mauaji ya Bwana Ali, alikiri kuibiwa upanga wake na Mwarabu ambaye alikuwa anaishi naye kama mgeni aliyekuja kwa ajili ya kufanya kazi ya ulinzi nyumbani kwake. Upanga huo ulioibwa ndio ambao ulitumika katika kukata kichwa cha Bw. Ali, jambo ambalo lilizua mshituko na taharuki kubwa kwa jamii hiyo. Masuala haya ya wizi wa mali za watu katika maisha halisi tunayoishi yameshamiri sana na hurejesha nyuma maendeleo ya jamii. Pia, huiweka jamii hiyo katika hali ya kutokuwa na imani na mtu ambaye anadhani kuwa ni mwizi.

Kwa upande wa riwaya ya *Kiu ya Haki,* mwandishi Zainab M. Mwanga anasawiri tukio la wizi kama jambo ambalo linaathiri jamii kwa kuwa linaiweka jamii hiyo katika hali ya wasiwasi juu ya usalama wa maisha na mali zao. Mwandishi anasema:

> Alisubiri kwa hamu siku ambapo maovu yatatoweka kabisa. Lakini kila kukicha tamaa mbaya ya binadamu iliendelea kuichafua dunia na kuifanya iwe uwanja wa maovu. Leo fulani kaibiwa vitu nyumbani mwake, kesho mshahara wa wafanyakazi wa wizara fulani umeibiwa, kesho kutwa mtu fulani kaporwa saa ya mkononi kwenye UDA… Vituko hivi vilimkera sana Mzee Toboa. Alijitahidi kujua kila chanzo cha ovu analolisikia. Kila alipofanikiwa kumjua muovu ama chanzo cha maovu, hakusita kwenda kutoa taarifa kwa wanausalama kuhusu mtu au kikundi cha watu waliohusika na maovu hayo (uk: 2).

Mwandishi kupitia nukuu hii anaonesha kuwa suala la wizi limekithiri sana katika jamii, kwani wizi hutokea majumbani, maofisini na hata katika vyombo vya usafiri.

Hata hivyo, mwandishi anaendelea kuifahamisha jamii kuwa wapo raia wema ambao hukerwa na kukasirishwa sana na matendo hayo maovu ya kihalifu. Amemtumia mhusika Mzee Toboa kupambana na maovu hayo kwa jitihada zake zote, akifanya upelelezi kwa kutafuta kila chanzo cha ovu analolisikia na kutaka kumtafuta kila muovu. Pindi alipofanikiwa kugundua hakusita kwenda kutoa taarifa kwa wanausalama kuhusu mtu au kikundi kinachohusika na maovu hayo. Katika uhalisi wa maisha ya kila siku, matukio ya wizi yapo na, kwa kiasi kikubwa, yamekuwa kero kwa wanajamii. Watendaji wa matukio hayo ya kihalifu huyafurahia kwa sababu hujiongezea kipato katika kuendesha maisha yao ya kila siku, ijapokuwa kipato hicho ni kinyume na taratibu za maisha ya wanajamii hao.

Matukio kama haya yanayoambatana na wizi pia tunaweza kuyaona katika riwaya ya *Mhanga wa Ikulu*, pale mwandishi anapomuonesha mhusika Popo akitumia gari lake kwa ajili ya kukodishwa kubebea mali za magendo na wizi. Mwandishi anasema:

> Gari lao lilikuwa linapanda mabonde na mashimo yaliyokuwepo kwenye barabara hizo. Huko ndiko alikokuwa akikuhitaji, njia za mitaani! Alikuwa gwiji wa uzoefu wa njia hizo. Ni njia anazozitumia wakati gari lake likiwa limebeba mali za wizi nyakati za usiku linapokuwa limekodishwa kwa shughuli hizo (uk: 101).

Kupitia nukuu hii, mwandishi amekusudia kuionesha jamii kuwa tukio alilolifanya Popo la kukodisha gari lake kwa ajili ya kubebea mizigo ya wizi na mali za magendo ni tukio la kihalifu ambalo linaikwaza jamii. Mwandishi anamuonesha Popo kuwa ni dereva mzoefu katika njia ambazo si rasmi kwa usafiri wa magari. Njia hizo huwa anazitumia kwa ajili ya kusafirisha mizigo ya wizi wakati

anapokodishwa na watu wa usiku[9]. Hivyo, matendo kama haya yanapotokea katika jamii huwa ni kikwazo kikubwa kwa jamii hiyo katika harakati za kuleta maendeleo. Matukio haya hupaswa kufanyiwa uchunguzi kwa lengo la kudhibiti na kukomesha mwenendo huo wa kihalifu.

### 4.4.3 Tukio la Ujambazi

Ujambazi ni wizi wa kutumia nguvu. Ujambazi ni tendo la kikatili ambalo hufanywa na mtu, ama kikundi cha watu wenye nia ya kudhulumu mali au kujipatia kipato kwa kutumia nguvu. Mara nyingi ukatili huu hufanywa kwa kutumia silaha kama vile, visu, mapanga na bunduki. Ukatili ni matumizi ya nguvu yanayompa mtu fursa ya kumtumia au kumkandamiza mtu mwingine ikiwa ni pamoja na kumsababishia kifo, woga au hofu, madhara ya kimwili, kifikra na kisaikolojia (UWAKI; 2013). Ujambazi huweza kusababisha maafa na madhara kwa mtu, jamii au taifa kwa jumla ambapo tukio hilo hufanywa kwa madhumuni ya kujipatia kipato kinyume na utaratibu wa maisha unaozoeleka katika jamii. Mtu aliyetekwa na majambazi hunyimwa uhuru wa kufanya maamuzi na hulazimishwa kutenda kinyume na utashi wake. Suala hili la ujambazi limeelezwa katika riwaya ya *Kiu ya Haki* pale mwandishi aliposema:

> Baada ya kufika nusu ya safari, nilistukia abiria aliyekuwa kiti cha nyuma ananilenga bastola kisogoni na kuniamrisha nisimamishe gari kando ya barabara kwa usalama wangu. Aliniamuru niinue mikono juu na kumfuata atakakoniongoza. Sikuwa na jengine bali ni kufuata amri. Moyoni sikuwa na shaka kwamba huo ndio ulikuwa mwisho wangu. Nilijuta kumwacha mwenzangu… Yule abiria aliyenilenga bastola aliniongoza hadi kichakani, ambako alinipekuwa na kuchukuwa shilingi 200/= na saa ya mkononi. Abiria aliyebaki kwenye gari nilijua naye

[9] Hawa ni watu ambao huutumia usiku kwa ajili ya kufanya matukio mbalimbali ya kihalifu kama vile wizi wa mali nabiashara haramu ya magendo.

> anafanya shughuli ya kufungua kisanduku cha fedha, ambamo mlikuwa na shilingi elfu mbili maana funguo alikuwa nazo…. (uk: 20).

Tulipoyaangaza maelezo yaliopo juu, tuliweza kuona kwamba mwandishi alikusudia kuifahamisha jamii kuwa, ujambazi ni tukio la kihalifu ambalo hufanywa kwa kutumia nguvu nyingi na za ziada. Hii ni kwa sababu watu wanaojishughulisha na matukio hayo ya ujambazi waliweza kutumia silaha za moto kama vile bastola ili kuyateka nyara magari ya Sikujua na Pondamali na kufanikiwa kupora fedha na saa ya mkononi. Killa yuko tayari kuua ili apate mali, Somba yeye hajali kitu cha mtu bali huchukua tu kwa kutumia nguvu na Kazamoyo hujilazimisha kukaza moyo wake kwa kutenda maovu kama hayo ya ujambazi.

Aidha, mwandishi, katika kuonesha ubaya wa tukio la ujambazi, ameamua kutumia nafasi yake kwa lengo la kuifumbua macho jamii ili iweze kupambana na kuondoa matukio haya maovu ambayo yanaweza kusababisha madhara makubwa katika jamii. Ameeleza kuwa, majambazi hutumia zaidi nyakati za usiku kuhujumu mali za wananchi. Kwa mfano, Sikujua tumeelezwa kuwa, aliingiliwa na majambazi wakati wa usiku na kuibiwa fedha. Mwandishi anafafanua hilo kwa kusema:

> Mzee Toboa alipofika nyumbani kwake, mkewe alimpa habari ya kusikitisha kuhusu Sikujua. Alimwambia kuwa, Sikujua aliingiliwa na majambazi usiku wa Jumanne, yani jana, saa saba na nusu usiku. Aliibiwa pesa zote na vitu vyengine… Tangu Ijumaa ya mkasa ule yale majambazi yalikuwa yakisoma nyendo za Sikujua na kule anakoishi. Yalipofanikiwa kumjua vema nyumba anyoishi, saa anazorudi nyumbani na chumba ancholala, yalimnyemelea usiku huo wa Jumanne na kupora fedha zote alizokuwa nazo pamoja na bastola tatu. Sikujua aliyatambua majambazi yale ingawa ilikuwa usiku wa manane (uk: 40).

Mwandishi ameonesha kuwa mmoja wa wahanga wa tukio la ujambazi ni Sikujua ambaye aliingiliwa na majambazi hayo wakati wa usiku na kumuibia fedha zote na

vitu vingine vilivyokuwepo ndani. Pia, tunafahamishwa kuwa, majambazi huanza kufuatilia nyenendo zako hadi pale watakapojiridhisha ndio hufanya uvamizi huo, kama vile ambavyo walifanya kwa Sikujua. Kihalisi, matukio kama haya huwa yanajitokeza mara kwa mara katika mazingira yetu tunayoishi. Wapo wanajamii ambao wamewahi kupatwa na matukio kama haya ya ujambazi yaliyosababisha kupoteza mali zao nyingi na hata familia zao. Kwani majambazi wanapovamia katika makaazi ya watu au katika sehemu za biashara huthubutu hata kuua ilihali wafanikishe walichokusudia kutenda.

### 4.4.4 Tukio la Utekaji Nyara

Suala la utekaji nyara ni moja kati ya matukio ya kihalifu ambayo huhitaji kufanyiwa uchunguzi pindi linaporipotiwa kutokea katika jamii. Matukio haya hujitokeza mara kwa mara katika jamii zetu licha ya serikali kuyakemea vikali. Katika harakati za kupambana na uhalifu huu, jamii hulazimika kutoa ushirikiano ambao husaidia kudhibiti matukio hayo ya uhalifu. Utekaji nyara ni kitendo cha kuchukua mtu/ watu au vitu kwa nguvu kwa kusudio la kulipwa fidia au kutimiziwa haja fulani. Hali hii ya utekaji nyara inaweza kusababisha madhara na maafa makubwa katika jamii, kwa sababu ni kitendo cha kuingilia uhuru wa mtu. Wahalifu wa matukio haya huona kama matukio ya kawaida; na moja kati ya biashara muhimu kwao ambayo huwapatia kipato cha kutosha huku wakiwaacha wahanga wa matukio haya wakidhalilika na kuteseka.

Waandishi wa kazi za fasihi wameliona jambo hili na kuanza kulisemea katika kazi zao. Utekaji nyara ni tukio la kihalifu lenye madhara na maafa katika jamii. Pia, hurejesha nyuma maendeleo ya jamii na taifa kwa jumla. Katika riwaya ya *Kiu ya*

*Haki*, mwandishi Zainab M. Mwanga amelionesha tukio hili kwa kumtumia mhusika kijana ambaye ni dereva wa teksi aliyemteka nyara abiria wa kigeni kwa lengo la kujipatia fedha na mali aliyokuwa nayo. Msanii anasema:

> Mumewe alimwambia kuwa, anamtilia shaka kijana mmoja dereva wa teksi ambaye alimshitaki kwa kosa la kumteka nyara abiria mgeni kutoka Kigoma. Kijana huyo alijipatia vitenge kutoka nchi jirani na fedha za kigeni kutoka kwa abiria huyo. Baada ya Mzee Toboa kutoa taarifa hiyo kijana huyo alipelelezwa na kupatika na mali ya nchi hiyo (uk: 36).

Tukio hili la utekaji nyara ambalo lilifanywa na dereva wa teksi linaonesha hali ya uovu na uhalifu uliokithiri katika jamii, ambapo watu hujitafutia kipato kwa njia zisizo za sahihi. Hata hivyo, wapo raia wema ambao hukerwa na matendo hayo maovu na kuamua kuchukua hatua zinazofaa ili kupambana na maovu hayo. Mwandishi amemwonesha Mzee Toboa akichukia sana tendo hilo, na hivyo, kuamua kutoa taarifa kwa polisi ili kijana huyo aweza kuchunguzwa. Kijana huyu anawakilisha watenda maovu katika sehemu zao za kujitafutia maisha ya kila siku na Mzee Toboa anawakilisha watetezi wa haki na wapinga maovu katika jamii zao.

Aidha, tukio jingine la utekeji nyara linawapata Sikujua na rafiki yake, Pondamali, wakati wakiwa katika harakati zao za kujitafutia maisha. Wakiwa katika hoteli ya Mtukunywa, Sikujua ambaye ni dereva wa teksi alipata abiria wawili na Pondamali alipata abiria mmoja. Hawa hawakuwa abiria wema, bali walikuwa ni majambazi ambao waliwateka nyara madereva hao wa teksi (uk: 20-21). Kitendo hicho kinaelezwa na mmoja wa majambazi hao ambaye ni Kazamoyo baada ya kutokea kifo cha Pondamali ambaye ni miongoji mwa madereva waliotekwa nyara na majambazi hao. Mwandishi anasema:

> Mtayaona: Endelea Kazamoyo, unaruhusiwa kueleza ukweli. Kazamoyo: Sisi tuliteka nyara teksi mbili na sio

> teksi moja kama mashtaka yanavyodai. Teksi moja ilikuwa namba DTS 00010 na teksi ya pili ilikuwa namba LMX 03001. Baada ya kushindwa nguvu na madereva wa teksi tuliowateka nyara tulikimbia na kuwaachia shilingi laki mbili na nusu na bastola tatu. Kwa maelezo haya tusingeweza kujua aliyemuua dereva wa pili wa teksi. Kama dereva wa pili wa teksi aliyekuwa na marehemu angaliweza kupatikana, yeye angaliweza kuisaidia sana Mahakama kutoa haki kwa wenye haki, maana yeye ndiye anajua ni nani aliyemuuwa dereva wa teksi mwenzake kama sio yeye aliyemuua (uk: 63).

Katika dondoo hili tumeoneshwa namna mhusika Kazamoyo alivyoisaidia mahakama katika kesi hii ya mauaji ya Pondamali kwa kuzungumza ukweli ulioambatana na ushahidi wa tukio hilo la utekaji nyara; ambapo, alithibitisha kuwa wao waliteka nyara teksi mbili na wala sio moja. Hivyo, aliomba apatikane dereva wa pili wa teksi huenda akawa anamjua muuaji wa dereva mwenzake kama sio yeye aliyemuua. Pia, nukuu inaonesha kuwa pindi akipatikana dereva wa pili wa teksi ambazo zilitekwa nyara na majambazi hao huenda akajulikana muuaji. Kwani, watekaji nyara hao wanadai kuwa walishindwa nguvu na madereva waliowateka nyara, na hatimaye, kuamua kuwaachia fedha na wao kukimbilia porini.

Kimsingi, utekaji nyara ni jambo ambalo lina uhalisi katika jamii, ambapo siku hizi matukio haya yamekuwa mengi sana katika jamii zetu. Uhalifu huo haufanywi katika shughuli hizo za teksi tu, bali hata katika mambo mengine ya kijamii kama vile, harakati za kidini, kisiasa, biashara na hata katika mahusiano ya kimapenzi. Yapo na makundi kadha ya wahalifu kama vile, watu wasiojulikana, mbwa mwitu pamoja na mazombi. Makundi haya huiathiri jamii, kiuchumi, kimawazo na hata kisaikolojia. Aidha, huwafanya wanajamii hao kukosa amani na utulivu katika maisha yao. Ongezeko la kadhia hii ya utekaji nyara katika jamii linaweza kutokana

na sababu kama vile, kujipatia fedha au utajiri, kujilimbikizia mali kwa ajili ya maslahi binafsi na kulinda heshima ya mkubwa ama chama fulani.

### 4.4.5 Kutoa/Kupokea Rushwa

*Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2004: 153) ikifafanua juu ya rushwa, inasema kuwa "Rushwa ni fedha au kitu cha thamani kinachotolewa na kupewa mtu mwenye madaraka ya jambo fulani ili mtoaji apatiwe upendeleo". Hutokea pale ambapo mtu mmoja hutoa kitu chochote cha thamani kwa mtu mwengine kwa minajili ya kupata upendeleo asiostahili (kuhudumiwa kwa haraka kwa kutofuata utaratibu unaotakiwa kisheria), kushawishi na kuyapindua maoni ya mtu mwengine, au kupata manufaa ambayo mtoa rushwa hastahili kuyapata. Wapo baadhi ya watu hupenda kupewa fedha au kitu cha thamani ili waweze kutoa haki ya msingi kwa mhitaji. Mathalani, fedha hutolewa ili watu waweze kupata kazi, kupendelewa au kupunguziwa majukumu ya kazi, kupandishwa cheo au kukwepa majukumu fulani. Katika taifa rushwa ni tatizo sugu kama moja ya kansa au donda ndugu lililo kwenye mifumo yetu ya maisha.

Kwa mfano, kadhia ya wazi ya rushwa iliyoikumba chama fulani cha siasa hapa nchini. Mnamo Julai 12, 2015, mkoani Dodoma mwananchi mmoja mwenye asili ya Asia aligunduliwa akiwa na shilingi za Kitanzania zaidi ya milioni 700. Baada ya uchunguzi wa polisi, iligundulika kuwa, fedha hizo zilikuwa ni shilingi za Kitanzania milioni (722,500,000)[10]. Kugundulika kwa raia huyo mwenye asili ya Asia aliyejulikana kwa jina la Amit Kevalramani katika hoteli ya *St. Gasper* iliyopo jijini Dodoma kulitokana na wananchi kuonesha hofu na mashaka juu ya mtu huyo.

[10] Kwa maelezo zaidi, tazama gazeti la *Mwanahalisi* la tarehe 12/07/ 2015.

Amit alidhaniwa kwamba anatoa hongo (rushwa) kwa wajumbe wa mkutano mkuu ambao walikuwapo kwa ajili ya uchaguzi wa viongozi wa chama hicho. Ndipo wasamaria wema wakafanya mkakati na kumkamata. Upo msemo usemao "Rushwa ni adui ya haki". Msemo huu una mawanda mapana sana, kwa sababu tumekuwa tukishuhudia mataifa mbalimbali ulimwenguni kote yakipiga kelele dhidi ya rushwa. Wanasiasa, viongozi wa serikali na wale wa dini pia hulikemea jambo hili la kutoa na kupokea rushwa. Hii yote ni ishara na dalili za wazi juu madhara na athari inayojitokeza kwa jamii na taifa juu ya adui huyo wa haki.

Wasanii na wanafasihi hawakuwa nyuma katika kupambana na adui huyu wa haki ambaye huingiza watu katika jinai. Hii ni kwa sababu mtoaji na mpokeaji wa rushwa wote huhesabika wametenda uhalifu katika jamii. Tukio hili la uhalifu limeelezwa katika riwaya ya *Kiu ya Haki* na mwandishi Zainab M. Mwanga kwa kuonesha ni jinsi gani polisi wala rushwa wanavyodhulumu haki za watu kwa kutofuata kanuni na sheria stahiki za nchi na maadili ya kazi zao. Anasema:

> "Njia fupi ni kumyamazisha yule aliyetutuma kwa kumpa chochote mzee, na mambo yatakwisha," alitamka yule Polisi wa kwanza kwa aibu kidogo. "Tena usiwe na wasiwasi. Akishapokea chochote basi, hatutathubutu kukufuatafuata tena," aliongeza Polisi wa pili. Mzee Fundisha aliingia chumbani, akachukua shilingi elfu 2000/= na kuwakabidhi hao Polisi. Nao bila kuuliza swali walizipokea na kuondoka huku maneno ya kumpoza Mzee Fundisha yakiwatoka… Kitendo cha Polisi kupokea shilingi elfu 2000/= kiliua imani ya Mzee Fundisha kwa Polisi. Alikuwa na uhakika kwamba ilikuwa ni baadhi tu ya Polisi waliojiingiza katika mambo kama haya (uk: 9).

Tukio hili linatuonesha jinsi rushwa ilivyokithiri na kuwa "adui wa haki". Kufuatana na msemo huu, mwandishi anatueleza kuwa, rushwa imekithiri sana hasa katika vyombo vya ulinzi. Jambo ambalo, vyombo hivyo vilivyotarajiwa kulinda na

kumdhibiti adui huyo vimekuwa mstari wa mbele kudai na kupoke rushwa, na hivyo, kusababisha kukosekana kwa haki. Kwa mfano, tunaelezwa kuwa, polisi wamekwenda hotelini kwa Mzee Fundisha kuchukua rushwa.

Ikumbukwe kuwa, hali iliyojitokeza katika nukuu hii inakwenda sambamba na uhalisi wa maisha katika jamii nyingi duniani kote, hususan nchi zinazoendelea kama Tanzania. Jambo hili la rushwa limezagaa sana hasa maeneo ya wafanyakazi wa taasisi za umma kama vile, Polisi, Mahakamani na ofisi mbalimbali za utumishi wa umma. Wanajamii walio na haki wanashindwa kupata haki zao kwa mujibu wa sheria na hulazimika kutoa rushwa, jambo ambalo ni kosa la jinai.

Tukio lingine la rushwa ambalo limeoneshwa katika riwaya hii ya *Kiu ya Haki* ambapo Inspekta Pwagu akiwa pamoja na Jaji Pwaguzi wanapanga njama za kujipatia fedha zisizo halali kutoka kwa Sikujua (uk: 45-50). Lengo ni kumsaidia ili wabatilishe haki kwa mwenye haki na kumtia hatiani asiyekuwa na kosa. Baada ya kukamilika mipango hiyo, Jaji Pwaguzi alimruhusu Inspekta Pwagu kwenda kwa Sikujua amuambie juu ya kesi hiyo na hatimaye amueleze kuwa, kama atatoa chochote wako tayari kumsaidia. Mwandishi anasema:

> "Sikiliza, Sikujua. Sisi habari zote tunazo kutoka hoteli ya Mtukunywa mpaka habari za hongo ya shilingi laki moja kwa Mzee Toboa. Mimi nimekuja hapa tuzungumze la maana, yaani kukusaidia…" "Nimekusikia bwana Inspekta. nasikitika sana nimesalitiwa… Nitashukuru zaidi kama nitapata msaada unaoniambia…" "Msaada utapata, lakini lazima utambue kuwa kesi hii ni kubwa, na kazi yake ni kubwa! Sitaifanya kazi hii mimi peke yangu. Jaji pia lazima nimshirikishe katika kukunasua kutoka kwenye kitanzi hiki kilicho katika shingo yako…" "Mm!" aliguna Sikujua. Alikuwa amekata tamaa kabisa ya kujinasua… "Ee Bwana mimi nipo," Inspekta Pwagu alimuhakikishia Sikujua. "Nitafanya juu chini uondokane na balaa hili na huyo aliyekusaliti ndiye apatikane…" "Hakuna mtu mwengine…

> Naomba msaada wako tafadhali." "Basi kama ni hivyo mambo yatanyooka tu usiwe na wasiwasi. Sasa unasemaje?" aliuliza Inspekta Pwagu. "Nakusikiliza wewe Bwana," alijibu Sikujua. "Unazo shilingi laki moja? Kesi hii si ndogo tena kumbuka tuko wawili," alisema Inspekta Pwagu na uso mkavu bila aibu… Baada ya muda mfupi mke wa sikujua alirejea na shilingi hamsini elfu, akamkabidhi mumewe, Sikujua, alimpa inspekta hizo pesa na kumuahidi kuwa fedha zilizo baki atampa siku ya pili akishazichukua toka benki (uk: 52-54).

Kupitia nukuu hii, kunaonekana waziwazi kuwa dhana ya kusaidiwa kwa mhalifu huyo inapingana na maana halisi ya msaada katika jamii. Mhalifu kisheria hapaswi kusaidiwa, bali anapaswa kuhukumiwa kulingana na kosa alilotenda. Msaada huo ulitaka kufanyika kwa lengo la kubatilisha haki baada ya kupokea rushwa kutoka kwa mhalifu. Pia, mtunzi alitaka kusisitiza kuwa wenye mamlaka na uwezo juu ya wengine hutumia mamlaka yao kwa lengo la kukandamiza haki huku wao wakinufaika kwa kutenda maovu hayo kwa jamii. Hivyo, utafiti uligundua kuwa, watu wa tabaka la juu katika maisha hutumia uwezo walionao kuzuia haki ya mtu fulani kwa lengo la kumkandamiza mtu huyo wa tabaka la chini (asiyekuwa na uwezo). Kwa mantiki hiyo basi, ni wazi kwamba dhuluma ambazo hufanywa kwa lengo la kujilinda ama kujinufaisha zimekithiri na kutawala katika jamii nyingi tunazoishi.

Vilevile, mwandishi anamtumia Inspekta Pwagu, mheshimiwa Jaji Pwaguzi na baadhi ya wananchi wenye nyadhifa serikalini wakiwa wanachukua rushwa kwa wananchi mbalimbali katika jamii. Viongozi hao walijua wazi kuwa, kitendo wakifanyacho ni kinyume na imani ya chama na miiko ya kazi yao, kwani ni kitendo cha kikatili na cha kihalifu. Hata hivyo, hawakusita kufanya hivyo waliendelea

kuchukua rushwa kwa lengo la kujiongezea kipato huku wakiwa na dhamira ya kutaka kubatilisha haki. Mwandishi anasema:

> Inspekta Pwaguzi aliwaza hayo huku bado ameshikilia mtoto wa meza. Alijua sana miiko ya kazi yake, imani ya chama na umuhimu wake pia alivitambua vema, lakini moyo wake ulishakufa ganzi juu ya suala la kula rushwa. Alijua ubaya wa kula rushwa lakini alishindwa kuacha tabia hiyo, kwani mwonja asali haonji mara moja; na asali sasa ilikuwa imemnogea. Aliona yafaa kuchonga mzinga! Dhamira yake ilikuwa haikutushwi tena na imani ya chama inayozuia kula rushwa (uk: 47).

Pia, tukio kama hili la utoaji na upokeaji wa rushwa limeoneshwa katika riwaya ya *Kiu ya Haki*, ambapo mhusika Sikujua anatoa rushwa ya shilingi laki moja kwa Mzee Toboa ili amtunzie siri ya mauaji ya rafiki yake Pondamali. Anasema:

> Uwe mtu wa msada mkubwa kwangu kama unavyoniahidi. Niko tayari kukupa chochote atakachonitajia ili mradi uitunze siri hii. Najua wewe na mambo ya uhalifu ni maji ya moto, na ndio maana nimeamua nikupe siri yote kwa kujihami (uk: 19-20).

Nukuu hii inatueleza kuwa wapo watu ambao hufanya uhalifu katika jamii zao, na hatimaye, kuhitaji msaada kwa kufichiwa siri yao hiyo ya uhalifu. Hapa tunamuona mhusika Pondamali akiwa tayari kutoa kiasi chochote cha fedha kwa Mzee Toboa ili aweze kumtunzia siri hiyo. Kutokana na kuchukizwa na matendo hayo maovu, Mzee Toboa anamlaghai Sikujua kuwa angeitunza siri akiwa na lengo la kupata ukweli wa tukio hilo na kuliripoti sehemu husika kwa ajili ya kuchukuliwa hatua za kisheria.

Kwa upande wa riwaya ya *Mhanga wa Ikulu*, tunaliona tukio la rushwa ambalo ni miongoni mwa matukio makubwa ya uhalifu katika jamii kupitia kwa mhusika Farouk ambaye ni mkurugenzi wa usalama wa taifa alipokubali kuvaa koti la Mheshimiwa Zumo. Huyu alikubali kwake kubeba jukumu la kununua picha kama yeye ndiye Mheshimiwa Zumo kutoka kwa Frank ambaye ni mwandishi wa habari

wa gazeti la CHAMBUA kwa lengo la kulinda chama chake. Kupitia picha hizo, Frank alidai kulipwa pesa nyingi sana zipatazo shilingi bilioni mbili kwa ajili ya kumuuzia picha hizo zilizoonesha ukatili na uhalifu wa mauaji kwa mke wa Zumo. Mwandishi anasema:

> "Dickson," Farouk alisema na kumwangalia Dickson. "Utaratibu umefanyika wa kuzipata pesa zinazotakiwa na Frank. Tumezikopa toka vyanzo vyetu vya pesa na ziko shilingi bilioni mbili kama ulivyodai ni kiwango anachokihitaji Frank," Farouk akauweka mkono wake juu ya begi lililokuwa juu ya meza. "Pesa ndizo hizi hapa na hizi pesa hazitapotea… ingawa hatujui ni masharti gani atakayoyatoa wakati wa makabidhiano ya hizi hela, lakini kwa vyovyote atakutegemea wewe katika mzunguko wote wa kukabidhiana pesa na cd."… "Nafahamu, wee zungumza!" Frank alisema kwa mkato. "Nimeonana na Mheshimiwa Zumo, ameziona picha kwenye mkanda niliompa. Amekwama! Amekubali kuinunua cd yako." "Kwa bei ileile?" Frank aliuliza na sauti ilionekana kutulia. "Ndiyo. Shilingi bilioni mbili." "Kwa hiyo hapo upo naye?" Swali hilo likamkwamisha Dickson. "Nani...? Mheshimiwa Zumo?" Dickson aliuliza na kuonekana kutaka kupoteza mhimili wa kujizuia kutotaharuki. "Mwambie yupo! Mwambie yupo!" Farouk alinong'ona huku mikono yake ikimhimiza Dickson ajibu hivyo haraka. "Ndiyo nipo naye," Dickson alijibu na kumuangalia Farouk kama angekuwa na lingine la kuongeze… (uk 56: 58).

Katika nukuu hii tunaweza kuona kuwa mwandishi ameonesha rushwa ambayo si ya moja kwa moja, yaani haikuwa wazi sana ila ni moja kati ya rushwa mbaya katika jamii. Farouk, ambaye ni Mkurugenzi wa Usalama wa Taifa, kupitia mpango wa Frank, amejifananisha na kubeba jukumu la Mheshimiwa Zumo. Anaonekana kukubali kununua picha hizo na kulipa kiasi hicho cha pesa kipatacho bilioni mbili kilichodaiwa na Frank kwa lengo la kukinusuru chama chake na kumlinda mgombea huyo wa urais. Kwa sababu picha hizo zikifika kwa wapinzani kuna uwezekano

mkubwa wa kuangushwa kwa chama tawala na kupoteza nafasi adhimu ya kuongoza nchi.

Kwa jumla, utafiti uligundua matukio tofauti ya kihalifu ambayo husababisha kufanyika kwa uforensiki. Matukio hayo ni kama vile; tukio la mauaji, tukio la wizi, tukio la ujambazi, tukio la utekaji nyara na tukio la kutoa na kupokea rushwa kama yalivyochambuliwa hapo juu. Matukio haya hufanywa na baadhi ya wanajamii na viongozi wa vyama na serikali. Aidha, utafiti umebaini kuwa matukio haya hutokea kutokana na sababu mbalimbali. Miongoni mwazo ni hasira zilizotokana na mapenzi, tamaa ya kupata fedha (mali) au cheo, kutokuwa na hofu ya Mungu, umasikini, imani potofu za kishirikina pamoja na kulinda hadhi ya chama na viongozi wake. Matukio haya ya kihalifu huweza kufanywa kwa siri au kwa dhahiri. Tukirejelea Nadharia ya Uhalisia tunaweza kuona kwamba lengo kuu la nadharia hiyo ni kuweza kuwafungua watu macho na kuweza kutoa uchafu uliomo katika jamii. Uhalisia huhitaji msanii kutupilia mbali mambo ya kubuni, na badala yake, kuwaza (Simiyu: 2015: 204). Utafiti ulibaini uhalisi wa maisha ulivyo juu ya matukio hayo ya kihalifu. Hii ni kwa sababu ni mambo ambayo yanawakuta wanajamii kila siku katika harakati zao za maisha ya kila siku. Matukio haya ya kihalifu huiathiri jamii pindi yanapojitokeza katika maeneo yao. Pia, huweza kusababisha upotevu wa mali, amani, imani na upendo na hata kusababisha maafa kwa mtu au jamii kwa jumla.

### 4.5 Miktadha Ambayo Taaluma ya Uforensiki Inafanyika

Wamitila (2013) anafafanua kuwa, muktadha ni dhana inayotumika katika kuzihakiki kazi za fasihi ili kueleza hali ya kujaribu kuliweka tukio au matukio ya

kazi za fasihi katika muktadha wa kijamii, kihistoria, kijiografia, kisiasa na kiuchumi. Kila kazi ya fasihi hufungamana na muktadha ulioizaa. Uforensiki, kama kipengele kimojawapo muhimu cha fani katika uandishi wa kazi za fahisi, hutawaliwa zaidi na miktadha ya kiutendaji ambayo huambatana na matukio mbalimbali yanayotokea katika jamii. Matukio katika riwaya pendwa ambayo hubuniwa na wanafasihi hufungamana na miktadha katika utendaji na utendekaji wake. TUKI (2004) inaeleza maana ya neno muktadha kuwa ni mazingira au hali ambamo tukio hutendeka. Hivyo, fasihi yoyote ile hufungamana na muktadha maalumu. Akifafanua juu ya muktadha, Songoyi (1997) anasema kuwa:

> *The word context refers to the situation within which performance take place. Context includes the time and the place at which the performance takes place. It also includes the physical, psychic and emotional condition of the performer and the skills he or she has. The form of art being performed, it's subject matter and the occasion during and which the performance is done, the audience, it's nature and composition are also aspects of context.*
>
> Neno muktadha linarejelea hali ambayo utendaji umefanyika. Muktadha unahusisha muda na mahali tukio linapofanyika. Pia, inahusisha mwonekano, hisia na hali ya matendo ya mtendaji na ujuzi alionao. Muundo wa sanaa inayotendwa, mada husika na tukio wakati ambapo utendaji umefanywa, hadhira, ni asili na mchanganyiko pia ni mambo ya muktadha. (tafsiri yetu).

Kwa mantiki hiyo, tunaweza kuona kwamba, muktadha wowote ule wa kazi ya sanaa ni lazima uhusishe mazingiza halisi ya jambo linalofanyika, muda wa kufanyika kwake na mahali jambo au tukio hilo linapofanyika. Aidha, yapo mambo yahusikayo katika muktadha kama vile muonekano wa jambo, hali ya mtendaji na kipaji alichonacho. Anaongeza kusema kuwa, muktadha pia unahusisha muundo wa sanaa inayotendwa, dhamira na hali ya uwasilishaji wake, hadhira, upokeaji wake na

mazingira husika. Kwa jumla, vipengele vyote hivi kwa umoja wake vinafanya muktadha wa kifasihi kukamilika.

Katika jamii zetu tunaweza kuona miktadha mbalimbali ambayo taaluma ya uforensiki hufanyika, kutegemeana na tukio la kihalifu lililotendeka. Ipo miktadha ya kisheria (kimahakama), utabibu, kisaikolojia, kipolisi, lugha, kisanaa na kijamii. Maeneo yote haya ambayo hupatikana katika jamii huweza kutumika na kusaidia kufanikisha uchunguzi (uforensiki) pindi panapotokea tukio la uhalifu ambalo linahitaji kufanyiwa uchunguzi huo.

Wanafasihi, katika kuimarisha sanaa zao kwa lengo la kuelimisha jamii juu ya matukio ya kihalifu ambayo hujitokeza katika jamii zao, hujaribu kutumia miktadha mbalimbali kuonesha matukio hayo, na jinsi ambavyo hatua za kiusalama na kiupelelezi zinavyochukuliwa kwa lengo la kukamata wahalifu husika. Hivyo basi, mtafiti alichambua miktadha hiyo kama iliyotumika katika riwaya teule kwa kuangalia misingi ya uhalisia na taaluma husika ya kiforensiki (upelelezi).

Katika kazi za fasihi, ipo miktadha tofauti ambayo imetumika kuonesha taaluma ya uforensiki ilivyotendeka. Miktadha hiyo, ambayo ndani yake taaluma ya uforensiki hutendeka, huambatana na nyenzo kadhaa zinazotumika kama msaada ama ushahidi kutokana na matukio ya kihalifu yaliyotokea katika jamii. Hivyo, husaidia kutambuliwa na kukamatwa kwa wahalifu katika jamii hizo. Miongoni mwa mambo hayo ni kama vile, matumizi ya vionjo vya lugha (sauti, namna ya uzungumzaji, na namna ya uandishi), matumizi ya michoro ya picha ili kutambua mhalifu, matumizi ya nyenzo za kielekitroniki kama vile (simu, ipad, saa, kamera na kompyuta), stadi

za kuchunguza lugha-uso, jinsi ya kutambua ishara mbalimbali katika mwili wa maiti au mtu aliyetendewa uhalifu huo.

### 4.5.1 Muktadha wa Kipolisi

Polisi ni neno lililotokana na lugha ya Kiingereza *Police* (*Protection of life and Investigation of criminal Events*). Polisi ni moja wapo ya vyombo vyenye mamlaka ya kuzuia makosa na kufanya upelelezi wa makosa ya jinai. Hiki ni chombo chenye majukumu mengi. Mojawapo ya majukumu makubwa ya jeshi la polisi ni kuhakikisha usalama na ulinzi wa raia na mali zao, kusimamia utekelezwaji wa sheria, kuzuia na kudhibiti uhalifu, kuwakamata watuhumiwa na kudumisha amani na usalama katika nchi.

Upelelezi unaweza kufanywa kwa lengo la kumtambua na kumkamata mhalifu pindi kunapotokea tukio la uhalifu katika jamii. Kumkamata mtu ni moja kati ya mambo yenye athari za moja kwa moja za kuingilia uhuru wa mtu kwenda anakotaka ambao unalindwa na katiba ya nchi. Hata hivyo, kwa mujibu wa katiba hiyo, mtu anaweza kuingiliwa katika uhuru wake huo kwa mujibu wa sheria. Polisi hulazimika kumkamata mtu katika shughuli zao za upelelezi pale ambapo imethibitika (wamejiridhisha) kuwa mtuhumiwa amehusika juu ya matukio hayo ya uhalifu yaliyotokea katika jamii[11]. Katika muktadha huu, Polisi huweza kufanya kazi hiyo ya upelelezi baada ya kupata taarifa ya kutokea kwa tukio la uhalifu kutoka kwa raia wema, na hivyo, hulazimika kufika katika eneo la tukio (*crime scene*) kwa ajili ya kutekeleza moja ya majukumu yao ya kupambana na uhalifu katika jamii.

[11] Maelezo haya yametolewa na mmoja wa maafisa wa upelezi ambaye hakutaka kutajwa jina lake wakati akifanya mahojiano na mtafiti siku ya tarehe 11/03 /2018 kisiwani Pemba.

Katika riwaya ya *Kiu ya Haki*, mwandishi Zainab M. Mwanga ameonesha muktadha huu kwa kumtumia mhusika Inspekta Paukwa ambaye alikuwa Ofisa wa Polisi mwenye cheo cha Mratibu Mwandamizi. Ofisa huyo ndiye aliyekuwa akipeleleza kesi ya mauaji ya Pondamali baada ya kupata taarifa za kutosha kutoka kwa raia mwema. Inspekta Paukwa alianza kazi hiyo ya upelelezi kwa kuwaita vijana wake wawili na kuwaamuru kwenda hoteli ya Mtukunywa kwa ajili ya kupeleleza majina ya watu watatu ambao waliingia hotelini hapo kati ya saa nane na saa tisa usiku siku ya Ijumaa. Mwandishi anasema:

> Maafisa upelelezi hao wawili waliondoka hadi hoteli ya Mtukunywa na kuonana na mpokea wageni. Baada ya mahojiano, walihakikishiwa na mpokea wageni huyo kwamba ni kweli kulikuwa na watu watatu waliowahi kufika hotelini … mpokea wageni, aliwapa vijana hao majina ya watu hao watatu… Wale maofisa upelelezi wawili waliendelea na kazi yao. Walitembelea kila hoteli iliyo maarufu jijini kuwasaka watu hao …ndipo walipoamua kwenda hoteli ya Mtoni… Mpokea wageni wa hoteli hiyo aliwaambia kwamba waliingia wageni watatu siku ya ijumaa usiku saa tisa na nusu hivi… Maofisa upelelezi hao baada ya kupata maelezo hayo wakawa na shaka na wapangaji hawa… walikiendea chumba namba 24. Ndicho walichoelekezwa kuingia. Kabla ya kupiga hodi walikuwa wamechukua muda mfupi kusikiliza mlangoni. Iliwabidi wawe na hadhari kwa vile watu hao kama kweli walikuwa ni majambazi…walipoingia watu hao … Maafisa upelelezi walitiwa moyo na kuendelea na upekuzi wao… Waliwazoazoa hadi kituo cha Polisi kilichoko karibu na stesheni ya gari moshi (uk: 41-43).

Katika dondoo hili, tumeweza kuona namna polisi wanavyotimiza baadhi ya majukumu yao ya kupambana na wahalifu. Nukuu inatuonesha kuwa upelelezi huanza mara tu baada ya taarifa za uhalifu kufika kwa vyombo vinavyohusika. Tunamuona Inspekta Paukwa akiwataka vijana wake wawili ambao wapo katika kitengo hicho cha polisi cha upelelezi kufanya uchunguzi. Vijana hao waliweza kufuata hatua muhimu za kiupelelezi kama vile kufika katika hoteli waliyoagizwa.

Hata hivyo, baada ya kushindwa kuwaona watu hao katika hoteli hiyo, walifuatilia katika hoteli nyingine mbalimbali zilizopatika mjini hapo huku wakiwa na vielelezo muhimu kama majina yao na kazi walizokuwa wanafanya kama walivyojieleza hapo awali katika hoteli ya Mtukunywa. Kwa umahiri na jitihada kubwa, polisi waliweza kuwapata wahalifu hao, ingawa walibadili majina na kazi zao kwa jinsi walivyojimbulisha hapo awali.

Aidha, miktadha hii ya kipolisi katika taaluma ya uforensiki (uchunguzi) tunaweza kuiona pale polisi wakiwa katika harakati mbalimbali za kutafuta ushahidi juu ya mtu aliyemuua Pondamali. Tumeona kuwa, waliwahoji watu kadhaa na wengine kuwakamata kwa lengo la kupata ushaidi utakaowezesha kumpata mhalifu husika. Jambo hili linathibitishwa na mhusika Sikujua pale aliposema; “Polisi wananiandama kila kukicha kunihoji eti niwaeleze aliyokuwa nayo marehemu na maadui zake walikuwa akina nani” (uk: 15). Pia, miktadha hii imeoneshwa pale polisi walipomkamata Mzee Toboa. Mwandishi anasema:

> Mzee Toboa alizolewa tarehe 29 Julai saa tisa alasiri, kwenye kituo chake cha kuegeshamagari. Alikwishapata habari za kukamatwa kwa Sikujua. Lakini alipowaona polisi watatu wenye sare na mtu mwengine asiye sare wanamsogelea alipatwa na wasiwasi… habari zako Mzee? Ofisa upelelezi ambaye hakuvaa alimsalimu. Nzuri bwana nzuri alijibu Mzee Toboa kwa shaka. Tunakuhitaji Mzee, alisema Inspekta Pwagu… Kwa shughuli gani aliuliza mzee toboa alikuwa amesimama nje ya gari lake. Hakujibiwa bali alifungwa pingu mikononi na Polisi wa pili. Mzee Toboa alianza kuona ugumu wa mambo (uk: 69).

Matendo na matukio haya ambayo hufanywa na polisi ni moja kati ya mambo ambayo husaidia kutafuta ushahidi juu ya uhalifu uliotokea katika jamii. Mwandishi anatuonesha kuwa, panapotokea tukio la uhalifu, polisi huanza upelelezi wao kwa kuwakamata na kuwahoji watu walio karibu na mwathirika wa tukio hilo, ama

waliokuwepo katika eneo la tukio hata kama hawakuhusika na uhalifu huo. Hufanya hivyo kwa lengo la kupata taarifa za awali juu ya tukio hilo. Hujaribu kuchunguza lugha mwili wakati wa mahojiano yao na watuhumiwa wa matukio hayo ya uhalifu kama hatua moja muhimu na ya msingi katika uchunguzi.

Kadhalika, muktadha huo wa polisi tumeweza kuuona katika riwaya ya *Mhanga wa Ikulu* kwa kuangalia harakati zinazofanywa na polisi ili kumkamata mtu aliyeshukiwa kuwa gaidi, ambaye alitaka kufanya tukio kubwa la kigaidi katika maeneo yenye mkusanyiko mkubwa wa watu (uk: 169). Mipango na mikakati madhubuti ya kiusalama iliandaliwa katika ngazi zote za idara ya usalama na ulinzi kwa kuanza kuwakamata na kuwahoji watu wake wa karibu. Hali hii imeoneshwa pale mwandishi aliposema:

> “Basil nataka unieleze ilikuwaje mkakamatwa?” Frank alieleza baada ya mhudumu kuondoka. “Tulikamatwa jana jioni tukiwa tunajiaanda kutoka kazini,” Basil alianza kuelezea… “Tulikamatwa mimi, Haji na Sele. Kisha tukaanza kuzunguka kuwatafuta Ben na Zagalo kwa kuwafuata nyumbani kwao… (uk: 226).

Harakati hizi za kuwakamata wafanyakazi wenzake Frank, ambazo zimeoneshwa na mwandishi katika nukuu hii zinadhihirisha hatua za awali za upelelezi. Hii ni kwa sababu polisi hao waliamini kuwa huenda wafanya kazi hao kwa kiasi fulani watasaidia kutoa taarifa za mhusika ambaye anatafutwa au kutoa taarifa juu ya picha alizokuwanazo Frank.

Mipango mingine ya kiupelelezi iliyoratibiwa ni ile ya kutumia vifaa vya kielektroniki kama vile simu. Polisi walifanya udukuzi wa mawasiliano ili kusaidia upelelezi wao na kurahisisha upatikaji wa mtuhumiwa. Mwandishi anathibitisha hili kwa kusema; “kama kawaida, zoezi hilo likapangwa kufanyika kwenye chumba

maalumu cha udukuzi wa mawasiliano ya simu. Zulfa akampigia simu Frank!... (uk: 244). Hali hii ya udukuzi iliendelea hadi pale alipopatikana mhalifu husika, mwandishi anaendelea kuelezea hali hiyo kwa kusema:

> "Lakini usiogope kunieleza yaliyotokea huko. Haya hebu niambie laptop ya Dickson ilikuwa na nini?" "Frank, naogopa kukwambia kwenye simu! Sijui alikuwa anakuchunguza huyu baba…maana hata sielewi!" "Nidokeze basi!" "Kama ingewezekana ningekwambia njoo tuzungumzie nyumbani,… "Lakini nafasi ya kutoka unayo?"… Baada ya maongezi hayo, angemkodisha Zulfa teksi ya kumrudisha na kisha yeye angeenda hadi kituo cha Tegeta ambako… ilikuwa rahisi kuliko walivyokusudia! Farouk alipumua kwa faraja wakati akiviondoa vifaa vya kusikilizia kutoka kwenye masikio yake. "*Very good!*" Alimwambia Zulfa. Kisha aliwageukia wenzake. "Safari hii nitahakikisha zoezi la kumkamata Frank nalisimamia mwenyewe ili kusitokee makosa kama yaliyotokea." "Sidhani kama safari hii ataupata mwanya mwingine wa kututoroka!" Cobra alisema (uk: 252-253).

Mwandishi, kupitia nukuu hii, amekusudia kuieleza jamii kuwa, moja ya mbinu muhimu za kiupelelezi ambazo zinaweza kutumika na kurahisisha kazi ya upelelezi ni udukuzi wa mawasiliano kupitia vifaa vya kielektroniki kama vile simu. Vifaa hivi huweza kurahisisha upelelezi kwa kiasi kikubwa, kwani huweza kuunganishwa kwa wawasilianaji zaidi ya mmoja wakiwa katika maeneo tofauti ya kijiografia. Hivyo, mwandishi anaonesha jinsi ilivyokuwa rahisi kukamatwa kwa Frank baada ya kutumia mbinu za udukuzi wa mawasiliano.

Kadhalika, muktadha wa kipolisi umedhihirika katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* ambapo mwandishi amemtumia mhusika Spekta Seif wakati alipokuwa akipeleleza mauaji ya Bwana Ali. Tumeelezwa kuwa, Spekta Seif alianza upelelezi wake kwa kumuuliza maswali Mmanga kwani tukio hilo la mauaji lilitokea karibu na mazingira ya nyumbani kwake, anasema:

> Spekta Seif alimtazama usoni, kisha akamuuliza tena, “Mgeni wako yuko wapi?” Mmanga akajibu, “Sigyui mimi wakti naondoka; sinaona yeye wakti matoka,… Spekta Seif alimtazama usoni bila ya kupepesa, kisha akaendelea na masuala yake, “Mgeni huyo anatokea Maskati siyo?” Alijibiwa, “Anha, natoka Maskat; asli yake Konga yeye, lakini baaden nasafir Maskat, ndio sasa nakugya Swahili” (uk: 55).

Mahojiano ambayo yamefanywa kati ya Mmanga na Spekta Seif ni moja kati ya harakati za awali za upelelezi wa matukio ya kihalifu, kwani maafisa wa upelelezi hufika katika eneo la tukio mara baada ya kuripotiwa tukio hilo la uhalifu. Moja ya mbinu za kiupelelezi ni kuangalia lugha mwili wakati wa mahojiano. Katika nukuu hii tumemuona Spekta Seif akimtazama Mmanga usoni kwa umakini sana wakati anapomuhoji Mmanga huyo na kuanza kujibu maswali hayo. Azma ya kumuangalia kwa umakini ni kutaka kujiridhisha na kujua ukweli uliomo katika nafsi yake juu ya mgeni wake na tukio hilo la mauaji. Hii ni kwa sababu Mmanga huyo ndiye ambaye alidhaniwa kuiba upanga na kumuua Bwana Ali.

Kadhalika, hali kama hiyo ya kiforensiki ambayo husaidia kugunduliwa kwa wahalifu katika jamii na mataifa mbalimbali ambayo hufanywa na polisi tuliithibitisha pale mwandishi anapomuonesha Spekta Seif na mfanyakazi mwenzake Chombeka wakati wakiwa katika eneo la tukio. Anasema:

> Sasa walifika kunako kichwa, na kunguru wamekizonga, wamo kukinyofoa tu, lakini wote waliruka kwa umoja walipoona watu wanakuja. Spekta Seif aliinama kukitazama. Chini yake palikuwa na mabonge ya damu iliyoganda; mengi katika hayo yamekwisha chukuliwa na kunguru. Spekta Seif aliinuka tena, “Chombeka! Chukua kichwa hiki”… “Unapima nini, Bwana Msa? Ee Bwana Msa, huachi? Hiyo si kazi yako; hutuachii wenyewe, bwana?”... (uk: 59).

Kama ilivyobainishwa katika nukuu hii, mwandishi amekusudia kuonesha uhalisi wa maisha katika kazi za uchunguzi na upelelezi wa polisi juu ya jukumu lao la kupambana na uhalifu. Msanii ametubainishia hili kuanzia katika hatua muhimu ya uchunguzi katika uhalifu ambayo ni kuwasili katika eneo la tukio na kuanza kujionea wenyewe hali halisi ilivyo. Hii ni kwa sababu katika eneo la tukio huweza kupata mambo mengi ambayo hutumika kama ushahidi. Mfano wa mambo hayo ni damu, silaha iliyotumika, mwili wa marehemu na mengineyo. Mwandishi anaonesha uwajibikaji mkubwa wa serikali katika kupambana na uhalifu kupitia Spekta Seif na Chombeka kufika katika eneo la tukio kwa ajili ya uchunguzi. Walianza kuona damu katika eneo hilo, na hatimaye, kuona kichwa kilichotenganishwa na mwili wake. Spekta Seif, alikiangalia kwa makini, hatimaye, akamuamuru Chombeka kuondoka na kichwa hicho kwa ajili ya uchunguzi zaidi.

### 4.5.2 Muktadha wa Mahakamani

Mahakama ni mfumo wa wataalamu na kamati maalumu ambao unatafsiri na kutumia sheria. TUKI (2004: 215) ikitafsiri neno mahakama inasema kuwa, “Ni mahali ambapo kesi na mashtaka mbalimbali husikilizwa na kuamuliwa”. Mahakama ni mfumo wa kutatua migogoro chini ya mgawanyo wa madaraka. Kwa kawaida, mahakama huwa haitungi wala kuunda sheria bali inatafsiri, kutumia na kutekeleza sheria katika ukweli wa kila kesi, pia ina kazi ya kuhakikisha usawa mbele ya sheria kwa watu wote. Katika hali halisi, sheria haziwezi kutaja kila kitu kinachoweza kutokea, hivyo ni mahakama pekee zinazoamua kwa njia ya kulinganisha kesi, sheria na maazimio yaliyotangulia.

Katika kazi za kifasihi, muktadha huu wa mahakamani unatumika katika kukamilisha upelelezi juu ya makosa ya jinai. Wanasheria au mahakimu wa mahakama hizo huweza kukusanya ushahidi juu ya kesi za jinai na kuufanyia uchunguzi wa kina; hatimaye kutoa maamuzi stahiki kisheria.

Katika riwaya *ya Kiu ya Haki* mwandishi amethibitisha hili juu ya kesi ya mauaji ya Pondamali iliyowahusisha Killa, Somba, Kazamoyo, Sikujua pamoja na Mzee Toboa. Lengo ni kujua ni nani hasa aliyehusika na tukio hilo la uhalifu. Mahakama inatoa hukumu baada ya kuridhika na uchunguzi wa ushahidi uliokusanywa na waendesha mashtaka hao ambao ni wanasheria. Anasema:

> Baada ya kusikiliza maelezo yote kutoka kwa washtakiwa watatu, maelezo kutoka kwa Sikujua na kutoka kwa Mzee Toboa na ushahidi wake, mahakama hii imeridhika kwamba washtakiwa watatu hawana hatia ya kuua. Lakini washtakiwa watatu hawa wana hatia ya kuteka nyara teksi mbili kwa nia ya kujipatia pesa. Kitendo hicho kinahesabiwa kuwa ni ujambazi. … "Mahakama inamuachia huru Mzee Toboa baada ya kuridhika na ushahidi wake. Hakuna ushahidi uliotolewa wa kuifanya mahakama hii iamini kuwa Pondamali kauawa na Mzee Toboa…" "Somba, Killa na Kazamoyo, wanahukumiwa kifungo cha miaka mitano na kazi ngumu kila mmoja kwa kosa la ujambazi…" "Sikujua amepatikana na hatia ya kuua kwa makusudi. Mahakama hii haina adhabu nyengine ya kumpa bwana Sikujua, bali, adhabu ya kunyongwa mpaka afe!" "Washtakiwa wote wana haki ya kukata rufaa," Mheshimiwa Jaji Utakunywa alifunga jalada la hukumu na kuondoka (uk: 88-90).

Kwa jumla, dondoo hii imeonesha kuwa, maamuzi ya kesi za makosa ya kihalifu/jinai hufanywa (huamuliwa) kitaalamu zaidi baada ya kukamilika kwa ushahidi uliokusanywa kutoka kwa waendesha mashtaka. Ushahidi huo ndio ambao hufanyiwa uchunguzi hatua kwa hatua hadi pale mahakama itakapojiridhisha na ushahidi huo. Jaji huanza kwa kuangalia historia za washtakiwa juu ya tukio hilo

kwa kuchunguza maelezo ya awali yaliyoripotiwa na watuhumiwa hao baada ya kukamatwa na kuhojiwa, ushahidi uliokusanywa, hatimaye, hutoa maamuzi kama ambavyo tumeona kupitia Jaji Utakunywa katika kesi ya mauaji ya Pondamali.

### 4.5.3 Muktadha wa Kitabibu

Huu ni muktadha ambao hushirikisha madaktari (matabibu) mbalimbali kwa lengo la kuchunguza maafa na madhara yaliyotokea juu ya mtu ama kiumbe chochote kilichofanyiwa uhalifu. Utafiti umegundua kuwa muktadha wa kitabibu katika taaluma ya uforensiki ni muhimu na ina mchango mkubwa sana katika kutoa ushahidi juu ya matukio ya kihalifu ambayo hutokea katika jamii zetu. Hii ni kwa sababu matabibu (madaktari) hao hutumia zana na vifaa tofauti vya kisayansi ambavyo husaidia kuthibitisha na kujua madhara, chanzo na sababu ya uhalifu huo. Mara nyingi, vifaa hivyo vinavyotumika hutegemeana na tukio lenyewe la kihalifu lililotendeka. Kwa mfano, uhalifu wa kijinsia/ makosa ya kijinsia (*sexual offence*) kama vile; kubaka, mauaji yaliyotokana na ubakaji, na mengine mengi.

Matukio kama haya, hufanyiwa uchunguzi kutokana na "*seminal stains"* madoa ambayo hupatikana katika mwili na nguo za muathiriwa au mkosaji, eneo lilipofanyika tukio hilo pamoja na vitu vilivyotumika katika kujisafishia wakati wa tukio ama baada ya tukio.  Mfano wa madoa yanayoweza kupatikana na kutumika katika uchunguzi ni kama vile, damu, nywele, na alama za vidole. Uchunguzi huu ni muhimu katika kuthibitisha juu ya tukio la kihalifu lililotendeka katika jamii, kwani husaidia kujua ni nani aliyetenda na wakati gani tukio hilo limetendeka. Naye, Makata (2011: 115), akieleza juu ya uchunguzi wa kitabibu katika makosa ya jinai, anasema:

> *Medical evidence may be used in both civil and criminal trials. Evidence given by doctor or health care workers my play a crucial role in assisting the court in diciding whether a person should be liable or not in civil cases and whether accused person should be found guilty or not guilty. In criminal cases medical practioners or health care workers my find themselves giving evidence etc.*
>
> Ushahidi wa kitabibu unaweza kutumika katika mashauri ya kiraia na jinai. Ushaidi uliotolewa na daktari au wafanyakazi wa huduma za afya unakuwa na kazi muhimu katika kusaidia mahakama kwa kuamua kama mtu anapaswa kuhukumiwa au la katika kesi za kiraia na kama mtuhumiwa anapaswa kupatikana na hatia au hana hatia katika kesi za uhalifu. Madaktari wa afya au wafanyakazi wa huduma za afya wanaweza kujikuta wenyewe wanatoa ushahidi (tafsiri yetu).

Wanafasihi nao hawapo nyuma katika kujadili suala hili kwenye kazi zao ambamo wanaakisi ushahidi ambao hutolewa na matabibu katika kufanikisha shughuli za kiupelelezi kwenye matukio ya kihalifu yanayotokea katika jamii. Mwandishi Zainab M. Mwanga katika riwaya yake ya *Kiu ya Haki* amelionesha hili kupitia tukio la mauaji ya Pondamali. Anasema:

> Maiti yake ilikutwa inaning’inia kwenye mti, katika kichaka kandokando ya barabara ya Bwagamoyo. Alama za vidole katika mwili wa marehemu huyu zilichunguzwa na kudhihirika kuwa ni zake mwenyewe marehemu. Kamba aliyotumia kujinyonga ni mkanda wa suruali yake… Mzee aliona yote, masikio yalisikia kwa umakini na akili yake ilitafakari yote aliyoyaona na kutafakari. Taarifa ya daktari ilieleza kuwa marehemu alikufa saa nane na robo usiku kwa kujinyonga au kunyongwa. Polisi walikuwa katika harakati za kupeleleza… (uk: 3-4).

Nukuu hii inaonesha jinsi maiti ya Pondamali ilivyokutwa katika kichaka ikining’inia kwenye mti. Pia, nukuu inatufahamisha kuwa, baada ya uchunguzi wa alama za vidole zilizogundulika katika mwili wake ni za marehemu mwenyewe pamoja na mkanda uliotumika ni wa suruali yake. Aidha, taarifa ya daktari iliyotolewa baada ya uchunguzi wa tukio hilo la mauaji ya Pondamali inathibitisha

kuwa, marehemu alijinyonga ama kanyongwa kwa kutumia mkanda wa suruali yake. Pia, ilibainika marehemu ameuawa saa nane na robo usiku wa Ijumaa. Hivyo, mwandishi ameonesha kuwa taarifa hiyo ya daktari iliweza kutolewa baada ya kufanyika uchunguzi wa kina kwa kutumia vipimo na vifaa vya kisayansi ambavyo viliweza kuthibitisha muda aliouawa marehemu na namna alivyouawa.

### 4.5.4 Muktadha wa Kijamii

Jamii ni mkusanyiko wa watu wanaoishi kwa pamoja katika eneo moja la kijiografia wakiunganishwa na historia yao na wakitambuliwa kwa utamaduni wao, lugha yao mila na desturi. Ili mkusanyiko fulani uweze kuitwa jamii ni lazima pawepo na watu wa jinsia na rika zote, wanaoishi pamoja katika kijiji ama mji fulani wenye eneo na mipaka maalumu. Katika kuchambua data, mtafiti alibaini kujitokeza kwa muktadha huu wa kijamii ambao pia ulionesha ufanisi katika uforensiki. Kadhalika, utafiti umebaini kuwa, wapo baadhi ya wanajamii ambao wanafahamu juu ya umuhimu wa taaluma ya uforensiki katika kutatua matatizo na migogoro mbalimbali katika jamii na kuendeleza harakati za kimaendeleo kwa kupingana na uhalifu. Wanajamii hao huamua moja kwa moja kupambana kwa nguvu zao zote kwa lengo la kuondoa kadhia hiyo ya uhalifu katika jamii zao. Hili hutokea kwa ama kufanya uchunguzi wao wenyewe au kutoa ushirikiano mzuri kwa vyombo na taasisi zinazohusika na uchunguzi huo wa matukio ya kihalifu na makosa mengine ya jinai katika jamii.

Kwa kuanza na riwaya ya *Kiu ya Haki*, utafiti umebaini kuwa, suala la uforensiki katika jamii ni muhimu sana kufanyika kwa wanajamii wenyewe pindi panapotokea uhalifu. Hii ni kwa sababu husaidia vyombo vinavyohusika na upelelezi huo kukusanya ushahidi utakaowezesha kupatikana mhalifu husika kwa urahisi.

Umuhimu huo umeoneshwa na mwandishi pale alipomtumia mhusika Mzee Toboa wakati akifanya upelelezi juu ya mauaji ya Pondamali. Baada ya kukamilisha upelelezi huo aliwasilisha taarifa hiyo kwa Inspekta wa Polisi kwa ajili ya kutendewa kazi zaidi. Mwandishi anathibitisha jambo hili kwa kuonesha hatua mbalimbali alizozichukua Mzee Toboa katika upelelezi wake. Anasema:

> Viungo vya fahamu katika mwili wa Mzee Toboa vilishiriki kwa ukamilifu katika msiba na mazishi ya marehemu Pondamali Malipesa, mzee aliona yote, masikio yalisikiliza kwa makini na akili yake ilitafakari yote aliyoyaona na kusikia… Mzee Toboa aliendelea na uchunguzi wake… "Hivi na wewe unasema kajiua?" Fundisha aliuliza… "Kumbe, basi nani kamnyonga?"… "Unaseama kweli, eh?" Alidakia Mzee Toboa, huku moyo ukimdunda kwa hamu ya kutaka kujua ukweli…(uk 4-6).

Hatua hizo za upelelezi kwa Mzee Toboa ziliendelea hadi pale alipokamilisha ushahidi alioukusudia, ndio alipochukua hatua ya kupeleka taarifa hiyo polisi. Msanii anaeleza ilivyokuwa kwa kusema, "Sikujua alitambua kuwa sasa amejipalia mkaa. Badala ya kumpeleleza mzee, sasa anapelelezwa yeye" … (uk: 18). Aidha, mwandishi anaendelea kusema:

> Baada ya kusalimiana, Mzee Toboa hakupenda kupoteza muda, hivyo alimweleza Paukwa kilichompeleka ofisini mwake asubuhi ile. Alimtobolea kisa chote cha kifo cha Pondamali kama alivyoelezwa na Sikujua. Inspekta Paukwa alimsikiliza kwa makini. Baada ya maelezo hayo, Mzee Toboa alimsihi na kumsisitiza... Alimuomba Inspekta huyo atumie maelezo aliyompa kumtia hatiani mhalifu bila kumuhusisha yeye ili kuepuka uadui… (uk: 39-40).

Katika jitihada hizo za kutafuta ukweli dhidi ya mauaji ya Pondamali, Mzee Toboa aliweza kufuatilia kwa kila aliposikia taarifa iliyohusu tukio hilo na hatimaye alipata ukweli wote kutoka kwa mhusika mwenyewe wa mauaji. Mwandishi kupitia nukuu hizo anatuonesha umahiri wa Mzee Toboa katika kutenda kazi ya kupambana na uhalifu katika jamii kama raia mwema ambaye anachukizwa na matukio ya uhalifu

katika jamii hiyo. Pia, nukuu inaonesha kuwa, Mzee Toboa aliweza kuzifikisha taarifa za uchunguzi wake katika sehemu husika kwa ajili ya kufanyiwa kazi zaidi na hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa dhidi ya mhusika wa tukio hilo la kihalifu.

Kadhalika, uforensiki katika muktadha wa kijamii unadhihirika kupitia riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* ambapo baadhi ya wanajamii wanachukua hatua mbalimbali za kiupelelezi kwa lengo la kutaka kujua chanzo cha mauaji ya Bwana Ali na kujua nani aliyehusika na mauaji hayo. Msanii amemtumia Bwana Msa kama mwanajamii ambaye anafanya uchunguzi kisanyansi (kitaalamu), na hatimaye, anafanikiwa kujua sababu ya kifo cha Bw. Ali na pia kuweza kumbaini mhalifu aliyehusika na kitendo hicho cha mauaji. Hali hii imedhihirika pale mwandishi aliposema:

> Spekta Seif alimtazama Bwana Msa kitambo, kwa vile alivyokuwa akijidai kutikisa kichwa na kujifanya kama ndio kwanza anasikia habari zile na kuona ajabu. Ndipo mwisho alipomuuliza kwa nia, "Lakini kweli kweli, Bwana Msa uliwezaje kufahamu mambo yote haya yaliyomfika Bwana Ali na ukaweza kuyapanga moja moja sawa sawa kama C.I.D. wa hadithini? ... hata mimi mwenye kazi ya polisi nakiri mbele yako kuwa, wewe umenishinda kwa upekuzi na upelelezi wa mambo!" (uk: 85)

Katika dondoo hili tunamuona Bwana Msa akielezwa juu ya umahiri wake katika kazi ya upelelezi ambayo ilisaidia kuondoa utatanishi wa mauaji ya Bw. Ali kwa kugunduliwa na kukamatwa mhalifu aliyehusika. Jambo hili limethibitishwa na Spekta Seif kwa kumuangalia Bwana Msa kitambo, baadaye kumuuliza ni jinsi gani aliweza kufahamu mambo yote hayo. Hatimaye, Spekta Seif anakiri kuwa, Bwana Msa aliweza kuyapangilia mambo kiutaalamu zaidi kama vile, C.I.D na kumshinda yeye ambaye yupo katika kazi hiyo ya polisi.

Kwa jumla, utafiti uligundua miktadha mbalimbali ambayo uforensiki ulifanyika kutokana na matukio ya kihalifu yaliyojitokeza katika maeneo hayo. Miktadha hiyo ni pamoja na; miktadha ya kipolisi, miktadha ya kimahakama (kisheria), miktadha ya kitabibu na miktadha ya kijamii. Miktadha hiyo ilionesha utokeaji wa matukio ya kihalifu kama vile, mauaji na ujambazi, ambayo ililazimika kufanyika uforensiki kwa lengo la kujua chanzo cha tukio na kumpata mhalifu aliyehusika na uhalifu huo. Aidha, licha ya kuwapo kwa juhudi na mikakati mbalimbali ya kupambana na matendo ya kihalifu katika jamii, utafiti ulibaini kuwa, bado serikali inakabiliwa na changamoto kubwa kwa watendaji wake. Kwani, miongoni mwa watendaji hao wa serikali wanaendelea kushirikiana na wahalifu ambao hutenda maovu kadri siku zinavyoendelea. Jambo hili, linaitia doa serikali na kuifanya jamii kukosa imani na viongozi wa serikali hiyo. Wapo viongozi na wanajamii ambao huthubutu kutenda na kusema kuwa, "imefikia wakati sasa kila mtu ale kivyake, uzalendo ulishaondoka miaka mingi ya nyuma" (Mfaume, 2015). Taifa lenye uozo mkubwa kama huu, siku zote hurudi nyuma kimaendeleo

## 4.6 Uhusiano Uliopo Kati ya Uforensiki katika Riwaya na Maisha Halisi ya Jamii

Mojawapo ya malengo ya tasnifu yetu ni kuchunguza uhusiano uliopo kati ya uforensiki katika riwaya na maisha halisi ya jamii. Hapa tumeweza kufanya tathmini na kubaini iwapo taaluma ya uforensiki katika riwaya ina uhusiano au haina uhusiano na maisha halisi ya jamii. Hili ni suala la ulinganishaji ambalo linategemea zaidi muktadha wa kimazingira na kiwakati. Ponera (2014: 39) akizungumzia juu ulinganishaji anasema kuwa, "kulinganisha ni kitendo cha kufanya tathmini ya vitu viwili au zaidi ili kujua ubora, kufanana, na kutofautiana kwavyo". Suala la

kuangalia uhusiano ulipo limeifanya tasnifu hii kujadili kwa muhtasari dhana ya uhalisi tukiongozwa na Nadharia ya Uhalisia.

Uhalisi hurejelea ukweli wa tukio au jambo jinsi lilivyo au lionekanavyo. Uhalisi ni mkondo unaosisitiza usanii wa matukio katika fasihi kama yalivyo katika maisha ya kila siku. Uhalisia kama nadharia ya uhakiki ambayo imetumika katika utafiti huu, inagusia namna ukweli unavyosawiriwa katika nyakati mbalimbali. Usawiri huo, unategemea matukio na miktadha mbalimbali kama tulivyoona kwa waandishi hawa wa riwaya pendwa ambao wameyasawiri maisha ya jamii katika kazi zao.

Uchunguzi wa matumizi ya uforensiki katika utanzu wa riwaya, hususan riwaya pendwa, unaambatana na uhalisi kwa kiasi kikubwa. Hivyo, hapana budi kurejelea mawazo yanayohusishwa na uhalisia, ambapo inasisitiza uhalisi kwa ukamilifu wake. Larkin (1977: 2) alieleza kuwa, mwandishi wa kazi ya fasihi ana lengo la kuwarudisha wanajamii katika ulimwengu wao wa kawaida na kwamba dunia atakayoiumba ni lazima ilandane na ukweli au uhalisi. Lucas (1972: 6) anasisitiza kuwa, kuna uhusiano mkubwa katika kazi ya fasihi na mtazamo wa msanii kuhusu mazingira anamokulia katika uandishi wake. Hivyo, kwa kiasi kikubwa, nadharia hii imesaidia kuonesha uhalisi wa mambo na kuweza kubaini kuwa matumizi ya uforensiki katika riwaya yanalandana na uhalisi wa maisha.

### 4.6.1 Uhusiano wa Uforensiki Kimatukio katika Riwaya na Maisha Halisi ya Jamii

Utafiti umebaini kuwa upo uhusiano mkubwa sana kati ya uforensiki katika riwaya na maisha halisi ya jamii. Hali hii inatokana na ukweli kwamba, vipengele vya matukio ya kisanii yaliyotumika, miktadha iliyobainishwa, wahusika na dhamira

iliyokusudiwa katika riwaya hizo teule zilizotumika katika tasnifu hii, kwa kiasi kikubwa vinaakisi uhalisi wa maisha ya jamii husika kwa namna fulani. Kutokana na vielelezo hivyo vya miktadha (mandhari), wahusika pamoja na matukio ya kihalifu na jinai yalijitokeza ndani ya riwaya hizo yameweza kusibu sifa na tabia zilizomo katika jamii pamoja na mienendo ya wanajamii hao, ambayo hupatikana katika maisha halisi ya kila siku.

Tukirejelea vigezo vitatu vilivyotajwa hapo juu, matukio ya kihalifu katika riwaya za waandishi teule yanaonekana kuwa ya kawaida na yanayohusiana na maisha ya kila siku. Tukio la uhasama na kufarakana kwa Sikujua na rafiki yake Podamali kulilotokana na hasira za mapenzi na tamaa ya fedha kwa Sikujua na kusababisha mauaji ya Pondamali linaakisi maisha halisi ya jamii. Pia, tukio la mauaji ya Bw. Ali katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* (uk: 85) lililofanywa na Mwarabu mgeni kwa sababu ya kumuharibia nyumba yake alipokuwa Kongo pia, linahalisika katika maisha ya jamii tunayoishi kila siku.

Aidha, kuuwawa kwa Mke wa Mheshimiwa Zumo mgombea urais kwa tiketi ya chama tawala. Kulitokana na utashi wa kisiasa uliambatana na imani potofu za kishirikina. Mauaji ya Zumo mwenyewe katika *Mhanga wa Ikulu* yalifanya kwa lengo la kulinda chama na kuficha maovu ya viongozi wa chama hicho. Matukio yote haya yaliyotokea kutokana na sababu mbalimbali, yanaweza kuonekana katika mazingira ya kawaida ya maisha halisi ya kijamii yakiambatana na sababu kama hizo za kimapenzi, kisiasa, tamaa ya kujipatia fedha na cheo.

Kwa mfano, kuuawa kwa Sultan Ali Tani Wete Kisiwani Pemba, Mei 12, 2017 kulisababishwa na wivu wa kimapenzi. Bi. Punje[12] akifafanua kuhusu mauaji hayo alieleza kuwa, ndugu Sultan Ali Tani alichomwa kisu chenye ncha kali na mke wake mkubwa Bi. Rahma Suleiman. Tukio hilo lilifanyika akiwa nyumbani kwa mke wake mdogo, mtaa wa Kizimbani Wete Pemba majira ya saa mbili na dakika thelathini usiku wa kuamkia Jumamosi. Hii ni baada ya kuchelewa kurudi kwa mke wake mkubwa. Ndugu Sultan alikimbizwa katika hospitali ya mkoa kwa ajili ya matibabu. Lakini, kwa bahati mbaya sana, hadi kufikia saa saba usiku alipoteza maisha.

Pia, tukio la kutiwa moto nyumba ya ndugu Suleiman[13] iliyopo Sizini Micheweni Pemba. Tukio hili lilitokana na utashi wa kisiasa, ambopo lilitokea Septemba 19, 2009 wakati wa uandikishaji wa wapiga kura kwa ajili ya uchaguzi mkuu wa 2010. Aidha, tukio la kupigwa ni polisi ndugu Fuchia[14] akiwa nyumbani kwake Chumbuni Zanzibar hadi kupoteza fahamu siku ya Alhamisi Octoba 19, 2000. Hali hii ilitokana na chuki na uhasama wa kisiasa uliopandikizwa na jirani yake, akidai kuwa anakashifu chama na serikali iliyopo madarakani. Jambo ambalo lilisababisha mhanga (muathirika) huyo baada ya kunusurika kufa, kuhama mtaa huo na kuhamia katika eneo la Mikunguni Zanzibar.

[12] Bi. Punje ni mzaliwa wa kijiji cha Kwale Micheweni Pemba, ambaye ndiye alikuwa mke mdogo wa marehe Sultan Ali Tani. Tukio hilo la mauaji limetokea nyumbani mwake. Alifanya mahojiano na mtafiti kwa njia ya simu akiwa nyumbani kwao siku ya siku alhamisi tarehe 24/05 2018, saa kumi na moja na dakika kumi na tano za jioni.

[13] Suleiman Shaame ni naibu wa Sheha mkaazi wa kijiji cha Sizini Wilaya ya Micheweni, akifanya mahojiano na mtafiti nyumbani kwake siku terehe 03/03/2018 saa nne asubuhi.

[14] Fuchia ni mzaliwa Chumbuni Zanzibar, alifanya mahojiano na mtafiti nyumbani kwake Mikunguni Zanzibar siku ya Ijumaa tarehe 30/03/2018 saa nane mchana.

Vilevile, tukio la utoaji na upokeaji wa rushwa (kula rushwa) kwa watendaji wa serikali kama vile, Askari polisi na mahakimu (majaji) katika *Kiu ya Haki* linasawiri hali halisi ya maisha ya binadamu katika jamii. Kwa mfano, kitendo cha kuchukuwa rushwa Inspekta Pwagu na Jaji Pwaguzi kwa ajili ya kumsaidia Sikujua juu ya kesi ya mauaji. Rushwa iliyochukuliwa na polisi wawili katika biashara ya Mzee fundisha; na rushwa iliyotolewa na Meneja wa kampuni ya mkaa kwa askari waliotoboa siri kwa meneja huyo.

Pia, inajitokeza mifarakano na magombano ya kisiasa kati ya viongozi na raia ambayo huwaingiza wanajamii katika uhalifu inaakisi uhalisi wa maisha katika jamii na taifa kwa jumla. Kwa mfano, mifarakano baina ya Farouk na Frank katika *Mhanga wa Ikulu.* Pia, yapo matukio ya ujambazi na uhalifu mwingine kama vile, utekaji nyara na ugaidi yanawakilisha uhalisi wa yale yanayowatokea baadhi ya watu walio wengine katika maisha. Pia, uovu unaojitokeza katika jamii husababisha chuki na mifarakano ambayo huifanya jamii hiyo kukosa amani na utulivu kutokana na matukio ya uovu na dhuluma yanayosababishwa na tamaa mbaya. Kwa mfano, matukio ya wizi katika riwaya ya *Kiu ya Haki* yanaakisi uhalisi katika jamii nyingi, kwani ni matukio ambayo yameenea na hutokea kila mara na kila mahala katika jamii nyingi.

Kwa mfano, ndugu Nassor Suleiman[15] anaeleza tukio la wizi lililomtokea Januari 07, 2004 akiwa safarini kutoka Dar es Salaam kuelekea Zanzibar. Anaeleza kuwa, akiwa katika kituo cha daladala Msimbazi akisubiria usafiri kwa ajili ya kuendelea

[15]Nassor Suleiman ni mjasiriamali ambaye hufanya shughuli zake za biashara ndodondogo kwa kusafiri maeneo tofauti ya Tanzania. Kwa sasa, anaishi katika kijiji cha Tumbe wilaya ya Micheweni Pemba, alifanya mahojiano na mtafiti nyumbani kwake, siku Jumatano tarehe 14/03/ 2018 saa nane mchana.

na safari zake za kibiashara, ghafla alifuatwa na watu wawili ambao walijitambulisha kama wageni na wafanyabiashara ya madini. Punde kidogo, watu wale walikodisha teksi na kumuomba waongozane naye ili awapeleke Kinondoni kwa ajili ya kwenda kufanya biashara hiyo. Hatimaye, wakiwa kwenye gari walimuweka chini ya ulinzi na kumuamuru atoe kila alichonacho, walifanikiwa kuchukua simu mbili na fedha taslimu shilingi za Kitanzania laki tano (Tsh 500,000/=), baada ya hapo walimchukua hadi barabara ya Namanga na kumuachia. Pia, tukio jingine la wizi wa fedha na vitu vingine vya thamani lilimtokea ndugu Nassor dukani kwake katika kijiji cha Tumbe Wilaya ya Micheweni Pemba usiku wa kuamkia Jumapili, Machi 22, 2009 baada ya kuvunjiwa na watu ambao hakuweza kuwatambua.

### 4.6.2 Uhusiano wa Uforensiki Kimuktadha katika Riwaya na Maisha Halisi ya Jamii

Kwa kuirejelea Nadharia ya Uhalisia, utafiti huu umebaini kuwa wahusika pamoja na miktadha iliyotumika kusawiri uforensiki juu ya matukio ya kihalifu yaliyojitokeza katika riwaya pendwa zilizofanyiwa kazi katika tasnifu hii inaakisi uhalisi wa maisha ya kila siku ya wanajamii. Kwa mfano, waandishi hawa wamejaribu kuunda mandhari ya ulimwengu halisi tulionao katika maeneo ambayo yanaweza kufikika na kuthibitika katika jamii. Mathalani, mandhari ya Mlimani City kulikoendeshwa upelelezi na maafisa wa usalama wa taifa ili kumkamata Frank wakati wa makabidhiano ya fedha na Dickson. Pia, kuna mandhari ya Morogoro kulikotokea mauaji ya mgombea urais Mheshimiwa Zumo, akiwa katika mkutano wa kampeni za uchaguzi mkuu uliotarajiwa kufanyika miezi michache ijayo. Aidha, tunaona mandhari ya *Oyterbay* kulikopigwa picha za mauaji ya mke wa Zumo

katika *Mhanga wa Ikulu*. Pia, katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* tunaona mandhari ya Baraste alikotoka Bw. Ali, na hatimaye, kuuwawa akiwa mzimuni wakati akielekea nyumbani kwake. Katika riwaya ya *Kiu ya Haki* kuna mandhari ya kituo cha polisi Ilala ambako Mzee Toboa alipeleka taarifa kamili kwa Inspekta Paukwa juu ya mauaji ya Pondamali. Mandhari zote hizi ambazo waandishi wamezitumia katika kazi zao ni mandhari halisi ambazo zinadhihirika katika maisha halisi ya jamii ya Tanzania.

Kwa upande wa wahusika, masuala yanayohusu kuwapo kwa utii kwa raia dhidi ya serikali na taifa kwa jumla ni jambo la muhimu. Suala hili linaonekana katika matendo ya Mzee Toboa wa *Kiu ya Haki* ambaye ilikuwa akipingana na kila tendo la uovu lililokuwa likitendeka katika jamii yake. Alipambana kila hali ili kudhibiti uhalifu na uovu huo usiendelee kutokea katika jamii yake. Hivyo, kwa mujibu wa misingi ya uhalisia ambayo inajaribu kuwasilisha maisha jinsi yalivyo kwa uhuru na demokrasia, inaonekana Mzee huyu anawakilisha binadamu (raia wema) katika jamii, ambao hupenda maendeleo ya jamii zao.

Pia, Bwana Msa na Najum katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* wanaonesha utii kwa jamii zao na serikali. hii ni kwa sababu walifuata maelekezo ya jamii kwenda kumuangalia Bw. Ali katika safari yake. Pia, tunaona pale wanapotoa taarifa katika vyombo vya usalama na upelelezi baada ya kugundua tukio la uhalifu na kuungana na polisi katika kutafuta chanzo cha uhalifu huo. Kwa mantiki hiyo basi, wahusika hawa wanawakilisha watu wenye utii kwa taifa lao. Katika maisha halisi, watu kama hawa wanakuwepo ingawa ni wachache mno na ni vigumu sana kuweza kuwatambua waziwazi. Hii ni kwa sababu ni watu ambao huhifadhiwa kwa

kutunzwa siri zao na vyombo husika vya serikali ili zisitoke nje katika jamii kwa kuhofu kuwafikia wanajamii wengine ambao hawana nia njema na taifa lao.

Aidha, wahusika kama vile, Frank, Dickson, Cobra, Nge na Farouk katika *Mhanga wa Ikulu* ni watu wanaonekana kutenda mambo kwa ajili ya kutafuta na kulinda maslahi binafsi. Wanafanya hivyo huku wakiliweka taifa na watu wake katika taharuki na mshangao mkubwa. Katika hali ya maisha ya kawaida, wapo watu katika jamii ambao wanatenda mambo kwa ajili ya kujijali wao wenyewe tu bila kujali na kuthamini utu wa mtu. Kwa muktadha huo, watu hao hudiriki kuwafanyia unyama na ukatili watu wengine wanaowajua na hata wasiowajua katika jamii ama taifa wanaloishi.

Kadhalika, wahusika kupitia riwaya zote teule zilizotumika katika tasnifu hii wamebainika kuwa, wahusika hao na matukio ya kihalifu yaliyojitokeza yana uhalisi kwa namna walivyochorwa na kubebeshwa matukio hayo. Kwa mfano, matukio kama vile, ujambazi, mauaji, wizi na rushwa yanahalisika na hutokea mara kwa mara katika jamii. Aidha, wahusika wa kihalifu katika riwaya hizo, mienendo na tabia zao za kihalifu zinawakilisha wahalifu katika jamii halisi ya Tanzania. Kwa mfano, matukio ya ujambazi yaliyofanywa na wahusika Killa, Somba na Kazamoyo yapo na yameenea katika jamii ya Watanzania. Wapo watu wa kawaida waliowahi kukutwa na matukio kama hayo katika mazingira tofauti. Pia, matukio juu ya uadui na mifarakano ya kimapenzi, kisiasa yanawatokea watu walio wengi na kila leo katika jamii ya sasa.

Kwa mfano, Ali Kassim[16] anasimulia tukio la ujambazi lililomtokea Mei 30, 2013 nyumbani kwake; kwamba, siku ya Alhamisi mnamo saa tano za usiku akiwa nyumbani kwake alivamiwa na majambazi wanne wakiwa na silaha za moto. Jambo hili lilimpa mshituko mkubwa. Hii ni kwa sababu tukio kama hilo halijawahi kutokea kijijini hapo uhai wa maisha yake yote aliyopata kuishi. Anaeleza kuwa, alijaribu kupambana nao akiwa pamoja na mke wake lakini walizidiwa nguvu na kujeruhiwa vibaya hadi kupoteza fahamu. Hivyo, majambazi hayo yalifanikiwa kuiba vitu mbalimbali pamoja na fedha taslimu shilingi milioni tatu za Kitanzania (Tsh, 3,000,000/=).

Aidha, tuliona tukio lililotokea Septemba 29, 2017 la mazombi[17] kumteka nyara na kumpiga hadi kusababisha kifo cha aliyekuwa kaimu mwenyekiti wa CUF jimbo la Mto Pepo, na Mkurugenzi wa Habari na Uenezi wa CUF wilaya ya Magharibi Zanzibar, ndugu Ali Juma Suleiman. Pia, tuibaini tukio la mauaji ya januari 26/27, 2001 lililotokana na maandamano ya kisiasa Zanzibar yaliyoitishwa kwa madhumuni ya kupinga matokeo ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2000.

Kwa jumla, matendo na miktadha ya kihalifu iliyobainishwa katika riwaya teule yanapaswa kufanyiwa uforensiki kwa lengo la kumpata mhalifu. Utafiti umebaini kuwa, matendo na miktadha hiyo ambayo huwakilisha wahusika katika uhusika wao ndani ya riwaya hizo, yamechota uhalisi wa jamii hasa ya Tanzania Bara na visiwani

[16] Maelezo hayo yametolewa na ndugu Ali Kassim mwenye umri wa miaka (57) wakati akifanya mahojiano na mtafiti nyumbani kwake Tumbe siku ya Jumamosi tarehe 11/03/ 2018 saa kumi na moja kamili jioni (11: 00).

[17] Mazombi ni kikosi maalumu kilichopo Zanzibar, kinachozunguka mitaani na kufanya unyama na ukatili mkubwa kwa watu wasiounga mkono chama tawala (CCM), hususani viongozi na wafuasi wa upinzani. Kikosi hiki hakipo kisheria, kwani hata serikali wanadai hawakitambui, ila kwa upande wa upinzani wanaona kimeratibiwa na kipo ndani ya serikali.

Zanzibar. Hii ni kwa sababu, matukio, falsafa na ujumbe unaojitokeza katika kazi hizo pamoja na wahusika wake wana uhalisi kulingana na mazingira ya Tanzania. Pia, fikra na falsafa zao zinalingana na jamii husika.

### 4.7 Muhtasari wa Sura ya Nne

Sura hii imeanza kwa kuangalia historia fupi za waandishi teule. Imefafanua kwa muhtasari riwaya za waandishi teule hao; ambapo kwa Muhammed Said Abdulla ni *Mzimu wa Watu wa Kale*, kwa upande wa Beka Mfaume ni *Mhanga wa Ikulu* na kwa Zainab M. Mwanga ni *Kiu ya Haki.* Misingi ya Nadharia ya Uhalisia ilitumika katika uwasilishaji na uchambuzi wa data. Matukio mbalimbali ya kihalifu kama vile, mauaji, ujambazi, wizi, rushwa na utekaji nyara yamechanganuliwa. Miktadha katika riwaya ambayo husababisha kufanyika kwa uforensiki kama vile, muktadha wa kipolisi, muktadha wa kitabibu, muktadha wa kisheria na muktadha wa kijamii pia imebainishwa na kufanyiwa uchambuzi. Aidha, Nadharia ya Uhalisia imetumika kutathmini na kujadili uhusiano wa uhalisi uliopo kati ya uforensiki katika riwaya na maisha halisi ya jamii. Hapa tuliweza kutumia vigezo vitatu vya msingi ambavyo ni matukio, miktadha na wahusika waliotumiwa na waandishi wa riwaya hizo. Sura inayofuata inahusu muhtasari, mapendekezo na hitimisho la utafiti.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii inahusu muhtasari wa utafiti, hitimisho la utafiti, mchango na mapendekezo mbalimbali yaliyopatikana kwa tafiti zijazo kutokana na namna na matokeo ya utafiti huu.

## 5.2 Muhtasari wa Utafiti

Utafiti huu ulilenga kuchunguza Uforensiki katika Riwaya Pendwa ya Kiswahili: Mifano kutoka katika *Mzimu wa Watu wa Kale, Mhanga wa Ikulu* na *Kiu ya Haki.* Utafiti huu ulifanyika katika mkoa wa Dar es Salaam na Dodoma kwa upande wa Tanzania bara na mkoa wa Mjini Magharibi kwa Unguja na mikoa miwili ya Pemba. Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa kuchunguza uforensiki katika riwaya pendwa ya Kiswahili katika riwaya teule. Tasnifu ina jumla ya sura tano.

Sura ya Kwanza imeonesha dira ya utafiti, kwa kutoa fasili na ufafanuzi wa dhana muhimu zilizotumika katika utafiti kama vile, fasili ya uforensiki, riwaya, riwaya pendwa, upelelezi, ushahidi na DNA, zilifafanuliwa kwa ufupi ili kutoa mwongozo mzuri wa utafiti. Aidha, sura imeelezea masuala yahusuyo usuli wa tatizo la utafiti, tamko la tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti na mwisho ni manufaa ya utafiti.

Sura ya Pili ilizungumzia mapitio ya maandiko ambayo yalihusisha maandiko tofauti yanayohusiana na mada ya utafiti huu. Maandiko hayo ndiyo yaliyokuwa mwega katika mchakato wa kubainisha mapengo ya utafiti yaliyojitokeza katika maandiko mbalimbali na kutoa fursa ya kuipigia mbizi dhana hii ya uforensiki

katika riwaya pendwa za Kiswahili. Maandiko hayo yaligawanywa katika sehemu mbili ambazo ni maandiko yaliyohusu riwaya pendwa na maandiko yaliyohusu uforensiki. Pia, katika sura hii lilizungumziwa pengo la utafiti pamoja na kiunzi cha nadharia ambacho kilihusiana na nadharia ya uhalisia kama nyenzo kuu iliyotumika katika kuchakata na kuchambua data za utafiti huu.

Sura ya Tatu imeelezea methodolojia ya utafiti ambayo imehusisha usanifu wa utafiti, walengwa wa utafiti, jamii ya watafitiwa, sampuli ya watafitiwa na upatikanaji wake na eneo la utafiti. Pia, imefafanua itikeli za utafiti ukusanyaji wa data, vifaa au zana za kukusanyia data, mbinu za ukusanyaji data kama vile, mahojiano, udodosaji na mapitio ya maandiko, mchakato wa ukusanyaji data na udhibiti wake. Vilevile, ilizungumzia uhalali na uthabiti wa matokeo ya utafiti, uchanganuzi na uwasilishaji wa data, mipaka ya utafiti na changamoto za utafiti, pamoja na mpango wa ripori ya tasnifu, sampuli iliyotumika pamoja na namna data zilivyokusanywa na kuchambuliwa.

Sura ya Nne ilihusu uwasilishaji na mjadala wa matokeo ya utafiti. Sura hii ilianza kwa kufafanua muhtasari wa waandishi teule ambao ni Muhammed Said Abdulla, Beka Mfaume na Zainab M. Mwanga. Pia, imefafanua kwa muhtasari riwaya za waandishi teule ambapo kwa Muhammed Said Abdulla ni *Mzimu wa Watu wa Kale*, kwa Beka Mfaume ni *Mhanga wa Ikulu* na kwa Zainab M. Mwanga ni *Kiu ya Haki.* Aidha, tuliweza kubaini na kuchanganua matukio mbalimbali ambayo husababisha kufanyika kwa uforensiki katika riwaya teule kama vile tukio la wizi, mauaji, ujambazi, rushwa na utekaji nyara. Kadhalika, miktadha mbalimbali ambayo taaluma ya uforensiki inafanyika pia imechanganuliwa. Vilevile, misingi ya

Nadharia ya Uhalisia ilitumika katika kuchanganua na kujadili matukio na miktadha ambayo hufanyika kwa uforensiki katika riwaya hizo teule.

Kadhalika, misingi hiyo ya Uhalisia iliweza kutumika katika kutathmini na kuangalia uhusiano uliopo wa kiforensiki katika riwaya na maisha halisi ya jamii. Sura ya Tano inayohusu muhtasari, mapendekezo na hitimisho la utafiti. Imeelezea utangulizi, muhtasari wa tasnifu, utoshelevu wa nadharia ya uchambuzi wa data na mjadala wa matokeo ya utafiti, mchango mpya ulioibuliwa katika utafiti huu pamoja na mapendekezo kwa tafiti zijazo.

## 5.3 Hitimisho

### 5.3.1 Mchango Mpya wa Utafiti

Mchango wa pekee wa utafiti huu katika uwanja wa kitaaluma ulitokana na uchambuzi wa data zilizokusanywa ambazo zilitokana na malengo mahsusi ya utafiti huu. Dhana hii ya uforensiki imeonekana kuwa dhana mpya kwa wanajamii walio wengi. Pia, baadhi ya waandishi wa kazi za kifasihi hawakuizamia kwa kina taaluma hii ya uforensiki katika kazi zao. Hivyo, waandishi hao hukitumia kipengele hiki kama kionjo tu cha kifani katika kazi zao bila kudhihirisha umuhimu wake kwa jamii na taifa kwa jumla. Utafiti huu umechambua na kuweka wazi dhana hii ya uforensiki na umuhimu wake katika jamii kwa kuangaza matukio ya kihalifu, miktadha pamoja na uhusiano katika uhalisi wa maisha ya kila siku na harakati za kimaendelo. Kimsingi, taaluma hii ina umuhimu mkubwa kwa jamii, hivyo wanafasihi wanapaswa kuiangalia kwa umakini mkubwa na kuizamia kwa undani wakati wanapoandika kazi zao kwa lengo la kuinufaisha na kuielimisha jamii wanayoiandikia.

### 5.3.2 Utoshelevu wa Nadharia Iliyotumika

Nadharia ya Uhalisia ndiyo iliyotumika katika kukusanya, kuchambua data na kuendesha mjadala wa matokeo ya utafiti. Uchambuzi wa data umejiegemeza zaidi katika msingi wa kwanza na wa tatu wa nadharia hii ambapo iliangalia matendo na miktadha mbalimbali ambayo matendo ya kihalifu hutokea na kusababisha kufanyika uforensiki katika kufichua na kuwapata wahalifu wa matukio hayo katika jamii. Pia, misingi hii ilisaidia kuchunguza na kutathmini kwa lengo la kuona uhusiano uliopo wa kiforensiki katika riwaya na maisha halisi ya jamii, ambayo anapambana nayo katika mazingira yake anayoishi kila siku. Aidha, msingi huu umesaidia kufahamu kuwa uforensiki ni ufundi wa kisanaa uliotumika ndani ya sanaa kuu ya utunzi wa riwaya pendwa ambapo, umewezesha kubaini kwamba, tungo bunilizi ambazo zinatumia uforensiki hulenga kuweka wazi hisia za ndani za mtunzi wa bunilizi hiyo. Hisia ambazo, kwa kiasi kikubwa, hutokana na matukio halisi yanayotokea katika jamii ama taifa.

Kwa jumla, utafiti ulibaini kuwa, Nadharia ya Uhalisia ilikuwa ni mwafaka kutumika katika kuchunguza uforensiki katika riwaya pendwa hizo. Kwa kule kuangaza matukio ya kihalifu/jinai na miktadha ya utokeaji wa matukio hayo, na jinsi waandishi wa bunilizi teule walivyoyasawiri katika kazi zao hizo kwa ubunifu mkubwa wakiwa na lengo la kufikisha ujumbe utakaoleta athari chanya katika maisha halisi ya jamii.

## 5.4 Mapendekezo ya Tafiti Zijazo

Msingi mkuu wa tasnifu hii ulikuwa ni kuchunguza uforensiki katika riwaya pendwa za Kiswahili. Matokeo ya utafiti yamebainisha kuwa, upo umuhimu mkubwa wa

kitumika kipengele hiki cha kifani katika riwaya pendwa za Kiswahili kwa lengo la kuonesha changamoto na athari zinazoikumba jamii dhidi ya matukio mbalimbali ambayo hutokea katika jamii hizo kila leo. Kwa mantiki hiyo basi, mtafiti anapendekeza kufanyike tafiti nyingine zenye mwelekeo kama huu na uwe katika kipengele cha uforensiki ili dhana hii iweze kueleweka zaidi kwa jamii. Ijapokuwa waandishi wa kazi za kifasihi hukitumia kipengele hiki, bado hawajaonesha matumizi na umuhimu wake kwa jamii wanazoziandikia. Pia, zifanyike tafiti ambazo zitachunguza dhamira za waandishi kutumia uforensiki katika kazi zao za kifasihi, hasa katika riwaya za pendwa. Sambamba na hayo, watafiti wengine wanaweza kutazama sababu zinazochangia kuzuka kwa matukio yanayohitaji kufanyika kwa uforensiki katika jamii.

### 5.5 Muhtasari wa Sura ya Tano

Sura hii imehusisha muhtasari, mapendekezo pamoja na hitimisho la tasnifu. Sura hii pia imezungumzia juu ya utoshelevu wa nadharia iliyotumika katika utafiti huu. Vilevile, imeelezea mchango mpya wa utafiti kulingana na utafiti ulivyobaini, yakifuatiwa na mapendekezo yaliyotokana na tasnifu yetu. Sehemu inayofuatia ni yenye marejeleo, ikifuatiwa na taarifa nyinginezo zinazohusisha viambatanisho kama vile, maswali ya makundi tofauti yaliyotumika katika utafiti huu.

## MAREJELEO


Abdalla, M. S. (1960). *Mzimu wa Watu wa Kale*. Tanzania. Publishing House, Dar es Salaam.

Ashoka. (2007). *Forensic Science and Police Science Theory and Practice.* India: Sudha Publication India.

BAKIZA. (2010). *Kamusi la Kiswahili Fasaha*. Oxford University Press, Dar es Salaam.

Bryman, A. (2004). *Social Research Methods (2nd Edition)*, Oxford University Press, Oxford.

Chuachua, R. (2010). Suala la Itikadi katika Riwaya za Shaaban Robert (Tasnifu kwa ajili ya mahitaji ya Shahada ya Umahiri, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.

Digamba, P. (2015). Novel Digital Forensic Framework for Cloud Computing Environment. (Thesis Submitted in Partial Fulfillment of the Requirements for the Degree of Doctor of Philosophy). BITS Pilan.

Duvall, N. E. (2013). Forensic Medicine in Scotland 1914-39. (Thesis Submitted to the Degree of Doctor of Philosophy in the Faculty of Life Sciences). University of Manchester.

Harris, D. (2007). *Forensic Science: Distance Learning Presentation for King DrewMagnet High School of Medicine and Science*, (haijachapishwa).

Jordan, S. N. (2002). Forensic Linguistic: The Linguestic Analyst and Expert witness of Language evidence in Criminal Trials. (Thesis Presented in Partial Fulfillment of the Requirements for the Degree Master of Arts in Applied Linguistic). Baola Univesity.

Kimura, E. (1992). *Mabadiliko ya Kijamii na Riwaya ya Upelelezi.* Tanzani Institute for the Study of Language and Cultures of Asia and Africa (ILCAA).

Kothar, C. R. (2009). *Research Methodology*: *Methods and Techniques.* New Delhi: New Age Internatinal (P) Ltd. Peblishers.

Kothari, C. R (2004), *Research Methodology, Methods and Techniques, Second Edition*, New Age International (P) Ltd.Delhi.

Larkin, M. (1977), *Man and Society in the Nineteenth Century Realism*, Macmillan Press, London.

Levi, G. (1975). *Mpelelezi Hodari na Genge la Wahalifu*. Nairobi: Kenya Literatu Bureau.

Lucas, G. (1972), Studies in European Realism. *A Sociological Survey of Writtings of Balzac, Stredhal, Zola Tolistoy, Gorki & Others,* Marlin Press, London.

Madumulla, J. S. (1988). *Riwaya ya Kiswahili (Tanzania) katika Miaka ya Themanini*, DSM. TUKI.

Madumulla, J. S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi*. Dar es Salaam: Mture Education Publisher Ltd.

Makata, A. (2011). *The Standard Operating Procedure (SOP) for Medical Forensic Practitioners, Investigation Authorities and Prosecutors in Zanzibar*. Zanzibar: Office of the Director of Public Prosecutions.

Mazongela, K. S. S. (2015). Matumizi ya Utanzia katika Riwaya Pendwa ya Kiswahili: Ulinganisho wa Riwaya ya Ben Mtobwa na Hussein Tuwa. (Tasnifu ya Kukamilisha Mahitaji ya Shahada ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili, Haijachapishwa), Chuo Kikuu Dodoma.

Mbarouk, J. M. (2015). Athari za Sayansi na Teknolojia katika Hadithi za Watoto: Mifano yaNgano Kutoka Wilaya ya Micheweni Pemba (Tasnifu kwa ajili ya mahitaji ya Shahada ya Umahiri sayansi na jamii katika fasihi ya Kiswahili, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.

Mfaume, B. (2015). *Mhanga wa Ikulu*. Dar es Salaam. Tuwakadabra Production

Mlacha, A. K na Madumulla, J. S. (1991). *Riwaya ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Mlacha, S. A. K (2004), *Kiswahili na Vyombo vya Habari*. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Dar es Salaam.

Mulokozi, M.M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria Tanzania.

Mwanga, Z. M. (2004). *Kiu ya Haki*. Dar es Salaam: Ruvu Publisher Ltd.

Nabar, B. S. (2002). *Forensic Science in Crime* Inverstigation. Delhi: Nallakunta S. P. GOGIA (H.U.F)

NIJ.(2015). *The Impact of Forensic Science: Research and Development.* Washington. DC.

Ntarangwi, M. (2004). *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*. PhD Thesis, Augustana College: Rock Island.

Ponera, A. S. (2010). Ufutuhi katika nathari za Shaaban Robert: Maana yake, sababu za kutumiwa, na athari zake kwa wasomaji, (Tasnifu ya Shahada ya Umahiri, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma

Ponera, A. S. (2014). *Utangulizi wa Nadharia ya Fasihi Linganishi*. Dar es Salaam: Karljamer Print Tecnology.

Saffar, A. J. (2006). *Mashtaka ya Jinai na Utetezi*. Dar es Salaam: UWAVITA

Samweli, M. (2015). *Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salam: MEVEL Publishers.

Sanga, A. N. (2012). Ujumi katika Riwaya Pendwa ya Kiswahili: Mifano kutoka kwa MSA na Aristablus Alvis Musiba. (Tasnifu ya Kukamilisha Mahitaji ya Shahada ya Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili, Haijachapishwa), Chuo Kikuu Dodoma.

Senkoro, Fikeni E. M. K. (1982). *Fasihi*. Dar es Salam: Press and Publicity Center.

Sharma, B. R. (2003). *Forensic Science in Criminal Inverstigation and Trials.* New Delhi: Universal Law Publishing Co. Pvt. Ltd.

Silverman, B. (2011). Research and Development in Forensic Science: a Review. www.homeoffice.gov.uk.agencies.public-bodies/fsr

Sumary, J. J. (2013). Riwaya ya Upelelezi na Mabadiliko ya Kijamii. (Tasnifu ya Kukamilisha Mahitaji ya Shahada ya Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili, Haijachapishwa), Chuo Kikuu Dodoma.

TUKI (2004*). Kamusi ya kiswahili sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.

Wafula, R. M. na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya fasihi*: *Istilahi na nadhari*. Nairobi: Focus Publishers.

# VIAMBATISHO

## Kiambatisho Na.1: Hojaji kwa Wanafunzi wa Vyuo Vikuu Wanaosoma Fasihi ya Kiswahili

Tunafanya utafiti kuhusu uforensiki katika riwaya pendwa ya Kiswahili. Utafiti wetu unalenga kuchunguza Uforensiki katika riwaya pendwa ya Kiswahili katika riwaya teule ambazo ni *Mzimu wa Watu wa Kale*, *Mhanga wa Ikulu* na *Kiu ya Haki*. Tafadhali tunaomba ushirikiano wako katika kujibu maswali yetu.

**Sehemu A: Taarifa za Mtafitiwa**

Jina la mtafitiwa ………………………..……………

Mahala pa Utafiti ……………………..………………

Tarehe ya Kutolewa Dodoso …………………………

**Sehemu B: Maswali**

1. Je unafahamu nini kuhusiana na uforensiki?

………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………
.

2. Je ni matukio ya aina gani yanayojitokeza katika jamii ambayo yanahitaji kufanyiwa uforensiki?

………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………
.

3. Ni sababu gani unahisi zinachangia kutokea kwa matukio ya uhalifu na jinai?

4. Je unadhani kuwa mhalifu anaweza kugunduika bila kufanya uchunguzi?

5. Nini madhara ya kutokufanya uchunguzi (upelelezi) wakati panapotokea tukio la uhalifu katika jamii?

……………….………………………………………………………………………..…

……………………………………………………………………………………….

6. Je ni nani wanapaswa kufanya uchunguzi wakati panapotokea tukio la uhalifu?

7. Kwa namna gani jamii inaweza kushirika katika kupunguza uhalifu?

8. Eleza ni upi mchango wa wanafasihi/ wasanii katika kupambana na uhalifu katika jamii?

…………………………………………………………………………………………
...………………………………………………………………………………………
…...……………………………………………………………………………………
……

9. Kuna uhusiano gani kati ya taaluma ya uforensiki katika riwaya na maisha halisi katika jamii.

…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………

10. Nini maoni yako kwa waandishi wa kazi za fasihi katika matumizi ya kipengele hiki cha kiforensiki katika kazi zao?

…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
.

**Kiambatisho Na.2: Mwongozo wa Hojaji kwa Wanajamii**

Sehemu hii inahusu baadhi ya maswali ambayo yatamwongoza mtafiti wakati wa mahojiano yake na watafitiwa. Vilevile, wakati wa mahojiano hayo, mtafiti anaweza kubadili kwa kuongeza, kupunguza na kurekebisha maswali hayo kwa lengo la kupata ufanisi zaidi. Baadhi ya maswali hayo ni kama yafuatayo:

1. Kwa mawazo yako uforensiki ni nini? Unashughulika na mambo gani?

2. Je ni matukio gani ambayo husababisha kufanyika kwa uforensiki katika jamii?

3. Uhalifu ni nini?

4. Je, ni sababu gani/zipi ambazo huchangia kutokea kwa matukio hayo ya kihalifu ambayo huhitaji kufanyika kwa uforensiki katika jamii?

5. Mara nyingi wapelelezi huwa wanaharakia kufika katika eneo la tukio lilipotokea. Je kwenda katika eneo hilo kunasaidia nini katika uchunguzi wao?

6. Kwa maoni yako unadhani tufanye nini ili kupunguza uhalifu na jinai katika jamii zetu?

7. Ni katika miktadha ipi hasa ambayo taaluma ya uforensiki hufanyika. Itaje?

8. Kwa maoni yako wasanii wakiwemo wanafasihi unadhani wanamchango wowote katika kupambana na uhalifu katika jamii?

**Kiambatisho Na. 3: Mwongozo wa Hojaji kwa Wataalamu kama vile Wanasheria, Polisi na Madaktari**

1. Nini maana ya uforensiki?

2. Je ni matukio gani ambayo hushughulikiwa katika taaluma ya uforensiki?

3. Ni matukio ya aina gani ya kihalifu ambayo hutokea mara kwa mara katika eneo lako?

4. Je ni kwa namna gani mhalifu anaweza kutambuliwa katika jamii?

5. Je ni vifaa gani vya kisayansi ambavyo hutumika katika uchunguzi?

6. Ni katika mikitadha ipi taaluma ya uforensiki hufanyika?

7. Mara nyingi wapelelezi huwa wanaharakia katika eneo la tukio lilipotokea. Je kwenda katika eneo hilo kunasaidia nini katika uchunguzi wao?

8. Ni vitu gani vinaweza kutumika kama ushahidi katika kumgundua na kumpata mhalifu?

9. Kuna changamoto gani zinazowakabili katika kupambana na uhalifu na jinai katika jamii?

10. Je kuna ushirikiano wowote munaoupata kutoka katika jamii wakati wa kupambana na wahalifu na uhalifu?

11. Je ni njia gani tunapaswa kuzifuata kama wanajamii ili tuweze kupunguza uhalifu na jinai katika jamii zetu?

12. Kwa maoni yako tufanye nini ili kupunguza uhalifu na jinai katika jamii zetu?

13. Fafanua uhusiano uliopo kati ya taaluma ya uforensiki katika riwaya na maisha halisi katika jamii.

**Kiambatisho Na.4: Mwongozo wa Udurusu wa Maandiko**

Mwongozo ufuatao umetumiwa na mtafiti kama dira katika udurusu wa maandiko tofauti yakiwemo maandiko ya riwaya teule.

a) Mtafiti alipitia maeneo yafuatayo kwa ajili ya kufanya udurusu wa maandiko kwa kupitia tasnifu na vitabu mbalimbali kwa lengo la kupata maarifa na rejea muhimu juu ya mada husika ya utafiti.

i) Chuo Kikuu cha Dodoma

ii) Chuo Kikuu cha Waislamu cha Morogoro

iii) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na

iv) Maktaba kuu ya Zanzibar

b) Kufanya uchambuzi wa riwaya teule

i) Kukusanya riwaya teule na kuzisoma

ii) Kufafanua matukio mbalimbali yanayosababisha kufanyika kwa uforensiki na

iii) Kubainisha miktadha mbalimbali ambayo taaluma ya uforensiki hufanyika.

**Kiambatisho Na. 5: Picha Mbalimbali za Utafiti**



**Picha Na. 1:** Kushoto ni mtafiti akiwa pamoja na mwalimu wa fasihi ya Kiswahili shule ya sekondar Tumekuja ndugu Massoud Aly nyumbani kwake Bububu akifanya mahojiano naye (Utafiti, 2018)



**Picha Na.2:** Kulia ni mtafiti akiwa pamoja na wanafunzi wa mwaka wa kwanza wa shahada ya Umahiri katika Fasihiya Kiswahili (MAKL) Chuo Kikuu cha Dodoma baada ya mahojiano ya utafiti (Utafiti, 2018).



**Picha Na. 3:** Kulia ni mtafiti akiwa pamoja na ndugu Fuchia Rashid nyumbani kwake Mikunguni Zanzibar siku ya tarehe 30/03/2018 wakati wa mahojiano ya utafiti huu (Utafiti, 2018).

THE UNIVERSITY OF DODOMA
DEPUTY VICE CHANCELLOR ACADEMIC, RESEARCH & CONSULTANCY
OFFICE OF GRADUATE STUDIES AND CONTINUING EDUCATION
P.o. BOX 259, DODOMA, TANZANIA.
Tel: +255 26 23 10173; Fax: +255 26 23 10005; Email: graduate@udom.ac.tz; website: www.udom.ac.tz

**REF:** UDOM/GRF/13 Vol. VI/89

Thursday, 23rd August 2018

Permanent Secretary,
Second President Office,
P. O. Box 239,
**ZANZIBAR.**

**RE: INTRODUCING MR. KOMBO F. JUMA**

The above named candidate is enrolled at the University of Dodoma for the degree of Master of Arts in Kiswahili Literature with registration number HD/UDOM/232/T.2016.

As an essential requirement of the study programme, each candidate is required to submit a dissertation report on a research undertaken within an industry and supervised by a member of the University's academic staff. Where possible the research should relate to a practical situation in an organisation or firm selected by the candidate. Candidates are expected to use their own initiative to identify a possible research and negotiate access with a local firm or organization.

The above named candidate has developed the proposal titled ***"UFORENSIKI KATIKA RIWAYA PENDWA YA KISWAHILI: MIFANO KUTOKA MZIMU WA WATU WA KALE, MIIANGA WA IKULU NA KIU YA HAKI"*** which has been approved for data collection. The work may take the form of a survey, ethnography, case studies, etc. Where the research may contain confidential information and its publication could be harmful to the organization, confidentiality is assured by the University. Such reports will be seen only by the Supervisor and Examiner for examination purposes.

I would be grateful if you would provide the candidate with this opportunity to facilitate his Studies while at the same time gaining some useful inputs for your own organization through the results of the research report.

THE UNIVERSITY OF DODOMA
DIRECTOR
23 AUG 2018
P.O. Box 259, DODOMA
GRADUATE STUDIES AND CONTINUING EDUCATION

Sincerely,

Said A. Ibrahimu
**For: Director, Graduate Studies and Continuing Education**

**C. c:** Director, GS&CE